ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani
12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais.
13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
17.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/\Jimbo la Jang'ombe
18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni

19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni
23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
32.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais

37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
56.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
57.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
58.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
59.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
60.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
61.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
62.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
66.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
67.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
68.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
69.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
71.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
72.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Kumi na Sita - Tarehe 6 Juni, 2014

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 50

Kupatiwa Msaada Kwa Shule Ya '*Ali Khamis Camp*'

Mhe. Jaku Hashim Ayoub (Kny. Mhe. Saleh Nassor Juma) - Aliuliza:-

Skuli ya Jeshi la Wananchi iliyopo Vitongoji (*ALI KHAMIS CAMP*) ni skuli inayosaidia sana kutoa taaluma kwa watoto wa wananchi wa Wilaya nzima ya Chake Chake.

Kwa kuwa skuli hii inamilikiwa na Jeshi letu na imejikita zaidi kutoa huduma ya elimu kwa vijana wetu, kwa kuwa hivi karibuni wana mpango wa kuanzisha Sekondari na huku wakiwa na mazingira magumu kifedha.

(a) Je, ni lini serikali itawapa moyo wapiganaji wetu kwa angalau kuwajengea banda moja la skuli.
(b) Kwa kuwa Makamu wa Kwanza na Makamu wa Pili wa Rais wameshakwenda kuona juhudi za jeshi letu, ni lini serikali itampeleka Rais kwenda kuona juhudi hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 50, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:- Nakubaliana na Mhe. Mwakilishi, kuwa Skuli ya Msingi iliyoko katika eneo la Kambi ya Jeshi ya *Ali Khamis Camp* huko Vitongoji imesaidia sana katika kutoa elimu kwa watoto wetu wa maeneo ya karibu ya Kambi hiyo. Hivi sasa, Skuli hiyo ina majengo mawili yaliyokamilika, yaliyo na madarasa 8, Chumba cha Mwalimu Mkuu, Chumba cha Walimu na Ghala. Pia, inaendelea na ujenzi wa jengo la vyumba 3. Wizara ilishirikiana na Jeshi la Wananchi wa Tanzania katika kukamilisha ujenzi wa jengo la mwanzo ambapo Jeshi la Wananchi wa Tanzania walianza ujenzi na wizara ikatoa mchango wa kumaliza jengo hilo. Vile vile, wizara imetoa mwalimu mmoja anayefundisha katika skuli hiyo, wengine ni walimu waajiriwa wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ninatoa pongezi zetu za dhati kwa uongozi wa Kambi ya Jeshi ya *Ali Khamis Camp* kwa juhudi zao za kutoa elimu, ninawaahidi kuendelea kushirikiana nao katika kuiendeleza skuli hiyo katika ngazi ya juu zaidi ikiwemo sekondari. Baada ya maelezo hayo sasa napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi kama hivi ifuatavyo:-

a) Wizara iko tayari kushirikiana na Jeshi la Wananchi wa Tanzania katika ujenzi wa majengo ya madarasa ya sekondari kwa utaratibu uliopo ambapo wananchi na wanajeshi wanapaswa kuanza ujenzi na wizara itamalizia itakapofikia hatua za mwisho. Wizara inatoa mchango pindipo tu skuli hiyo itaaendelea kusomesha wanafunzi bila ya malipo.
b) Kiutaratibu, uongozi wa Jeshi la Wananchi ndio wenye wajibu kuwasilisha maombi ya kutaka kiongozi wa Kitaifa kama vile Mhe. Rais wa Zanzibar kutembelea skuli yao.Wizara inaahidi italizingatia ombi hilo na kulifikisha kwa Mhe. Rais, pindipo tu uongozi wa Jeshi utawasilisha ombi hilo rasmi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, kwa kuwa amekiri kuwa skuli hiyo imesaidia sana vijana katika elimu, katika mwaka huu wa fedha serikali hii imetenga kiasi gani kusaidia wizara hiyo ili kupata elimu bora katika skuli hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, wizara mwaka huu bado haijatenga pesa kwa kuisaidia skuli moja tu, imetenga pesa kwa kusaidia skuli zote ambazo wananchi wamezianza na wizara tunatakiwa tuzimalize skuli hizo. Kama nilivyozungumza katika jibu langu mama kuwa skuli hii kama wizara tumeisaidia sana, ilipoanzisha jengo lake la kwanza walianza sisi tukamaliza, jengo hili la pili wameanza wakitukabidhi, basi na sisi tutaendelea na utaratibu kama tunavyofanya katika skuli nyengine.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Spika, na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Katika mukhtaz huo huo wa kuzisaidia skuli kumalizika kujengwa. Je, Mhe Naibu Waziri, anaweza kulieleza Baraza hili hadi sasa wana skuli ngapi ambazo kwa ahadi yao kwamba wananchi wafike kiwango fulani cha kujenga halafu wamalize, ni majengo mangapi sasa hivi wanaripoti kwamba yamekamilika kiasi hicho na hawajayamaliza.

Mhe. Spika, vile vile, kwa yale majengo ambayo yana zaidi ya miaka 10 au 12 yamejengwa katika kiwango cha linta ambacho wizara ina ahadi ya kuyamaliza, anatoa wito gani kwa wananchi katika maeneo hayo ambayo majengo hayo sasa mengine yameanza kuporomoka.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, majengo ambayo tunayo kwa hivi sasa ndani ya wizara ambayo tayari tumekabidhiwa na skuli husika ni majengo yasiopungua 200, ambayo tumeyakamilisha, siwezi kutoa takwimu hapa nitamletea kwa maandishi kwa sababu bado ujenzi unaendelea. Lakini niwaahidi wananchi na walimu wote ambao wamo katika jitihada kubwa ya kuhakikisha kwamba wanafunzi wetu wanapata mazingira mazuri ya kusomea, kwamba wizara tuko pamoja nao na tutahakikisha tunayamaliza majengo hayo siku hadi siku kwa mujibu wa fedha ambazo tutazipata kutoka serikalini. Vile vile, tuna mahangaiko ambayo tunahangaika kutoka kwa wafadhili. *SIDA* wanatusaidia sana. Kwa hivyo, tunajitahidi naamini penye nia pana njia tutamaliza tu.

Nam. 36

Wajibu wa Kijamii kwa Kampuni ya *ZANTEL* kwa Hospitali ya Kijiji Cha Muyuni

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Kwa kuwa Kampuni ya *Zantel* ndiyo pekee inayoungwa mkono na idadi kubwa ya wateja wa huduma ya mawasiliano Zanzibar. Kwa kuwa Kampuni hiyo imeweka miundombinu yake ya minara katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar ikiwemo eneo la Hospitali ya Kijiji cha Muyuni na kwa kuwa Kampuni yoyote inakuwa na wajibu wa kijamii (*Corporate social responsibility*) kwa jamii ambayo huduma na miundombinu yake inatolewa na kupatikana.

(a) Je, kwa nini Kampuni ya *Zantel* haijatekeleza wajibu wake wa kijamii kwa kuisaidia Hospitali ya kijiji cha Muyuni ambapo katika eneo lake kumewekwa miundombinu ya mnara wao.
(b) Ni kwa kiasi gani Hospitali ya Kijiji cha Muyuni itafaidika kwa kuwepo miundombinu hiyo ya Mnara wa *Zantel* katika eneo lake.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 36 lenye kifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, katika eneo la kijiji cha Muyuni Kampuni ya *Zantel* inamiliki mnara mmoja tu ambao umejengwa katika kiwanja cha shamba la Bwana Soud Saleh Makame, mnara huu umejengwa baada ya kufanyika makubaliano maalum baina ya Kampuni ya *Zantel* na mmiliki wa kiwanja hicho. Makubaliano hayo ni ya kukodishwa kiwanja hicho na Kampuni inamlipa kwa kila mwezi mmiliki huyo kwa mujibu wa makubaliano hayo.

Mhe. Spika, hata hivyo, Kampuni ya *Zantel* imejitolea katika kuchangia huduma za jamii kama vile kuweka huduma ya maji safi katika maeneo mbali mbali ambayo yalikuwa na shida ya maji na ukosefu wa huduma hii muhimu.

Mhe. Spika, pia, kwa mwaka huu, Kampuni ya *Zantel* ina mpango wa kusaidia madawa na vifaa vya Hospitali katika Hospitali mbali mbali za Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, kituo cha afya cha Muyuni pamoja na watu wake watafaidika kwa kuwepo wa mawasiliano mazuri ya *Zantel* pamoja na huduma nyengine za kijamii kama ilivyo sehemu nyengine za Zanzibar.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, kwanza nichukue fursa hii kwa dhati ndani ya moyo wangu kumpongeza Mhe. Naibu Waziri kuwa kipindi cha bajeti kinakaribia hivi sasa, kuchukua jitihada ya barabara ya Kinazini kuichimba, barabara ya Sogea sasa hivi inapitika, barabara yetu ya Kisiwandui nimeona shughuli hizo zinaendelea vizuri na hii itamsababishia akifanya haraka bajeti yake huenda ikapita muda bado anao wa kujipanga. Waswahili wanasema; "Mpungwa naye hupungwa, ukupigao ndio ukufunzao".

Mhe. Spika, naomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Wateja wa Jimbo la Muyuni wa *Zantel* ni wengi. Je, ni sehemu gani wanaopata kufaidika katika msaada huo ulioutaja.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, la kwanza tunapokea pongezi na hongera zake kwa kazi tunayoifanya.

Mhe. Spika, la pili, anauliza kwamba kwa kiasi gani wananchi wa Muyuni kwa sababu *Zantel* ina wateja wengi wananufaikaje. Majibu ni yale yale kwamba *Zanztel* wajibu wake wa msingi ni kuimarisha huduma zake za mawasiliano kwa wananchi wa Muyuni, Kitogani, Bwejuu, Paje pamoja na Zanzibar nzima na maeneo yote ambayo wanapata huduma hii, lakini yeye anauliza kwamba watanufaikaje? Kimsingi kwa utaratibu wa *Low corporate society*. Mimi nimthibitishie kwamba *Zantel* wamekuwa wakitoa mchango huo kwa maeneo tofauti, kwa mfano kutoka mwaka 2012/2013 *Zantel* ilichangia mabomba yenye thamani ya shilingi 11 milioni kwa jimbo la Kitope na Dole.

Mhe. Spika, aidha, *Tour operator* kwenye mwaka wa 2011 walichangia takriban shilingi 11.2 milioni, *Zanzibar Association of Tourism Investors* (*ZATI*) mwaka jana walipewa shilingi milioni nane (8), Polisi mwaka jana walipewa pikipiki 10 zenye thamani ya shilingi 16 milioni, *ZFA* ligi ya vijana zawadi zao walipewa shilingi milioni 32, wamechimba visima vitano kwa kushirikiana na *ZECO* vyenye gharama ya shilingi 21 milioni, wakati mwaka huu 2014 *Zantel* wameweza kushirikiana na *ZATI* katika usiku maalum wameweza kuchangia shilingi 16 milioni, lakini pia, katika *May Day* ya mwaka huu wameweza kuchangia zawadi ya shilingi milioni tano kwa mshindi wa mpira wa miguu katika mashindano ya wafanyakazi.

Mhe. Spika, kwa hivyo, nimhakikishie Mhe. Mjumbe kwamba *Zantel* kama yalivyo mashirika mengine inasaidia sana jamii katika huduma na nyanja tofauti.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, ahsante na mimi kwa ruhusa yako naomba niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa tumeshuhudia maeneo mengi ya serikali ikiwemo maeneo ya skuli, kwa mfano Hamamni na maeneo mengine kuwekwa minara hii ya simu, ninataka kujua labda utaratibu unaotumika kuweka minara ya siku kasika maskuli na faida ambayo skuli zile zinaweza kuipata.

Mhe Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, ni kweli kwamba eneo la Hamamni kuna mnara wa *Zantel*, lakini mnara ule ni eneo ambalo limetolewa makusudi na serikali likiwemo pamoja na eneo la Kikwajuni, Fumba ikiwa ni sehemu ya mchango wa serikali katika uwekezaji wa *Zantel* katika visiwa vyetu asilimia 18. Mimi naamini kwamba malengo ya kuweka minara huwa inawekwa maeneo maalum kwa ajili ya kuweza kupata nguvu ya mawasiliano, lakini mabadiliko haya yanapokuja ya kiduni tunaamini si muda mrefu sana katika kipindi kisichozidi miaka 20, matumizi haya ya minara yatakuwa yametoweka na naamini kwamba njia kubwa ya mawasiliano itabaki ya *Satélite* au njia nyengine.

Mhe. Spika, kwa sababu hivi sasa hata ile minara ya *fixed* inapungua sana, wenyewe wanakuja na minara mipya wanaita *CAW* kwa maana ya *Cell on Wheels***.** Kwa hivyo, *automatically* kwamba maeneo haya ni kwa ajili ya kupata *covering*, sio lazima yawe maeneo ya skuli ni maeneo yote ambayo yatakuwa na maeneo karibu ya kuweza kutengeneza *network* zao vizuri kwa ajili ya kupata mawasiliano, kwa ajili ya kuunganisha *Satélite.* Kwa hiyo, tunaamini kwamba kama maeneo ya Hamamni na maeneo mengine yataondoka tu, kadiri mawasiliano yanavyokuja

Satélite itachukua nafasi kubwa zaidi kuliko minara. Kwa hivyo, maeneo haya lengo ni kuimarisha mawasiliano, sio lazima yawe maeneo ya skuli.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Spika, ahsante sana, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha siku ya leo kufika hapa kwa ajili ya mambo yetu ya Kitaifa.

Mhe. Spika, kwa kuwa *Zantel* imesajiliwa hapa Zanzibar na kwa kuwa ina wananchi wanaoitumia. Je, Mhe. Naibu Waziri, ataliambia vipi Baraza lako hili tukufu kwamba ni mashirikiano yepi wao na *Zantel* kwa vile najua wizara hii ni ya miundombinu na mawasiliano, wana mashirikiano yepi ya kuwafanya wao wakazungumza na *Zantel* kwa mambo mengine mbali mbali. Kama wana mashirikiano, je, atatueleza vipi Mhe. Naibu Waziri na kama hawana pia alieleze Baraza lako tukufu hawana mawasiliano mazuri kwa nini.

Vile vile, haoni kwamba kuna haja ya kuja kutufanyia semina hapa kwa sababu *Zantel* siku nyengine zagazaga, mara unapata mawasiliano mara hupati.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, ni kweli kwamba Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ina ushirikiano wa karibu sana na Kampuni ya *Zantel*, mashirikiano yetu sisi yanahusiana zaidi masuala ya kiufundi. Tunatambua kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina hisa katika Shirika hili la *Zantel* na Mjumbe wa kuiwakilisha serikali katika Kampuni hiyo kwa malengo ya hisa ni Wizara ya Fedha. Kwa hivyo, wajibu wetu Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ni kuona kwamba huduma na mawasiliano ya *Zantel* zinakuwa bora na hilo ndio eneo ambalo tunashirikiana.

Mhe. Spika, suala jengine ni kwamba sisi kama watu ambao tunashirikiana katika mfumo wa kutoa huduma na kuimarisha mawasiliano, tutajaribu kuzungumza nao wenzetu wakiona kwamba kuna ulazima au haja ya kufanya semina kwa malengo ya kukuza uelewa na upeo kwa huduma zao wanazotoa kwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu hatuoni tatizo, tutafanya mawasiliano na watakachotujibu tutaona sasa utaratibu wa kuweza kulijuilisha Baraza hili kwa kupitia kwako.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa
Mwaka 2014/2015 - Wizara ya Afya

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii ya kwanza kwa siku ya leo ili niweze kutoa mchango wangu katika hotuba hii iliyopo mbele yetu.

Mhe. Spika, kwa kuanza nataka, nianze na ukurasa wa 8 kuhusu Kitengo cha Kufuatilia Mwenendo wa Maradhi.
Mhe. Spika, wananchi wetu wa Zanzibar sasa hivi kwa kipindi kirefu sasa wamekuwa wakisumbuliwa na maradhi mengi, maradhi ambayo hapo zamani kidogo hayakuwa yakijitokeza sana katika jamii, lakini katika miaka ya hivi karibuni yameondokea kujitokeza kwa wingi sana, kwa mfano maradhi ya moyo, sukari, figo, maradhi ya viungo haya hasa magoti na maradhi ya kuziba choo cha mkojo yamekuwa mengi sana. Sasa bila shaka maradhi yanakuwa na sababu zake. Sasa nilikuwa namuomba Mhe. Waziri atueleze kama kuna utaratibu wowote ambao Wizara imepanga kufanya utafiti ili kujua hasa kinachosababisha maradhi haya ni kipi. Na pengine kama kuna haja ya kutoa tahadhari, basi wananchi wapatiwe taaluma hiyo ili waweze kujikinga na maradhi ya aina hii ambayo kwa kweli yanatupotezea nguvu kazi katika kiwango cha kutisha sasa.

Mhe. Spika, sasa hivi kila mtu anatembea kama kwamba anajifundisha sasa kwenda, miguu haifanyi kazi vizuri, mtu unamkuta leo na hali yake kesho ukimkuta tayari amenyauka tatizo nini sukari. Sasa nafikiri kuna haja serikali kufanya utafiti wa makusudi tukajua kama kuna chakula tunatumia kinatudhuru, basi tukiache au kama tunakosa aina fulani ya chakula ndani ya mwili wetu, basi watushauri tuweze kutumia ili tuweze kuepukana na matatizo kama haya.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo mimi naligusia kidogo kama tanbihi kwa Wizara na kwa sababu ni Wizara ya Afya watakuwa washauri wazuri.

Mhe. Spika, vijana wetu mashuleni sasa inaonekana wanapata tatizo la macho kwa wingi zaidi, watoto wadogo sasa hivi unawakuta wanaongezeka kuvaa miwani kila uchao. Sasa katika utafiti wa haraka haraka tulioufanya tunagundua kwamba yale madarasa wanayosomea hayana mwangaza wa kutosha kutokana na yale majengo ya skuli yanavyojengwa sasa hivi na kwa sababu watoto wanakaa mle muda mrefu wanayalazimisha macho kutaka kuona yale masomo yao. Kwa hiyo, wameanza kupata matatizo ya macho kwa wingi. Sasa naona hili ni jambo ambalo kwa kweli lazima tuliwahi mapema kabla halijakuwa tatizo huko baadae.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nilisema nilizungumze na nilitaka nilizungumze kwa sababu ukifungua ukurasa wa 22 kuna takwimu za gharama hapa kwa kweli zinaanza kupita sasa. Haya ni matibabu ya wananchi wanaopelekwa nje ya nchi kwa matibabu. Gharama zake kwa mfano mwaka jana kwa mujibu wa kitabu cha Waziri, Wizara ilipangiwa milioni 500 kwa ajili ya kusafirisha wagonjwa kupeleka nje ya nchi, lakini kwa mujibu wa takwimu zake hapa uhalisia ametumia zaidi ya bilioni 2,564,000,000/=. Sasa hii ni tofauti kubwa sana iliyopo. Sasa nimeona humu kwamba kuna mpango Wizara wamepanga wa kuwaita ma-*expert* kuja kupiga kambi hapa na kujaribu kuwatibu wananchi kwa baadhi ya yale matatizo ambayo yanalazimika kuwapeleka nje ya nchi.

Mhe. Spika, lakini nilikuwa na wazo kwa nini tusisomeshe vijana wetu katika fani hizo ambazo sisi humu ndani hatuna, kwa sababu naona *expert* huyu akija hapa inawezekana wengine ni misaada ya nchi washirika wa maendeleo, lakini inawezekana mara nyengine tunawalipa sisi, lakini tukisomesha wetu kwa vyovyote vile gharama itapungua.

Mhe. Spika, sasa nilikuwa nashauri kwa nini kusiwe na *project* japo ikawa kubwa kidogo, lakini tukafika pahali tukaweza kuwa na madaktari wetu, tukaweza kuwa na vifaa vyetu vya kufanyia tiba hizi ambazo mara nyengine tunajitahidi kidogo tunaweza kuzikwepa gharama kubwa kama hizi. Nilikuwa naomba nishauri hilo.

Mhe. Spika, jengine nilisema nizungumzie kidogo kuhusu tiba asili au tiba mbadala. Nimeona humu Waziri ametolea ufafanuzi katika ukurasa wa 46. Hili jambo ni muhimu kwa sababu matibabu sasa ni ghali na hali za wananchi wetu tunaziona zilivyo wanyonge sana na ukiangalia tiba hizi za asili kuna unafuu kidogo, halafu zina faida nyengine ni kwamba hazina ma-*chemical* mengi kwa hiyo haziathiri sana katika viwiliwili, lakini ni dawa ambazo zinaweza kupatikana kwa urahisi.

Mhe. Spika, Mwenyezi Mungu anatupenda sana sisi waja wake. Miti tunaiona katika nchi yetu yote ina faida fulani fulani na faida kubwa ni kwa ajili ya kuwatibu binadamu. Tunachokosa sisi ni taaluma ya kujua mti upi ni tiba ya maradhi gani. Sasa nilikuwa namuomba sana Mhe. Waziri hili suala lipewe kipaumbele cha kutosha, kwa sababu mambo mengine hayataki gharama, kwa mfano kuna mzee mmoja anasema yeye akipata malaria wala haendi Hospitali, anatafuta vilele vya mpapai akachemshe na maji akanywa malaria yakaondoka, lakini sasa inataka taaluma mtu ajue, je, vilele vya mpapai vinatibu malaria? Kama hujui, basi huwezi kufanya tiba.

Mhe. Spika, kuna mara nyengine tunapata matatizo kwa sababu ya kutokuwa na virutubisho fulani, kwa sababu wataalamu wanasema maradhi yoyote ndani ya mwili yanakuja kwa sababu ya kukosa aina fulani ya virutubisho. Tuna matunda mengi sana hapa visiwani ambayo kama tungejua faida zake tukayatumia, basi tungepata hivyo virutubisho na yale maradhi yasingekuja, lakini bahati mbaya hatujui.

Mhe. Spika, kwa mfano parachichi lina faida nyingi sana, bamia lina faida nyingi sana. Kuna mtu mmoja ananiambia jamaa yake mmoja kenda India kutibiwa magoti haya matatizo ya viungo, basi kufika kule wakampima wakamwambia bwana wewe umekuja kuhangaika bure, huko huko kwenu tiba ipo na ngojea tutakuonesha. Wakamtibu kwa maji yale ya mabamia mpaka akapoa, halafu wakamuuliza mabamia kwenu hayapo? Sasa haya ni mambo wanahitaji wananchi kuyajua ili kukwepa gharama, ili kupata virutubisho kwa bei nafuu zaidi, lakini tatizo wananchi hawajui.

Mhe. Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba sana Mhe. Waziri hili jambo lipewe kipaumbele cha kutosha ikiwezekana kuwe na maskuli kabisa ya kufundisha faida hizi za miti hizi, huu una kitu gani na huu una kitu gani, ili tuweze kupata tiba kwa unafuu na kuweza kuwarahisishia wananchi maisha, kwa sababu tunasumbuliwa sana na kugharimia afya zetu.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nilisema niligusie kidogo ni kuhusiana na Hospitali yetu ya rufaa ya Mnazi Mmoja. Ile Hospitali ilijengwa miaka mingi sana iliyopita na wakati ule ilipojengwa idadi ya watu Zanzibar ilikuwa

ndogo sana, lakini pamoja na udogo huo walioitengeneza waliweka milango mitatu ya kuingia na kutoka mle Hospitali.

Mhe. Spika, sasa kuna *modification* zinafanywa, mpaka kuna siku nimekwenda ile ngazi pale katikati imefungwa. Imefungwa ngazi ile wakati *population* yetu imetoka kutoka watu laki tatu mpaka milioni moja na laki tatu. Sasa hatari iliyopo ni kwamba Hospitali ile sasa inabeba watu wengi zaidi, hata hao wanaokwenda kuangalia wagonjwa ukifika ule wakati wa kuangalia wagonjwa wanakuwa wengi mle Hospitali. Kwa hiyo, tuwe na tahadhari ya kuja kutokea jambo mle Hospitali likabidi, sasa kuna haja ya watu kuteremka kwa kasi.

Mhe. Spika, kwa mfano Mwenyezi Mungu atuepushe mbali unaweza ukaingia moto au likatokea balaa lolote lile. Kuna haja ya kuwa *outlet* ya kutokea watu kwa kasi kubwa sana. Leo ikiwa katika karne hizi ndio tunafunga ngazi, tunafanya nini, litakuja kuwa janga lije litufundishe wakati tumeshaharibikiwa. Sasa nilikuwa naomba sana Mhe. Waziri atafute wataalamu ikiwezekana ile ngazi ama waifungue au watafute uwezekano wa kuweka ngazi nyengine za ziada ili likitokea jambo watu wapate pa kukimbilia.

Mhe. Spika, hivi karibuni kuliingia moto pale kwenye studio ile ya Annur. Ulipoingia ule moto kulikuwa na watu kule juu wapo kazini. Mmoja baada ya kukosa pa kutokea ililazimika aruke kutoka kwenye fleti ya kwanza mpaka chini akaumia miguu, lakini akanusuru maisha yake. Sasa kungekuwa na utaratibu mzuri angeweza yule kutoka bila ya kuumia. Sasa na sisi tutawalazimisha watu waje waruke kutoka Hospitali ya Mnazi Mmoja waanguke chini pale tutakuwa na walemavu wengi kweli kweli na mtu akiona moto unamjia anaweza akaruka. Sasa naona niseme hili ili tuweke tahadhari mapema kabla athari haijatokea.

Mhe. Spika, jengine nafikiri ndio la mwisho na hili nalisema kwa masikitiko kidogo na ni nyimbo ya wananchi na Waheshimiwa Wawakilishi kila wakati wanalisema jambo hili, kama mtu anahitaji kuthaminiwa ni mgonjwa. Mgonjwa anatakiwa apewe lugha laini, apewe nasaha, kwa sababu yale maradhi peke yake ni *frustration* kubwa. Sasa ukimuongezea na maneno mengine ya kuudhi utammaliza. Sasa sijui ni sababu zipi hasa zinazowafanya hawa wauguzi wakawa na lugha mara nyengine zinaudhi sana. Si wote, unawakuta wengine wana imani zao, wanakusemeza kwa lugha nzuri, lakini kuna wengine tuna jeuri na ufedhuli, ni watukanifu, maana yake unajua kuna wakati mtu anaweza kufanya kazi mpaka akachoka, akishakuwa na *frustration* kichwani akipata mambo mengine akawa anaropokwa ovyo.

Mhe. Spika, lakini nadhani kuna haja ya kuongeza bidii ya kuwasomesha hawa watu ili wajue kama wanatoa huduma kwa watu wanyonge sana wanaohitaji upole wa hali ya juu. Sisi ni waislam, sifa moja waislam ni wapole, ni watu wenye huruma, watu walio na imani. Sasa ukimkuta mtu mgonjwa halafu ukamtolea lugha mbaya kwa kweli unakuwa humtendei haki hata kidogo. Sasa nilikuwa namuomba sana Mhe. Waziri pamoja na juhudi alizonazo, lakini aendelee kutoa nasaha hizi kwa wauguzi wetu ili hatimae tujenge picha nzuri hasa katika Hospitali zetu hizi za serikali.

Mhe. Spika, maana yake utashangaa ukenda kwenye Hospitali za binafsi huyakuti haya yanapungua kwa kiasi kikubwa, lakini kwenye Hospitali hizi ambazo wanyonge wa Mungu ndiko wanakimbilia, basi kunakuwa na lugha ambazo si za kuridhisha hata kidogo. Kwa hiyo, naomba sana Mhe. Waziri afanye bidii zaidi, ikiwezekana kuwe na darasa maalum,kwa sababu kila pahala pa kazi panakuwa na saikolojia yake, ukenda polisi kuna saikolojia maalum ya kumfanya mtu a-*provoke* kile alichokifanya. Sasa analazimika kama kuna mambo anayaficha akiona mtu katufanyia hapa atayasema, mara nyengine atasema mpaka uongo, lakini kule Hospitali kunahitaji lugha laini sana ili kumfanya yule mtu hata kama hujampa tiba, lakini yale maneno yako yawe tiba. Mimi naomba sana hilo.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo sina mchango mkubwa. Mimi naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja.
Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, na mimi nichukue fursa hii adhimu asubuhi ya leo kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba hii ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Afya.

Mhe. Spika, kwanza nichukue fursa hii adhimu kuushukuru uongozi wa Wizara ya Afya kwa jitihada wanazozifanya, lakini shukrani za pekee zimuendee Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii, dada yangu Mhe. Mgeni Hassan Juma kwa namna anavyojitahidi kutoa mashirikiano kwa Wajumbe wake wa Kamati na kuweza kusimamia mapinduzi ya afya kwa Zanzibar. Katika kipindi chake tumepata kuona mabadiliko makubwa ambayo yameweza kufanyika.

Mhe. Spika, lazima tukiri jitihada za serikali katika kuleta mabadiliko ya Mapinduzi ya afya yanafanyika hatua kwa hatua na wahenga wanasema "Mwenye macho haambiwi tizama". Tumeweza kuona jitihada namna ya kutaka kupambana na kuweza kuondosha misongamano ya kitengo kile cha mama wajawazito kwa matayarisho ya kuhamia katika jengo la zamani lililokuwa Kiwanda cha Madawa. Tumeona jitihada za ujenzi wa jengo jipya ambalo tunategemea tutaweka *ICU* na maradhi maalum. Sasa hizi ni jitihada ambazo serikali yetu inaonekana za kupiga hatua katika suala la afya.

Mhe. Spika, lakini pia, nishukuru kwa jitihada za kuweza kupandisha daraja Hospitali zetu mbili; Hospitali ya Mpendae na Hospitali ya Kwamtipura, lakini pamoja na jitihada hizo ambazo zinaonekana kweli tumejaribu kupunguza wingi wa idadi ya watu kukimbilia katika Hospitali yetu ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Spika, lakini pamoja na jitihada hizo bado tunakuwa tunakabiliwa na changamoto nyingi tu na changamoto kubwa ambayo imekabili Wizara ya Afya ni suala zima la mapato madogo ambayo wanaingiziwa na serikali. Sasa hili nimuombe Mhe. Waziri wa Fedha. Unajua utaratibu wetu wa kupitisha bajeti Zanzibar umekuwa tofauti na wenzetu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wenzetu sasa hivi wameanzisha utaratibu kule kwamba ile bajeti kuu ya serikali huwa inapitishwa mwisho baada ya kujadili bajeti za kisekta. Kwa hiyo, pale panapoonekana pana mapungufu, basi Kamati za bajeti zinakuwa zinakaa ili kuona kuweza kusaidia kuongeza yale mafungu katika zile bajeti ambazo zinaonekana zina mashaka ili kuweza kusaidia ufanisi wa kazi zao. Sasa hili najua utaratibu baadae utakuja, lakini tuendelee kama wenzetu wanavyofanya.

Mhe. Spika, maeneo mengi ambayo iwe mimi au Wajumbe wenzangu wamepiga kelele, basi lazima tukubali kutokana na ufinyu wa bajeti ya Wizara ya Afya. Kuna tatizo katika kila eneo. Kaka yangu pale Mhe. Jaku Hashim Ayoub jana alitaka kulia akakirembea kitabu kwa kadhia ambazo zimeikuta Wizara ya Afya. Akatoa mifano ya watu kulala kiza *Mental Hospital* kwa umeme kutokuingizwa, lakini watu wanashindwa kuingiza kwa sababu ya fedha. Angalau tungekuwa tunatoa malalamiko kwamba watu hawakuingiza kwa sababu fedha wanazo ingekuwa hilo ni tatizo, lakini tatizo kwamba watu hawana fedha ni sababu ambayo wanashindwa kuingiza huo umeme na mambo mengine.

Mhe. Spika, sasa nitajaribu kuelezea katika maeneo mbali mbali baada ya hii dibaji kidogo, lakini kwanza nitoe shukrani zangu za pekee kwa Daktari Bingwa wa Mifupa kaka yangu Shaib, natoa pongezi kwa namna alivyoonesha jitihada katika kukabiliana na tatizo ambalo lilinikuta katika jimbo langu la vijana waliopata ajali waliokuwa wakielekea Makunduchi. Kwa kweli alifanya jitihada za kutosha kuweza kuokoa maisha ya vijana wetu, lakini katika hili nataka nitoe indhari kwa Wizara ya Afya kwamba Daktari Bingwa tuliyekuwa naye sasa hivi ni mmoja.
Mhe. Spika, sasa ninasema Mwenyezi Mungu anakuwa anawapenda sana madaktari bingwa pamoja na walimu, kwa sababu mara nyingi walimu na madaktari bingwa huwa wanakawia kufa, mara nyingi ukifanya tathmini. Mwenyezi Mungu anafanya hivyo kwa hekma zake na rehma zake kwa sababu kama daktari Shaib atakufa leo, tutakuwa tuna matatizo katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Sasa nina imani Mwenyezi Mungu atampa maisha marefu ili serikali iweze kujipanga katika siku za usoni ili kuweza kuwapata madaktari ambapo akiondoka yule mtu kuweza ku-*cover*.

Mhe. Spika, hiyo ni sehemu moja, lakini sehemu nyengine mara nyingi madaktari bingwa wenzetu wanaoujua umuhimu wao wanakuwa wanawanyemelea sana. Tulikuwa na daktari bingwa hapa Ndugu Rashid ambaye sasa hivi amechukuliwa na kuhodhiwa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Hakwenda hata mafunzo, wapomuona tu walimchukua wamempa ma-*rank*. Hivi sasa ninafikiri ameshafikia Kanali, anapanda vyeo siku hadi siku kutokana na umuhimu wake. Kwa sababu wetu wamekuwa wanajali ule muhimu wa wale madaktari.

Mhe. Spika, sasa niombe serikali kuangalia hawa madaktari bingwa wote, sio Ndugu Shaibu peke yake, kuwatengea mazingira yaliyokuwa mazuri ili baadae wasije wakachukuliwa tukaja kukosa madaktari bingwa katika mahospitali yetu, kwa sababu ninasikia kwa funu za mbali hata na yeye huyu Jeshi la Wananchi linamuhitaji. Sasa akija akichukuliwa na yeye tutakuja kuwa mtihani kwa Hospitali yetu ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Spika, sasa watengeneze mazingira mazuri kwa madaktari wetu ili waweze kutulia na kufanya kazi katika mazingira mazuri, yanapokuwa mazingira mazuri tunaanzia na masuala ya maslahi, makaazi bora, usafiri uliokuwa mzuri na mahitaji yote ambayo yanayomfanya mtu aridhike na eneo lake lile la kufanyia kazi.

Mhe. Spika, ninataka nizungumzie kadhia ambayo nimekuwa nikizungumzia kwa muda mrefu juu ya jengo la watu ambao wanafika katika Hospitali ya Mnazi Mmoja kwenda kuangalia wagonjwa. Nilizungumzia kwenye swali,

nilizungumzia katika bajeti ya mwaka jana na leo ninazungumza tena. Ninaiomba serikali, leo naona sana hapa simuoni Balozi Seif Iddi, wala simuoni Mhe. Mohammed Aboud. (*Makofi*)

Mhe. Spika, hapa naiomba serikali baadhi ya taasisi zimefikia pahala zinakwamisha jitihada za serikali katika kuondeshea kero wananchi. Karibuni tu tulikuwa na kipindi cha mvua kisichopungua miezi miwili. Nilikuwa nikimwambia swahibu wangu Mhe. Waziri wa Afya, leo jua kali watu wanapumzika chini ya miti, wakati wa mvua hawa watu watapumzika wapi? Ni unyonge watu wanakwenda kusubiri muda, kwa sababu mtu anatoka masafa ya mbali, anafika Hospitali saa sita au sita na nusu, anasubiri saa saba ifike mvua inanyesha mtu pa kujificha hana.

Mhe. Spika, baada ya kwenda kumuangalia mgonjw,a anaanza kuumwa yeye na homa kutokana na kadhia ya mvua anayoipata. Sasa kwenye Kamati pia hili nililizungumza, nikapata majibu ambayo hayajaniridhisha na leo ninazungumza tena ili serikali inisikie, mimi nitakuwa mgumu kwenye bajeti ya ardhi siku itakayofika, juu ya suala la Mamlaka ya Mji Mkongwe kuidhalilisha Wizara ya Afya katika kutoa eneo la kuweza kujenga kituo cha watu kupumzikia.

Mhe. Spika, ninasema ninapata mashaka sana na nitakuwa mkaidi sana, kwa sababu tumejaribu kuomba kama wizara, Kamati imepiga kelele, lakini kutoa eneo kwa muda wa miaka miwili, watu wanapanda ngazi kwa Mkurugenzi wa Mji Mkongwe kwenda na kushuka majibu hakuna. Wananchi waliokuwa wengi wanateseka. Hili ni tatizo na kinachonisikitisha utaambiwa eneo la hifadhi, hifadhi hii inakuwa kwenye vitengo vya serikali na katika maeneo ya watu wa raia au wafanyabiashara mbona wanaruhusiwa.

Mhe. Spika, juzi nilizungumzia jengo ambalo limejengwa katika *open space* pale Darajani.Mji Mkongwe haukuonekana.Mkunazini kwenye Mbuyu kumezungushwa maduka na asili yake tunaijua, watu wameruhusiwa Mji Mkongwe hauoni, lakini leo tunataka kujenga banda la watu kupumzika kwenda kuangalia wagonjwa, Mji Mkongwe wanatoa *comments* mbali mbali. Hili ni tatizo.

Mhe. Spika, ninasema ninamsubiri Mhe. Waziri wa Ardhi aje anijibu. Juzi ninasikia kwenye vyombo vya habari wanazungumza kwamba wameruhusu kujengwa jengo la dharura. Haya ni maajabu, banda la dharura kwenye Hospitali ya Mnazi Mmoja, maana yake labda watu baadae watakuwa hawaumwi tena, maana kitu unapozungumza cha dharura inabidi kikae, halafu kiondoke, kwa sababu unapojenga jengo unahitaji kuna baadhi ya mahitaji yanahitajika.

Mhe. Spika, hilo eneo limejengwa mabanda mbali mbali, maduka ya madawa, sijui pamejengwa mabanda ya kuchomea *chips*, yote yameruhusika, pana Ofisi ya Kitengo kile cha Ukimwi sijui, yote yameruhusika, lakini banda la kupumzikia wagonjwa haliwezekani! Ninamsubiri Mhe. Waziri wa Ardhi, Waziri wa Afya asiwe na wasi wasi katika hili. Jitihada nimeziona na amejitahidi kama Waziri, wameomba wafadhili, wafadhili wapo tayari, lakini sekta inayohusika inatukwamisha katika hili. (*Makofi*)

Mhe. Spika, ninataka niombe mwalimu wangu wa siasa Mhe. Omar Yussuf Mzee. Ni mwalimu wangu wa siasa amenielewa tangu mdogo, ndiye ambaye aliyenishawishi nikachukua Udiwani, ndiye ambaye aliyekuwa ananisaidia changamoto zangu katika masuala ya Udiwani na leo nipo naye. Namuomba sana ajaribu kutumia hekma zake na busara katika kuisaidia Wizara ya Afya ili kuondokana na changamoto zinazojitokeza.

Mhe. Spika, hii sekta ni muhimu. Mimi kama angekuwa ananikubalia au tunakubaliana, ningemwambie azuie ununuzi wa magari katika taasisi wa serikali kwa muda huu wa mwaka mmoja. Kweli tuzuie, tuzuie kununua magari katika kila taasisi kwa sababu nina imani kwamba magari yapo na viongozi wanafika, lakini tumeshaona viongozi maisha yote wanapenda raha tu, sisi tunapenda raha wakati wananchi wa chini wanateseka. Tuzuie kununua magari katika Ofisi za Serikali kwa mwaka, pesa zote tuzipeleke Wizara ya Afya zikasaidie wananchi wetu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nasema hili kwa sababu tukijipanga tunaweza. Kama tulivyothubutu kutafuta namna ya kuweza kukata baadhi ya mapato au mafao katika serikali katika wizara, tukaweza kupata pesa kununua meli, basi iweje leo tuweze kupanga mpango wa kununua meli, tushindwe kupanga mipango ya kuweza kununua vifaa katika Hospitali yetu.

Mhe. Spika, Hospitali inatisha ina masikitiko makubwa, lakini kutisha kwake kote, matatizo yake yote ni suala la fedha. Hospitali kuna aibu, aibu sio ya Waziri na sio ya watendaji. Aibu inatokana na uwezo finyu wa kuweza kununua vitendea kazi.

Mhe. Spika, sisi wanasiasa huwa Hospitali hatuondoki kwa sababu ya kuwahudumia wananchi wetu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, juzi katika ajali hiyo hiyo iliyotokea Makunduchi imetokea aibu. Mimi nipo katika chumba cha *X-ray* na Mhe. Jaku Hashim Ayoub juzi alizungumza tulikaa muda mrefu, tulikaa *X-ray* tangu saa tatu mpaka tisa za jioni, lakini aibu iliyojitokeza zile zana zimepitwa na wakati. Huu sio wakati tena wa kupiga yale ma-*X-ray* yaliyokuwepo pale Hospitali ya Mnazi Mmoja. (*Makofi*)

Mhe. Spika, sasa hivi watu *X-ray* wanakwenda na *digital*, mgonjwa wangu ambaye ameumia mkono na Mwenyezi Mungu amsaidie ambao sasa hivi mkono ule umekatwa Hospitali ya Dar-es-salaam na Mheshimiwa mwenyewe alinishuhudia *Airport* kumsafirisha mgonjwa yule. Yule mgonjwa Mheshimiwa kakatwa bwana, mkono kakatwa na sasa hivi ni mlemavu.

Mhe. Spika, lakini cha kusikitisha tunamuingiza mgonjwa *X-ray* kwenda kupigwa picha, baada ya kupata taarifa Dkt. Shein kwamba lazima apigwe kuangaliwa hali yake, picha imepigwa katika ile hali ya kawaida, kwenye ukuta pale wenyewe wana mashine ya kuangalia ile picha, picha imeangaliwa. Kaka yangu Ali Mmarekani pale hakuona kitu, yaani picha haioneshi. Akaichukua picha ile akaiangalia kwa juu picha haioneshi, akavua miwani picha haioneshi. Haya mambo yamepitwa na wakati kabisa.(*Makofi*)

Mhe. Spika, zana za sasa hivi ukipigwa *X-ray*, *digital* inatoa kule, inatoa *result* ya nini tatizo na tatizo mgonjwa ameathirika kiasi gani. Sasa haya mambo ya kutizama kwa picha. Mhe. Waziri wa Fedha, tusaidie kuweka vifaa vya kisasa. Hebu tumia jitihada zako, kama ulivyotumia akili yako ya kukata mafao ambayo hayana msingi katika mawizara, tukate mafao tupeleke Hospitali ya Mnazi Mmoja. Tutawalaumu madaktari, tutalaumu Mawaziri, lakini tatizo ni fedha na zana zimepitwa na wakati. (*Makofi*)

Mhe. Spika, katika hizo jitihada ambazo za ndugu zetu kupandisha daraja Hospitali ya Mpendae na ya Kwamtipura. Bado hizi Hospitali zina changamoto na changamoto ni zile zile kukosa fedha za kuzisaidia. Vifaa vingi Hospitali ya Mpendae wana mapungufu, kuna baadhi ya vifaa vya kuchemshia wanakuja kuchemsha Hospitali ya Mwembeladu. Masafa marefu huyo anayepeleka kifaa usafiri hana, ile Hospitali yenyewe haina usafiri wa dharura na wakati Kamati ilipopita wametoa kwamba kuna watoto wawili wamewahi kufariki kwa kusubiri gari ya kumtoa pale kumpeleka Hospitali ya Rufaa. (*Makofi*)

Mhe. Spika, *distance* ya kutoka kwenye Hospitali mpaka barabarani kuja kusubiri daladala ni kubwa. Sasa pia hiyo njia yenyewe ina *corrugation* ambayo sio nzuri na Kamati iliambiwa kwamba ile barabara itatengenezwa kutoka kwenye kituo cha daladala kwenda kwenye ile Hospitali watai-*grade* ile ili ipitike katika hali nzuri. Hili kidogo Mhe. Waziri akija atanisaidia kwamba ile barabara tayari wameshaifanyia marekebisho, kwa sababu muliniahidi kwenye Kamati katika kutoa malalamiko, lakini suala la gari la dharura linahitajika, kwa sababu inapotokezea kesi ya mgonjwa kutaka kupelekwa katika Hospitali ya Rufaa haraka wanashindwa, wanabidi wasimamishe vyombo ambavyo havina uhakika.

Mhe. Spika, katika masuala haya haya ya kifedha kwenye Hospitali yetu ya Mnazi Mmoja imekuwa ikikabiliwa na changamoto nyingi tu. Ninasikia tu kwamba *Theatre* kule kuna mapungufu ya baadhi ya vifaa na yanapelekea wakati fulani kwamba zile *operation* za kawaida zinakuwa zinasitishwa. Baada ya kufanywa kila siku zinakuwa labda mara mbili kwa wiki kwa sababu ya uhaba wa vifaa. Sasa ninarudi kwamba bado tunawatesa watu wetu kwa sababu pamoja na kwamba ni *operation* ya kawaida, lakini wanakuwa wanaumwa na wanahitaji huduma.

Mhe. Spika, lakini sio hilo tu, kuna masuala ya gesi, inafika pahala gesi zinamalizika Hospitali kwa sababu ya ukosefu wa fedha na zinapomalizika.

Mhe. Spika: Una dakika tano Mheshimiwa.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, ahsante sana, nitajitahidi, lakini niongezee japo dakika moja tu kidogo. Inapotokezea masuala hayo, yaani huu ukosefu wa fedha au kuingiziwa fedha unapokuwa mgumu, kunakuwa na ukosefu kama huu, kwa sababu ya kujali muda wako ninataka nimalizie mambo mawili.

Mhe. Spika, suala la mwanzo la uvujaji wa mapato katika maeneo ya *CT scan* na *X-ray*. Kumekuwa na uvujaji wa mapato katika haya maeneo na ninazungumza hivi kwa ushahidi kabisa. Ninaelewa Kamati ya Uongozi ya wizara imeshaliona hili kwamba kuna watu hawapewi risiti, wanaambiwa kama una laki wewe lete tu, kwa sababu utaratibu ni shilingi laki moja na nusu upewe risiki yako, lakini ipofika pahala mtu anaambiwa tu, basi kama una shilingi laki wewe lete tu, lakini risiti ndio hatuwezi kukuandikia. Sasa hili naomba uongozi wa wizara kulifanyia kazi kwa makini ili kuweza kuzuia huu mwanya wa uvujaji wa mapato katika hii Hospitali yetu ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Spika, lakini jengine ni suala la masikitiko. Kuna taarifa hili kama kweli Mhe.Waziri, atakuja kunieleza na kama si kweli, basi nitaomba radhi, lakini kuna taarifa kwamba *AC* ya *theatre* ya wodi ya wazazi iliibiwa. Haya ni masikitiko na katika kuibiwa kwake walioshiriki ni wafanyakazi wetu na gari ya Hospitali, ndio iliyohusika na kuichukua, lakini kwa taarifa nilizokuwa nazo ni kwamba Kamati ya Uongozi imewaitwa wahusika na taratibu zinaendelea. Niwaombe basi hatua zitakazostahiki za kisheria itakapogundulikana kadhia hii iweze kufanyiwa kazi.

Mhe. Spika,baada ya hayo kwa heshima yako naunga mkono hotuba hii ya makadirio ya Wizara ya Afya kwa asilimia mia moja. Ninashukuru sana.(*Makofi*)

Mhe. Spika: Tunashukuru. Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Wanu Hafidh Ameir, baadae Mhe. Ismail Jussa Ladhu wakati Mhe. Mgeni Hassan Juma anajitayarisha.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Spika, ninakushukuru na mimi kunipatia nafasi hii kuweza kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mhe.Spika, kwanza naomba niungane na wenzangu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na uzima kukutana hapa leo ili kujadili bajeti ya Wizara ya Afya, lakini pili, nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii na mimi kutoa mchango alau kidogo katika wizara hii.

Mhe. Spika, kwa kuanzia naomba nimpongeze Mhe. Waziri kwa uwasilishaji mzuri wa hotuba yake, lakini pia, nimpe pole kwa majukumu mazito ya kuendesha wizara hii kubwa na yenye umuhimu ambayo kila mwananchi anaitegemea. Nimpe pole zaidi Mhe. Waziri kwa ugumu wa kazi alizonazo, lakini pia, ugumu wenyewe hauendani na bajeti ama na uingizwaji wa fedha anazoingiziwa. (*Makofi*)

Mhe. Spika, ukiangalia *page* ya 3 hapa, kuna mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Ukiangalia mapato ambayo wizara imeingiziwa, kazi za kawaida ni asilimia 26 tu, lakini pia, ruzuku yenyewe haijafika hata asilimia 50, ni asilimia 45 tu ambayo amepata, lakini pia, kazi za maendeleo kwa upande wa SMZ ni asilimia 28 na kwa upande wa washirika wa maendeleo ni asilimia 31. Kwa hivyo, ukiangalia tu hapa utaona kwamba kweli Mhe. Waziri ana kazi nzito, lakini uzito huo unazidiwa pamoja na ufinyu wa bajeti ambao anaukabili.

Mhe. Spika, niungane na Mheshimiwa aliyekaa kwamba kwa kweli hata kama tukilaumu hapa hamna litakalokuwa kwa sababu uwezo wa kufanya kazi ni mdogo kutokana na bajeti ambayo inaingizwa. Mhe. Jaku Hashim Ayoub alitaka kulia hapa, lakini mimi niseme tu hata tukilia machozi ya damu kama Wizara ya Fedha haitoingizia Wizara ya Afya fedha za kutosha, hamna litakalokuwa. (*Makofi*)

Mhe. Spika, mimi nina barua hapa kutoka Wilaya yangu ya Kati kwamba kuna upungufu wa umeme katika vituo vya afya vya Wilaya tunaombwa kuchangia. Sisemi sichangii kila aki-*play part*, ndio mambo yanavyosonga vizuri. Nitachangia katika vituo hivi, lakini niwaombe na Waheshimiwa Wawakilishi wa majimbo; Chwaka, Koani na Uzini kama Mhe. Mohammedraza Hassanali alivyosema jana yeye ameshapokea milioni zake kumi na tano na alisema hapa kwamba yeye ataziingiza katika huduma ya afya. (*Makofi*)

Mhe. Spika, niwaombe na wale wengine wawe na mpangilio mzuri wa kutumia pesa hizi, ni kwa maendeleo ya majimbo yao, lakini pia, wasisahau kuhudumia katika vituo vya afya. Mimi naungana na Mhe. Ali Salum Haji na Mhe. Hamza Hassan Juma, pia, alisema kuna siku hapa, sasa ipo haja ya kubadilisha huu utaratibu wa kusoma bajeti yetu. Bajeti kuu ije mwisho, hizi bajeti za kisekta ndio zianze ili tuone kwamba pale panapomapungufu akihisi tuna-*reallocate* pesa inaingia ile sehemu ambayo ina mapungufu. La si hivyo, basi ile Katiba yetu ibadilishwe, kile kipengele ambacho kinawafunga Wawakilishi kukataa bajeti kwa sababu kipengele kinatufunga sisi, kibadilike angalau tuwe na heshima; seikali iheshimu *backbenchers* na sisi *backbenchers* tuheshimu serikali. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nikimaliza hapo, naomba niingie Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja. Niipongeze serikali kwa kuona umuhimu wa Idara hii na kuipa *vote* yake inayojitegemea. Hiyo yote ni kutaka kuona kwamba Idara hii inafanya kazi kwa ufanisi, lakini kuwapa *vote* yao wenyewe haitoshi, kuwaingizia pesa ndio itatosha. Kwa maana hiyo niiombe Wizara ya Fedha tena hapa kwamba iwe inaangalia sana Idara hii ya Hospitali ya Mnazi Mmoja ili watimize majukumu yao kisawasawa.

Mhe. Spika, basi kama Wizara ya Fedha haitoweza kuingiza ile bajeti, ile fedha yote ambayo imeombwa, lakini angalau kile kinachoingizwa kiwe kinafanana na kile ambacho wamekiomba. Pia, niipongeze Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa kupata daktari bingwa wa maradhi ya akina mama, niseme tu kwamba mchango wangu nita-*base* sana kwa akina mama kwa sababu nilikuwa naangalia takwimu ya maradhi mbali mbali na mambo mbali mbali, mengi yanatu-*affect* sisi akina mama.

Mhe. Spika, kwa hivyo, niseme kidogo nita-*base* kwa akina mama kwa sababu inaonekana tatizo kubwa ndio lipo kwa upande wetu. Hivyo, niipongeze Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa kutafuta daktari bingwa wa akina mama ambaye atatoa huduma kwa muda wa miaka miwili. Hii inaonesha ni jinsi gani daktari huyu ametoka *Auckland*. Hii inaonesha ni jinsi gani kwamba serikali yetu inahangaika kuona kwamba wananchi wake wanapata matibabu ambayo yanayostahiki.

Mhe. Spika, lakini pia, nichukue fursa hii kutoa wito kwa akina mama na wanawake wote, wale ambao wanasumbuliwa na maradhi ya akina mama kama matumbo ya uzazi na kadhalika na mambo yanayohusiana na hayo, wafike katika Hospitali ya Mnazi Mmoja ili kupata huduma hii, kwani huduma hii madaktari kama hawa wanakuwa ni *very rare* kupatikana na wanapopatikana, basi tutumie ile fursa inayopatikana kwa inavyostahiki.

Mhe. Spika, lakini pia, nichukue fursa hii kutoa wito kwa kina mama, tumeambiwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja ukitizama hapa katika takwimu zao, kati ya wagonjwa 50 waliochunguzwa saratani, wagonjwa 35 wamegunduliwa wana saratani ya shingo ya uzazi. Idadi ni kubwa sana. Kwa hivyo, nitoe wito huu tena kina mama kujitokeza kwa hiari na sisi Waheshimiwa Wawakilishi wanawake kwa umoja wetu, tuwaongoze wanawake kwenda kufanya uchunguzi wa saratani, ili kushajihisha wanawake wenzetu nao wawe na tabia ya kufanya uchunguzi wa saratani kwa hiari.

Mhe. Spika nikitoka katika Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja, naomba nimalizie na usafi, nilikuwa namuuliza Mhe. Waziri, kwa nini asitumie njia ile ile ambayo ametumia kuondosha msongamano katika Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa kuajiri Kampuni ya Ulinzi, kwa nini asitumie njia ile ile kuboresha usafi wa Hospitali na maeneo yake yanayozunguka, kwa kuajiri Kampuni ambayo itakuwa inafanya kazi kwa masaa 24 pale, ili kuhakikisha kwamba usafi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja unaimarika.

Mhe. Spika, nikiachana na Hospitali ya Mnazi Mmoja, naomba niingie kidogo katika Hospitali ya Kidongo Chekundu katika ukurasa wa 28. Hapa kidogo nimeshtushwa na ongezeko la wagonjwa wa akili, kuna ongezeko la wagojwa 479 ukilinganisha na mwaka uliopita hii idadi ni kubwa sana. Hapa ningemuomba Mhe Waziri, akija atueleze kwa kina na atoe elimu kwa Baraza na wananchi kwa ujumla. Ni tatizo gani hasa linalopelekea mpaka kunakuwa na ongezeko la wagonjwa wa akili kiasi hiki. Najua kuna sababu nyingi ambazo zinapelekea ukiachia mwenyewe Mwenyezi Mungu *Subhaanahu wa Taala*, kuna sababu nyengine kama madawa na mapenzi pia yanasababisha.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri aje atueleze hasa ile sababu inayosababisha kwamba kunakuwa na ongezeko kubwa la hawa wagonjwa wa akili ni nini? Kwa sababu ongezeko la wagojwa 479 kutoka mwaka jana mpaka mwaka huu sio dogo. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri akija anieleze kwa ufafanuzi kwa faida yangu, faida ya Baraza na kwa faida ya wananchi.

Mhe. Spika, vile vile, nimeona kwamba Hospitali ya Kidongo Chekundu ina mpango wa kujenga kituo cha *Ditoxification Centre*, yaani jengo la kutolea huduma ya matibabu kwa vijana waliathirika na madawa ya kulevya na nimeangalia nikaona kuwa jengo litajengwa kwa gharama za wafadhili.

Mhe. Spika, naomba wakati Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, alipokua akiwasilisha bajeti yake na yeye alikuwa na mpango huo huo wa kujenga kituo cha *Ditoxifiacation Centre* katika maeneo ya Kidimni. Sasa nataka kuuliza kwamba hiki ndio kile kile au wanajenga vituo viwili tofauti na kama ni vituo viwili tofauti kwa

serikali hai-*join force* pamoja, ili kuona kwamba kituo hiki kinajengwa haraka na kinaleta ufanisi zaidi badala ya kujenga tofauti, kama ni kimoja sawa. Mhe. Waziri aje kunielezea.

Mhe. Spika, sasa naomba niingie katika miradi ya maendeleo na kabla sijaingia katika miradi ya maendeleo, naomba nizungumzie kuhusu Idara ya Sera Mipango na Utafiti. Nataka kujua kwanza hii Bima ya Afya imefikia wapi? Mhe Waziri, akija atupe maelezo wamefikia wapi na labda wanategemea lini, kwa sababu imeshakuwa muda mrefu, sasa tumeanza kuisikia katika Wizara ya Utumishi na najua wanafanya kazi kwa pamoja, lakini ni bora wakatueleza ni lini hasa itaanza kufanya kazi, ili wananchi wanufaike na mpango huu wa Bima ya Afya.

Mhe. Spika, nikiingia katika miradi ya maendeleo, naomba nianze na mradi shirikishi wa afya ya mzazi na mtoto. Kama nilivyosema leo nita-*base* sana katika mama na mtoto. Nipongeze jitihada zinazochukuliwa katika kuona kwamba shabaha na malengo ya mradi huu yanatimizwa, lakini bado kazi kidogo haijafanyika vizuri, tuzidishe jitihada, tungependa kuona kwamba hakuna vifo vya mama na watoto kabisa kama ilivyokuwa hakuna malaria.

Mhe. Spika, kwa sababu ukiangalia katika ukurasa wa 57 wamesema kwamba kwa mwaka huu kuna ongezeko la vifo 37. Kwa hivyo, tulikuwa tunaomba kwamba kama walivyochukua jitihada kukawa hakuna malaria, basi ni vyema wakatumia jitihada zile zile ili kuona kwamba hivi vifo vya mama na mtoto vinapungua.

Mhe. Spika, naomba nichukuwe muda katika mradi huu, ili niongelee yale mafanikio na masikitiko kidogo ambayo niliyonayo kutokana na mradi huu. Kwanza katika kifungu cha 13(4) (2), ukurasa wa 58, niungane na hotuba ya Mhe. Waziri kwamba sasa kina mama wamepata muamko sana, niwapongeze kwa kujifungulia katika vituo. Pia, niwapongeze kina baba kwa kuona umuhimu na kuwasaidia wenzawao ili kuona kwamba wanakwenda kujifungulia katika vituo vya afya. Hii nayo itasaidia kupunguza vifo vinavyotokana na uzazi.

Mhe. Spika, vile vile, nimeona kuna maendeleo makubwa kwa kinamama wanaotumia uzazi wa mpango na mimi niungane na hotuba ya Mhe. Waziri kwa kuwapongeza wanawake na kinamama kwa ujumla kwa kuona kwamba sasa kuna umuhimu wa kutumia uzazi wa mpango, hasa katika kisiwa cha Pemba. Katika miaka ya nyuma ilikuwa kidogo kisiwa cha Pemba kiko nyuma kwa watu ambao wanatumia uzazi wa mpango, lakini sasa hivi kuna mwamko mkubwa nashukuru kinamama wamejua umuhimu wa kutumia uzazi wa mpango.

Mhe. Spika, pia, nitowe wito kwa akinababa kutoa ushirikiano katika hili, ili angalau unamuacha mama kidogo anapata afya, halafu ndio anazaa mtoto mwengine, sio kufululiza hapo kwa hapo. Kwa hivyo, niwapongeze kina mama wa Pemba na kina baba wazidi kuwaacha kina mama ili afya zao zirudi kwanza, halafu ndipo wawezalishe watoto wengine.

Mhe. Spika, kwa upande wa Pemba vile vile angalau kuna ongezeko katika kupeleka watoto kupata chanjo. Hili nalo ni pongezi, kina baba nawapongeza sana kwa kuona kwamba kuna umuhimu wa watoto hao kupelekwa kupata chanjo, lakini kidogo nina masikitiko yangu katika kifungu cha 13.4.5, hapa kuna jumla ya wajawazito 47,978 waliweza kuchunguzwa *VVU* katika kliniki na wodi za wazazi. Kati ya hao, kina mama wajawazito 171 waligundulika kuwa na *VVU*. Hapa kidogo nimesikitishwa na idadi hii, lakini niwaombe tu kina baba kwa sababu ukiangalia wao idadi yao ya waliochunguzwa ni 880, lakini waliokutikana na *VVU* ni kina baba 5 tu. Hii inaonesha kwamba idadi ya wale kina baba ni ndogo kuliko ya kina mama.

Mhe. Spika, kwa hivyo, hapa nitowe wito kwa kina mama tu kujilinda zaidi, wasiwaendekeze hawa kina baba ambao kama mnavyoona hapa wao idadi yao ni ndogo ya wenye *VVU*, lakini sisi idadi inakuwa kubwa, nafikiri hii inatokana na ile mmoja kuchukuwa wengi.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, una dakika tano.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Spika, namalizia, nimalizie na mradi wa kusaidia kupunguza vifo vinavyotokana na uzazi, katika ukurasa wa 64. Mradi huu umetekelezwa katika kipindi cha miaka 5, lakini pia, umeongezwa muda wa mwaka mmoja na nusu, basi waziri angetufafanulia japo kwa takwimu faida zilizopatikana kutokana na mradi huu ni vifo vingapi na kwa miaka mingapi vimepungua, ili tuone *effectiveness* yake. Kwa sababu mwaka huu kuna ongezeko la vifo, hebu angetuambia huu mradi umekuwa *effective* kwa kiasi gani?

Mhe. Spika,...

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nawaomba naona mikutano imekuwa mingi kidogo, kiasi cha kwamba inatuvurugia hata *Hansard* yetu. Mhe. Mjumbe malizia.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Spika, katika mradi huu, kwenye ukurasa wa 65 katika kifungu cha mwisho cha mradi huu kinasema, aidha ununuzi wa vifaa kwa ajili ya wodi ya wagonjwa wa akili, yaani *Mental Wing* katika Hospitali ya Wete umefanyika.Nilikuwa najiuliza huu mradi wa kusaidia kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi. Hii wodi ya wagonjwa ambayo kumenunuliwa vifaa vya *Mental Wing*, nilikuwa najiuliza inahusiana vipi na mradi wa kusaidia kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi au hii *Mental Wing* iliyotengwa ni ile ya kina mama ambao wako *mental disturb*, ndio wanajifungulia huko, kwa sababu naona hakuna uwiano. Mradi ni wa kupunguza vifo, lakini huku kuna ununuzi wa vifaa kwa ajili ya wagonjwa wa akili. Kwa hivyo, nilikuwa naomba maelezo kidogo hapa.

Mhe. Spika, baada ya hayo, nakushukuru na naunga mkono hotuba hii ya waziri, lakini nimuombe sana Mhe. Waziri wa Afya aiangalie *sector* ya afya, kwani ni *sector* muhimu inayohusu wananchi. Nakushukuru.

Mhe. Spika: Ahsante sana, naomba sasa nimkaribishe Mhe. Ismail Jussa Ladhu, baadae Mhe. Mgeni Hassan Juma na Mhe. Saleh Nassor Juma ajitayarishe.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu za kusimama hapa nikiwa hai na mzima, sio nguvu zangu, sio jeuri yangu, ni pumzi zake mwenyewe *Subhanahu wa Taallah.*

Mhe. Spika, nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Afya na kwa sababu ya uchache wa muda nimpongeze Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake wa hotuba hii,lakini nieleze masikitiko yangu makubwa sana na mimi nitofautiane na wenzangu waliosema, ikiwa wamesema kwa nia ya kuwa tuonekane tunazungumza lugha nzuri tu sijui, lakini mimi nasema serikali haiwapendi wananchi wake katika suala la afya. Nasema hivyo, kwa sababu sina haja ya kukieleza chochote zaidi ya hotuba hii ya Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, nikiangalia kwenye ukurasa wa 86 kwenye kiambatisho Nam. 12, kuhusu uingizwaji wa fedha za matumizi ya kazi za kawaida katika wizara hii, basi hali halisi inajitokeza, Idara pekee zilizofikia asilimia 90 ni Idara ya Utumishi na Uendeshaji kwa Unguja na Pemba, kwa sababu kuna mishahara, lakini Ofisi Kuu Pemba asilimia 18.1, mipango Unguja asilimia 25, kinga Unguja asilimia 17, tiba Unguja asilimia 22, tiba Pemba asilimia 46, kinga Pemba asilimia 18, Hospitali ya Mnazi Mmoja ndio angalau asilimia 54, bohari kuu ya dawa asilimia 14, Mfamasia Mkuu wa Serikali asilimia 7, Mkemia Mkuu Unguja asilimia 35, Mkemia Mkuu Pemba asilimia 77, Chuo cha Afya Mbweni asilimia 36.

Mhe. Spika, tukitizama hali hii najiuliza mtu anaposema kwamba serikali inajitahidi, ni kigezo kipi kinachotumika, zitakuja wizara tutakuja kuziambia kama tulivyoziambia mwaka jana hapa, katika kuziingizia fedha zinafanya vizuri sana, lakini kile ambacho tumeambiwa ndio kipaumbele cha kwanza cha awamu ya saba *sector* ya afya hali ndio hiyo na hili sio kwa mwaka huu tu.

Mhe. Spika, nakumbuka mwaka juzi nilisimama nikaorodhesha hivi hivi, mwaka jana nikasema haya haya, huu umekuwa ndio utaratibu mzima wa uingizwaji wa fedha katika Wizara ya Afya. Sasa utanishawishi vipi, kuamini kwamba kweli kuna lengo la kusaidia kunyanyua afya za wananchi wetu na kuwatibu wanapoumwa wananchi wanyonge ambao hawana uwezo wa kwenda popote zaidi ya kwenda katika Hospitali za Serikali na vituo vya afya vya serikali.

Mhe. Spika, lakini kama hilo halitoshi, mimi nasema kuna suala moja kuingiziwa fedha, lakini na hicho kinachoingizwa, nini vipaumbele vya Wizara ya Afya na watendaji wake na vipi matumizi yanafanywa. Kuna eneo moja, nimekuwa nikilisema na nitaendelea kulisema na ninamuomba Mhe. Waziri, tunamuambia sijui yeye mwenyewe anafanya nini baada ya kuondoka hapa. Bado sijaona juhudi za dhati za kutazama suala la matumizi ya matibabu nje ya nchi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mwaka juzi nilizungumza na nikatoa mifano hapa na nikatoa hoja na Mhe. Waziri alitoa ahadi hapa kwamba watakwenda kuiangalia tena Hospitali *Miot* Hospital kweli inafaa kuendelea kuwahudumia wagonjwa wetu. Kwa kutoa uzoefu wa watu waliokwenda kule, nimeona wanavyofanyiwa wagonjwa wa Kizanzibari

wakilinganishwa na wagonjwa wengine ambao wanaonekana wana ugonjwa zaidi. Mhe. Waziri aliniahidi kwamba wataangalia Hospitali nyengine.

Mhe. Spika, nilimwambia Mhe. Waziri kwamba sio rahisi kufanikiwa kwa sababu watendaji wake ninavyoamini, wana maslahi katika Hospitali ile. Suala hili limejitokeza tena katika mwaka huu unaomalizika. Alitokezea mtu hapa, tena mtu mwenye hadhi yake kubwa sana hapa Zanzibar, alikwenda, lakini alikwenda kwa shughuli zake na kujitibu yeye mwenyewe binafsi. Akaulizwa na wagonjwa wenzake kama yeye ambao wamekwenda kujitibu binafsi katika Hospitali hiyo hiyo moja, lakini alichokiona ni kwamba kwa maradhi yanayofanana, gharama zinazotumika na mgonjwa anayepelekwa na serikali ni mara tatu ya gharama anazolipa mgonjwa binafsi aliyekwenda kujitibu mwenyewe.

Mhe. Spika, mara tatu na Mhe. Waziri akitaka nitampatia jina la mtu huyo ili akae na azungumze na yeye ampe ushahidi uliokuwepo pale, ndio maana alitupa ahadi toka mwaka juzi, lakini naamini wanamkwamisha watendaji wake, kwa sababu wana maslahi yao katika mradi ule wa kupeleka wagonjwa Hospitali za nje.

Mhe. Spika, hata ukitizama mwaka huu, kuna shilingi milioni 871 kwa upande wa Unguja na kuna shilingi milioni 101 kwa ajili ya kuwapeleka wagonjwa nje ya nchi, sina hakika hata katika uendeshaji wa mfuko huu kwamba kweli Pemba wana maamuzi yao mbali na Unguja wana maamuzi mbali, sina hakika na hilo, lakini katika mgao inaonekana Pemba zimetengwa mbali shilingi milioni 101 na Unguja zimetengwa mbali shilingi milioni 871. Namuomba tena Mhe. Waziri awatazame Wazanzibari wana uchungu wa fedha zao, *change* zilizokuwepo zikawa zinatumika kuwanufaisha watu binafsi badala ya kuwanufaisha wananchi kuwatibu. Suala hili niliachie hapa kwa sababu ya muda.

Mhe. Spika, jengine tunahitaji vile vile, tutizame kama tunavyosema vipaumbele. Nikitizama bajeti hii nasikitika sana kwa mara hii hatuna muda, lakini ningedondoa Idara moja moja humu, kweli kwa makisio, sijui wamepata kiasi gani mwaka huu, lakini kwa makisio nimefanya hesabu ya jumla, ukichanganya vifungu vyao vyote, wana kama 59 bilioni. Ingekuwa watapewa hizo pengine zingenufaisha sana, lakini hata baada ya kupewa ni nini vipaumbele vya watendaji wake Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, nilichokiona mimi humu, mafungu yaliyonona katika vipaumbele kama anawapa na hizo 59 bilioni, ni viburudishaji, matengenezo ya zana, gharama ya *petrol* na *diesel*, gharama za mafunzo. Najiuliza ningetegemea nione kwamba ili na suala hili nimeshalisema humu katika bajeti zilizopita, ili gharama za vilainishaji, mafuta, *petrol*, utengenezaji wa zana iongezeke tena iongezeke, maana yake imeongezeka kwa asilimia kubwa sana, sina muda wa kupitia moja moja, namuomba Mhe. Waziri, aangalie mafungu hayo katika kila Idara ya wizara yake, tungeona kumeongezeka vyombo katika wizara. Kungekuwa kuna ongezeko la gari (*Ambulance),* mapikipiki na mavespa, halafu ndio gharama hizi *corresponding* zikazidi. Uta-*justify* vipi kama hakuna ongezeko la zana, lakini bajeti za maeneo hayo zimevimba.

Mhe. Spika, nataka kutoa mfano mwengine kwamba watendaji wake watamuangusha Mhe. Waziri, aangalie bajeti yake ya utumishi na uendeshaji katika Idara yake Unguja. Utaona kwamba Hospitali katika Idara ya kinga na tiba zimewekewe fungu lake mbali mbali, ungetegemea kuwa mtiririko wa bajeti yake ilivyokaa ya Wizara ya Afya, basi Idara ya utumishi na uendeshaji ingekuwa inashughulika na uendeshaji wa Ofisi, basi wizara. Kwa sababu mafungu mengine yanayohudumia Hospitali huko na huduma zake yako katika mafungu yao, lakini hebu yaangalie.

Mhe. Spika mimi nataka kumpa mfano mmoja tu, kwa sababu sina muda, aangalie kwenye vifaa na huduma, *sub-vote* ya vifaa na huduma katika Idara hii ya utumishi na uendeshaji, mwaka jana ilikuwa shilingi milioni 29 na mwaka huu imepangiwa shilingi milioni 172 milioni, natoa mfano mmoja tu ,lakini tizama mafungu yote ya Idara ile, sasa Idara ile inahudumia Wizara sasa hivi kwa sababu kwenye Hospitali na vituo vya afya mafungu yake katika Idara za kinga, Idara za tiba Unguja na Pemba zimegawiwa vizuri kabisa.

Mhe. Spika, lakini najiuliza vile vile kwamba hii bajeti inafanywa kitaalamu kweli au ishaweza fungu inabandikwa bandikwa tu na nitatoa mfano na naomba kama hili nimekosea Mhe. Waziri akija anirekebishe, kwa vyovyote vile uwiano wa watu kwa visiwa vya Unguja na Pemba haulingani Pemba ina asilimia 37.5 ya watu wake. Kwa hivyo, ningetegemea hata asilimia ya wagonjwa iende kwenye *correspondingly*, lakini angalia bajeti ya chakula cha wagonjwa kwa Pemba fungu limewekwa pamoja lote katika Idara ya Tiba ni Shs. 224 milioni, lakini Unguja ya Jumla imewekwa 162 milioni samahani Hospitali ya Mnazi Mmoja 162 Unguja imewekwa 54, ukiunganisha za

Unguja zote 216, bajeti ambayo kweli imetengenezwa kitaalamu haiwezi kuwa na uwiano kama huu, kwamba kwa uwiano wa wagonjwa utakavyotegemewa kulingana na idadi ya watu ilivyo kwamba gharama za chakula kwa Pemba cha wagonjwa ziwe 224, kwa Unguja 216 watendaji wake wanapanga vipi bajeti hizi.

Mhe. Spika, mimi naamini wanapewa mafungu wakishapangiwa Wizara ya Fedha yanakwenda yanabandikwa bandikwa na hilo tumelisema miaka mingi katika serikali hii, kwamba watendaji siku hizi hawaitwi, Wizara zote wanapewa mafungu wakifika kazi yao kuyapachika katika mafungu yao, wanajua wao wanavyoyatumia na kubadilisha vifungu wanavyotaka wao, tunadanganya tu, sijui kuna *MTEFU,* sijui kuna nini, tunadanganywa sisi na kumdanganya Mhe. Rais kwamba sijui Bango kitita hakuna lolote katika bajeti hiiM ni kiini macho tuM haziingii akilini, hata kwa mimi niliyekuwa si mtaalam wa mipango.

Mhe. Spika, wenzangu wamzungumza matatizo mengine ambayo yapo kama tulivyosema yapo mengi sana hatuwezi kuyamaliza na kwa muda uliotupangia, mara hii inabidi mtu uyataje taje tu, lakini naomba nisaidiwe, vile vile, Wizara imejipanga vipi katika kuhudumia tumeambiwa kipaumbele kimoja, ni kuhudumia mama wajawazito, lakini ukenda katika wodi ya wazazi wamezungumza wenzangu hapa, hata ukitizama kwenye vyombo vya habari unakuta wazazi wako chini wamelazwa kwenye kitanda kimoja wapo watatu, nilikwenda Mwembeladu nimepata *show* kali niliyoiona pale na ungetegemea pale ndio papunguzwe mzigo unaokuja Mnazi Mmoja, leo tunaambiwa hata *Ambulance* huduma za msingi kutoka Mwembeladu kuja Mnazi Mmoja hakuna, sasa tunapoambiwa kipaumbele cha serikali hii ni kuhudumia wananchi katika sekta ya afya katika eneo gani.

Mhe. Spika, nimeangalia bajeti humu na naomba nisaidiwe vile vile kwamba katika ununuzi wa madawa Pemba, nimeliona fungu Unguja, lakini silioni fungu Pemba, lakini kuna 00 pale katika Idara ya tiba, nikategemea labda nitalikuta katika Bohari kuu nimeangalia katika Bohari kuu sikuona kitu nimeona mafungu yamevimba katika yale mafungu niliyoyataja gharama za *petrol* na *diesel*, viburudishaji na matengenezo ya zana kwenye dawa sikuona kitu. Sasa nimeangalia katika sehemu ya maendeleo kwamba labda ziko huku zinategemewa kutokana sikuona kitu. Sasa hebu atwambie Mhe. Waziri hizi shughuli za Bohari kuu zilizotajwa, sio kununua dawa kwanza la msingi.

Mhe. Spika, eneo jengine la kutizamwa kuna maeneo mengine ni usafi, lakini pia, ni utamaduni ukenda katika Hospitali zetu zote za serikali, vituo vya afya ukenda hizo *Cottage* Hospital si za Pemba, sio za Unguja, hali mbaya kabisa, mwaka juzi tulimbana Mhe. Waziri, akatwambia hata bajeti ya usafi hajaingiziwa, sasa sijui hali iko je, maana bajeti imesomwa, lakini uingizwaji wa fedha ilivyom lakini nasema hata wakishazipata vipaumbele vyao viko wapi, tumeona *allocation* walivyoipanga mwaka huu.

Mhe. Spika, kuna maeneo mengine ya maslahi ya watumishi wa sekta hii mwaka jana walitujia madaktari hapa na palikuwa na kasheshe kubwa sana madaktari kutaka kugoma na wakigoma madaktari, maana yake tunaua wananchi wetu tukawanasihi sana walipokuja Wawakilishi tukawaambia msigome masuala yenu tutayaeleza.

Mhe. Spika, mpaka leo bado kuna hoja nyingi sana kuna madaktari wameondoka kuna madaktari wamejitafutia kwenda kusoma kwa sababu wanasema mantiki na maadili ya kazi hawawezi kukaa wakaona watu wanakufa mbele yao, tumewakosa wengi na tutaendelea kuwakosa kila siku kwa hali hii, hata watumishi wengine kuna posho zao mali mbali kuna *night allowance*, *risk allowance* na kuna madaktari wanataka wapewe posho la dhamana zote hizi hazipatikani kiutaratibu.Sasa najiuliza wengine wanasema imeshafika miaka mitano hawajapata, *Management* ya Wizara ya afya wanafanya nini katika haya, *priority* yao ni kusafiri tu basi.

Mhe. Spika, angalia katika hilo buku, angalia mafungu ya safari na katika hili nataka kauli ya Mhe. Waziri wa fedha serikali itujibu hapa inatwambia nini na inafanya nini, maana Waziri wa fedha alipokuja hapa alitwambia kwamba serikali imeamua.

Mhe. Spika: Unazo dakika tano.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, nitamalizia, hivyo hivyo ingawa nimebakisha mengi sana alitwambia hapa kwamba wameamua mara hii kupunguza semina na mikutano yakifanyika yafanyike katika mikutano yao, kupunguza safari, lakini humu nikiangalia bajeti ya Wizara ya Afya haitoi picha, mafungu ya safari yamenona kila pahala safari za ndani na safari za nje, sio kwa wagonjwa ila kwa watumishi wao. Kuna nini katika hili na tunaona safari zinavyokwendwa, hii ndiyo *priority* ya Wizara ya Afya na hii ndio *priority* ya serikali hii, isijali wananchi masikini wanyonge wa nchi hii.

Mhe. Spika, kuna suala alizungumza Mhe. Jaku hapa, unakwenda katika Hospitali yetu ya rufaa lifti unakwenda haifanyi kazi, kuna lifti upande mmoja limekaa pale kama vile *Beit el ajab* limebakia sanamu tu, pale kwa kuwa watu wajue kuna mwaka Zanzibar ilikuwa na lifti basi, hata haya tutaambiwa hakuna fedha vile vile. Kuna suala la jiko la kuchemshia vifaa katika *Emergency Theater,* kifaa cha kuchemshia vifaa vile ni shilingi 80,000, basi Wizara nzima ishindwa na 80,000/= au siyo *priority,* wala sio kipaumbele, watendaji kufuatilia mambo kama hayo.

Mhe. Spika, mimi nataka kusema kwamba kuna masuala mengi, lakini kutokana na muda kuna moja nataka nilizungumze kwa sababu lote ni jimbo langu. Serikali imekuja na mpango kwamba Hospitali ya Mnazi Mmoja ni Hospitali ya Rufaa wengine wote wapate rufaa kutoka katika vituo vyao, kuna wananchi wa Jimbo la Mji Mkongwe Hospitali ya Mnazi Mmoja ipo katika jimbo lao, anakwenda pale anaambiwa aende Rahaleo, Kwamtipura, Mpendae, hata katika Hospitali za Rufaa kubwa kubwa duniani kunakuwa na kitengo kinahudumia wagonjwa wanaohitaji huduma za haraka katika maeneo yale kote duniani, sasa mwananchi wa Mji Mkongwe anaumwa unamwambia aende Rahaleo na huko Rahaleo ulikomwambia aende au Kwamtipura tunajua sisi hali ilivyo vile vile, madaktari wenyewe hatuwajui idadi iliyokuwepo, unawasambaza katika hali hii.

Mhe. Spika, nataka maelezo nukta hizi, la si hivyo, mimi peke yangu, lakini nitaikwamisha bajeti hii, nitaikwamisha kwa sababu mbili; moja kama ni *protect* kwa serikali kwamba haina nia ya kusaidia wananchi wa nchi hii sababu ya uingizaji wa fedha hivi ulivyo, lakini pili kwamba na vipaumbele vya Wizara ya Afya yenyewe haviko katika kuhudumia sekta ya afya viko katika huduma ya kujuhudumia wao wenyewe watendaji wa Wizara ya Afya. Siungi mkono mpaka niridhishwe, Ahsante sana.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mhe. Spika, awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetujaalia leo kufika hapa tukiwa wazima wa afya, nikushukuru na wewe kwa kunipa fursa ya kuchangia katika hotuba ya Waziri wa Wizara ya Afya.

Mhe. Spika, mimi nichukue fursa hii kumpongeza binafsi yeye mwenyewe Waziri, Naibu Waziri, pamoja na Watendaji wake wote wa Wizara ya Afya, hususan Katibu Mkuu pamoja na Wakurugenzi wa Wizara hii. Pongezi hizi sizitoi tu kwa kuwa nataka kusifu hii hotuba au laa, lakini natokea pongezi kwa sababu wanafanyakazi ngumu katika mazingira magumu hasa kwa kuwa kile ambacho wanapewa ni kidogo sana kutokana na yale ambayo wanayapanga.

Mhe. Spika, nataka kuzungumzia suala zima kwanza ni jambo ambalo kwa kweli linanitia wasi wasi, ndio maana nalizungumzia na mengine sitoweza kuyazungumzia sana kwa sababu mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii na Wizara, hii imo ndani ya Kamati yangu. Kwa hivyo, mengi ambayo tumeyaona katika kazi zetu mbali mbali za Kamati tayari tumeshayazungumzia ndani ya ripoti yetu.

Mhe. Spika, kwanza nataka kuzungimzia suala la mradi wa kupunguza malaria, tumeona kwa kipindi kirefu sana, tukiwa na mradi huu kuna punguzo kubwa la maradhi haya ya malaria, hilo wenyewe binafsi tumeliona hasa katika kupungukiwa na wagonjwa katika Mahospitali, lakini hata majumbani mwetu, lakini mimi nitazungumza zaidi ya mradi huu, kwa sababu naanza kuona kwamba mradi huu unaanza kusahaulika na kutofikiriwa kwamba ni mradi ambao niwa kipaumbele cha Taifa letu.

Mhe. Spika, mradi wa kupunguza vifo vya wanawake na watoto hautaweza kufanyika ikiwa suala zima la kupunguza malaria litakuwa halipo, mradi huu karibu unamalizika, lakini hakuna mpango wowote ambao umepangwa kuhakikisha kwamba mradi huu utaweza kuendelea, tukiwa katika Kamati tumelizungumza sana hili na mimi mwenyewe tumewahi kukaa kwenye Kamati ya Wanyeviti nikalizungumza pamoja na Makatibu Wakuu na Waziri alikuwepo pale kuhusu mradi huu, mradi huu bado serikali haijajipanga, lakini Wizara ya Afya ilishauri Wizara ya Fedha namna ya kuweza kupatikana fedha za kuendeleza mradi huu.

Mhe. Spika, nasema hivyo, kwa sababu mradi huu hapo mwanzo tulifadhiliwa, lakini kama tunavyofahamu wafadhili wengi wanaondoka na hata sasa sio tu kuwa wanaondoka, lakini lazima serikali itie nguvu ili kuhakikisha kwamba mradi huu basi unatekelezwa vizuri, sasa tatizo hilo nalizungumza na namtupia Mhe. Waziri wa Afya, lakini namuelekeza kwa Mhe. Waziri wa Fedha, kama tutadharau mradi huu, basi tunahakikisha kwamba vifo vya akina mama vingi vitaongezeka pamoja na watoto. Naomba sana tunusuru Waziri wa Fedha uje hapa utwambie

katika Wizara hii utwambie leo nitaondosha shilingi, lakini naiondosha shilingi kwa kumuelekeza Waziri wa Fedha, sitokubali kupitisha wizara hii ikiwa wizara haitakuwa na kifungu cha malaria, sitokubali.

Mhe. Spika nasema hivyo, kwa sababu najua Zanzibar tumekuwa tukipunguza vifo vya wazazi na watoto ukilinganisha na wenzetu Bara kwa sababu ya kupunguza malaria, kwa sababu malaria tumeweza kuidhibiti sasa ikiwa tutaacha na hatutoweza kufikiria vipi vya kuweka fedha na kuendeleza miradi hii, tukiona kwamba tutapata fedha za wafadhili, haitowezekana na tayari wataalam wetu wa Wizara ya Afya wametoa mpango kamili Wizara ya Fedha ikae ifikiri kama haikukaa haikufikiria, mimi nitaondosha shilingi.

Mhe. Spika, jengine nazungumzia suala zima kwanza nipongeze sana Wizara kwa juhudi zao ambazo tayari wameshazifanya kuongeza katika ukurasa wa 61, wakizungumzia mradi wa kupandisha hadhi Hospitali za Wilaya na vijiji. Mimi nipongeze sana mpango huu, ni pamoja na kuongeza hadhi na kuifanya Hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa Hospitali ya Rufaa, lakini bado kuna changamoto nyingi sana na moja katika changamoto kubwa nafikiri wenzangu wengi wamezungumzia hili suala zima la uingizwaji wa fedha katika Wizara hii. Tunasema afya ni moja katika mambo muhimu ya Taifa hili, bila ya kuangalia afya ya kila mwananchi, hatutokuwa na wananchi ambao wataweza kufanya kazi kwa sababu watakuwa wanaumwa sana, lakini vile vile, vifo vya wananchi katika nchi hii vitaongezeka.

Mhe. Spika, suala la fedha kuingiziwa Wizara hii, kwa kweli ni changamoto kubwa na namuona Waziri wa Fedha na namwambia Waziri wa Fedha kwamba hii ni changamoto kwa sababu tukipita katika kila wilaya, changamoto kubwa hawana vifaa vya kufanyia kazi, vifaa vyengine ni aibu kusema na hatuwezi kuwalaumu watendaji, wala hatuwezi kuilaumu Wizara, lakini uingizwaji wa fedha katika maeneo hayo unakuwa mbaya, mimi nimpongeze Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwa kuona na hili nafikiri ni tatizo, sijui wapangaji wetu wabajeti wako je? Sijui wanafanyaje, lakini hali halisi haiwezekani kwamba leo zichukuliwe fedha ziingizwe katika mafungu ambayo tunaona kwamba hayana umuhimu na inawezekana sana haya mafungu ndio yale pia yaliyokuwa hayaingizwi yanabakia huko huko. Kwa hivyo, mimi nina wasi wasi sana na bajati yetu kwa ujumla wake lazima turudi tena tuitizame, kwa kweli kuna vifungu vingi unaweza kushangaa kwa nini hiki kimepewa *priority* kuliko kingine.

Mhe. Spika, jengine ninalotaka kuzungumzia ni suala zima la uzazi wa mpango, mimi nimefurahishwa sana kuona kwamba kwa wenzetu wa kisiwa cha Pemba wamepiga hatua katika mpango huu, lakini nafikiria ni juhudi ambazo zimechukuliwa na wananchi wote kwa ujumla pamoja na viongozi wao, kwa sababu hapo zamani kulikuwa na tatizo hili, lakini baada ya Wawakilishi wetu wengi kulizungumzia hili tatizo, basi hili tatizo sasa tunaona linaondoka kidogo kidogo, ningewaomba sana Wawakilishi wa kisiwa cha Pemba, sio Pemba tu, lakini hata Kaskazini Unguja kuna tatizo hilo, kwamba wafanyekazi pamoja na watendaji wa Wizara ya Afya kuhakikisha kwamba basi yale ambayo yanapangwa na Wizara hii, basi kuwasaidia kwa sababu wananchi wengi wanategemea sana kauli za viongozi wao wa kisiasa.

Mhe. Spika, kwa hivyo, mimi niwapongeze sana Wizara kwa hatua hiyo waliyoifikia, lakini vile vile, ningesisitiza kwamba sisi wanasiasa tuna jukumu kubwa la kuweza kuwasaidia wananchi wetu katika masuala hayo.

Mhe. Spika, mimi nataka kwenda katika kurasa ambayo inazungumzia changamoto vile vile zinazokabi Wizara hii, Changamoto ambazo zinakabili Wizara hii ni suala zima hawa wauzaji wasio rasmi wa dawa za asili, hili ni tatizo, lakini vile ambavyo tumezungumza jana katika Wizara Katiba na Sheria, tukisema kwamba Sheria tunazo, lakini hatuzitekelezi, inawezekana sheria kama hii ipo, lakini utekelezaji wake umekuwa mgumu kwa sababu ya mazingira yaliyokuwepo, sasa hivi mimi ningeiomba Wizara kuitizama sheria inayohusiana na masuala ya dawa za asili ili kuhakikisha kwamba wananchi wetu hawadanganywi wakatumia dawa ambazo sizo za asili na matokeo yake sasa tunaona mzigo unarudi pale pale serikalini.

Mhe. Spika, lakini niiombe sana Wizara yako kwamba uhakikishe kwamba elimu ya masuala ya maradhi hasa yale yasiyoambukiza, masuala ambayo ya maradhi hasa ambayo sasa hivi yamekuwa ni maradhi makubwa, masuala ya sukari na saratani, lakini wananchi waelimishwe kwa sababu wengi, wanakata tamaa na wengi wanarudi katika dawa za asili kwa sababu labda wanaona kwamba kwenye Mahospitali yetu hamna matibabu na ndio maana hasa ya kutumiwa hizi dawa za asili, sio kwa sababu watu wanatumia tu, lakini wanakata tamaa.

Mhe. Spika, sasa mimi ningeomba sana wizara yako kwamba ihakikishe katika vitengo hivi, basi dawa ziwepo, lakini vile vile, wale ambao wagonjwa wa maradhi haya, basi huduma iwe nzuri zaidi. Wataacha tu pale ambapo

kwamba huduma zitakapokuwa nzuri zaidi na dawa zitakuwepo. Mimi ninaamini kabisa mgonjwa yoyote huwa anatapatapa na anapotapatapa atakwenda kuchukua dawa yoyote ambayo ataambiwa na mtu yoyote kwamba hii inafaa, lakini ikiwa matibabu yale yapo Hospitali na ni mazuri, hawezi kwenda sehemu nyengine.

Mhe. Spika, ninasema hivyo kwa sababu maradhi haya si ya Zanzibar peke yake, lakini nchi zilizoendelea, wenzetu hapa mtu inakuwa pigo kubwa akiambiwa tu kwamba ana ugonjwa wa sukari. Kwa nchi zilizoendelea ugonjwa wa sukari, sio tatizo mradi tu mtu akiweza kutumia dawa anazoandikiwa na daktari, lakini na kutimiza yale masharti anoambiwa tatizo hapa liwe kila siku, gonjwa hili linazidi kukua. Sasa tatizo liko kwenye kumhudumia yule mgonjwa. Naomba Mhe. Waziri, hilo watendaji wako waliangalie vizuri ili kwa sababu hata hizo dawa ambazo tunasema za asili, basi dawa za asili ziko nzuri na wanaweza kutumia, lakini lazima serikali au wizara itie mkono katika suala hili.

Mhe. Spika, ninazungumzia suala zima la wafanyakazi wako katika changamoto, umesema kwamba sasa hivi kumekuwa na jitihada za serikali kuajiri na kuwapeleka masomoni wafanyakazi. Mimi niipongeze sana wizara ya Mhe. Waziri, kazi hiyo kwa kweli inafanywa nzuri, wengi wanaondoka kwenda kusoma kuongeza utaalam wao, lakini kuna tatizo hapa Mhe. Waziri na tatizo hili tumeshawahi kulizungumza katika Kamati. Mhe. Waziri, unafahamu na Mhe. Mshimba alisema jana kuna muongozo ambao umetolewa na Wizara yako kwa wanafunzi ambao wanataka kusomea masuala ya afya waliomo ndani ya Wizara yako.

Mhe. Spika, tunajua kwamba Wizara yako inahitaji wafanyakazi wengi sana wenye taaluma mbali mbali, lakini hawawezi kutoka tu wakenda wakasoma bila ya kupata idhini ya wizara yako ikiwa kama muajiriwa. Hilo linatokea wengi wanaondoka wanakwenda kwenye mafunzo, lakini huku tukiwa hatuna wafanyakazi ndani ya wizara yako wafanyakazi hao wanaondoka wanaacha pengo. Kwa kweli hilo ni tatizo na ni tatizo kubwa lazima kufatwe utaratibu ambao umekubalika, hatuwezi leo tunaamua kwamba wasiondoke hawa tukaweka hesabu vizuri, halafu baadae tena inakuja kubadilishwa hapana wende. Mhe. Waziri, hilo ndani ya Wizara yako linafanyika na kwa bahati mbaya sana kwa kweli inapunguza uwezo wa wafanyakazi ndani ya Wizara yako.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri, wataalamu wengine ndani ya Wizara yako ambao ni watu ambao tunawategemea wanabadilisha, leo anatoka anaacha kazi yake ambayo inategemewa anakwenda kusoma vitu ambavyo havitakiwi na hilo si Wizara yako tu mpaka Wizara ya Elimu tumeligundua. Anatoka mtu *technician* anakwenda kusoma mambo ya *Human Resource* imehusu nini? Tunapungukiwa Mhe. Waziri, lazima tufate mpango ambao wizara imekubali, uongozi mzima umekubali kwamba huu ni mpango ambao tutautumia, *otherwise*, Mhe. Waziri, tutakuwa kila siku tunalalamika kuhusu masuala ya wafanyakazi.

Mhe. Spika, mimi nimalizie tu kwa suala zima la mfumo mzima ambao amesema kwamba katika malengo yake wa kufanya *performance apprises system.*

Mhe. Spika: Unazo dakika tano.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mimi nipongeze sana kwa hili na nilipongeza kwa sababu hii ni *system* ambayo itasaidia sana kuwapa moyo wafanyakazi wa Wizara ya Afya. Sisi sote tunazungumza hawa wafanyakazi wa Wizara ya Afya wanafanya kazi sana na wanafanya kazi katika mazingira magumu, lakini katika kipato kidogo, tukubali hilo. Wakiondoka wakivuka maji na wakenda kwengine, wanatakiwa sana, lakini tunapoanza kuwatupia kitu lawama wao, kwa kweli saa nyengine tunakosea. Wapo wafanyakazi ambao kwa kweli wanajitahidi sana. Mimi ningeomba sana mfumo huu wa *performance apprises system* uwe ni mfumo wa haki ambao mtu hatotizamwa sura, wala jinsia...

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tumsikilize Mhe. Mjumbe, anachangia hatutakiwi tuseme kwa ghasia tunong'one.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mhe. Spika, na wala anatoka wapi, atizamwe mtu kutokana na utendaji wake wa kazi. Nasema hivyo kwa sababu wizara yako ina wafanyakazi wazuri sana wanawake, lakini katika Idara zako na hili ni la kwako wewe, wala sio la Mhe. Rais peke yake. Niambie kuna Kurugenzi nane kama sikosei ni mmoja tu mwanamke, Dr. Salhia ambaye keshokutwa na yeye anataafu.

Mhe. Spika, tunataka kuona nyuso za wanawake kwa sababu tunajua wanaweza katika wizara hii wanaweza, wapewe na wao nafasi na hii *system* ndio maana nikakwambia kwamba isitizame na jinsia, haya malengo ambayo umeyapanga mimi sisemi kwamba wasipewe wasioweza, nasema wapo wanaoweza na nina uhakika kwa sababu ninawajua. Kuna watu ambao wana uwezo mzuri wa kuweza kukamata na kuongoza Idara zako, Mhe. Waziri waone wanawake hao ili uweze kutekeleza kazi uliyopewa na nchi hii, kazi hii hutoifanya peke yako, utaifanya na watendaji wako na sisi, lakini pamoja na wananchi wote.

Mhe. Spika, la mwisho kabisa nasisitiza lile lile ambalo nimekuwa nimelisema tangu hapo awali na naomba sana Mhe.Wizara ya Fedha kuwatilia fedha vizuri kwa sababu bila hayo, kuna Hospitali nyingi Wilayani ambazo zina matatizo mengi, hawana umeme, umeme umekatwa Mahonda, imekatiwa juzi, wanatwambia kwamba jamani tumekatiwa umeme *Ultrasound* haifanyi kazi na nyengine Pemba tumekwenda nyingi wamekatiwa umeme. Namuomba Waziri wa Fedha hayupo, lakini atanisikia, namuomba sana kwamba fedha katika Wizara hii basi iwe ni Wizara ya kwanza, iongoze katika kutiliwa fedha vizuri ili kuendesha wizara yako.

Mhe. Spika, nakushukuru, naunga mkono hotuba.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipatia fursa ya kutoa mawazo yangu kuhusu hoja iliyopo mbele yetu. Kabla ya kuanza kuingia kwenye hoja, nitumie fursa hii kukushukuru kwa kunipatia fursa na kwanza nimpongeze Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii Wanawake na Watoto ya Baraza letu kwa kututaka sisi tuendelee kutoa taaluma ya uzazi wa mpango kule Pemba, sisi ni wataalamu sana katika mambo haya Wawakilishi wa Majimbo kule Pemba. Sasa tungemuomba asitwambie Pemba tu na atuambie mpaka Kisiwa hiki cha Unguja tuje tufanye kazi vile vile ya kutoa taaluma katika masuala mazima ya *Birth control* na sisi wataalamu na hatutumii *pills* ila tunatumia *natural control,* tunawaelimisha kinamama na hawatumii madawa kwamba yatawaathiri. Kwa hivyo, tungeomba na huku waturuhusu. Baada ya maelezo hayo, nende moja kwa moja sasa katika hoja iliyoko mbele yetu.

Mhe. Spika, leo tutazungumzia Wizara ya Afya. Kama kuna Wizara ambayo inatakiwa iwe makini sana katika kutoa huduma zake ni hii na kama serikali iliyopo madarakani inatakiwa iwe makini na kuhakikisha kwamba nguvu zake nyingi inazielekeza katika Wizara hii ya Afya.Nimefanya utafiti haujakamilika, lakini nimefanya nusu ya utafiti wangu inaonesha nchi kadhaa katika ulimwengu bajeti ya Wizara ya Afya haiteremki asilimia 35, hata zile zilizoko Kusini mwa Jangwa la Sahara. Inasikitisha sana kwamba serikali iliyo madarakani, Wizara yetu ya Fedha haiko makini katika kupanua bajeti yake kwa hii Wizara.

Mhe. Spika, mimi napenda nitumie fursa hii kuwapongeza kuanzia Waziri, Naibu Waziri na katika benchi la ufundi la Wizara ya Afya kwa jinsi walivyokuwa wataalamu katika shughuli zao, lakini hawawezeshwi. Huwezi kumlaumu dereva kwamba gari haitembei huku huifanyii *service* wewe tajiri na kuitia mafuta, ikiwa gari huitii mafuta na huifanyii *service,* wa kulaumiwa sio dereva ila ni mmiliki wa ile gari kabisa kabisa.

Mhe. Spika, mimi naomba kwamba hii bajeti hii Waheshimiwa tukubaliane kwa pamoja kwamba bajeti ya Wizara ya Afya irudi serikali ikakae kitako ione jinsi gani inaweza kuipanua ili wananchi wa nchi hii tuweze kunufaika na hii *National cake* ya nchi, inasikitisha. Mimi ninaamini *team* iliyopo Wizara ya Afya ikiongozwa na mchumi Mhe. Juma Duni Haji na daktari aliyebobea katika masuala ya tiba ambaye ni Naibu Waziri na Katibu Mkuu aliyebobea katika masuala haya ya kupasua pasua mambo ya mishipa na mambo mengine na lile *bench* la ufundi lile la Wakugenzi kama tutawawezesha, basi nakuhakikishia ugonjwa Zanzibar ibake rehma ya Mwenyezi Mungu, lakini kwa mbu mbu hawa, naamini sana wangefanya kazi ya ziada hawa ni wataalamu bwana. Mimi nikiliangalia lile *bench* pale, si dhani kama yuko aliyeikosa *degree* mbili katika wale pale.

Mhe. Spika, lakini inasikitisha kuona kwamba Wizara ya Afya ambayo tulikuwa nayo sisi katika miaka ya 1970, inafanya vizuri siku zile Mzee Kingwaba Hassan Kingwaba ilikuwa tumemkabidhi ile wizara. Ukiangalia hiyo *Staff* ya Mzee Kingwaba Hassan Kingwaba ilikuwa haina ma-*degree holders* kama wale ilikuwa na kina *Assistance Medical Officer* na *Medical Assistant,* lakini walikuwa wakifanya kazi nzuri kwa sababu ilikuwa tunawawezesha. Leo hapa kuna wataalamu waliobobea akina rafiki yangu pale Katibu Mkuu Dr. Jidawi, rafiki yangu pale ila jamani hawafanyi vizuri kwa sababu hatuwawezeshi hawa, tusiwalaumu, wa kulaumiwa ni Wizara ya Fedha. Kwa hivyo, nawaomba sana Waheshimiwa tuikataeni hii bajeti irudi ikapanuliwe hii. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kutokana na ufinyu wa bajeti wa Wizara hii, huduma za afya katika nchi hii zimekuwa tete, nianze na Hospitali ya Chake Chake pale. Hospitali ya Chake Chake ni Hospitali iliyoko kati kati ya mji wa Pemba, ni Hospitali ambayo sisi wakaazi wa Kisiwa kizima cha Pemba, pamoja na wageni tunaitegemea kwa kiasi kikubwa. Inasikitisha kwamba pale pana tatizo sasa, sio la dawa tu, lakini hata vifaa havipo. Mimi kuna mwana CCM mmoja nilikuwa ninampiga kampeni sana kipindi kile cha uchaguzi aje kwenye CUF ambaye ni miongoni mwa CCM sana katika Wilaya ya Chake Chake anaitwa Abdalla Ng'onda.

Mhe. Spika, huyu Abdalla Ng'onda nilimwambia udhaifu wa nchi hii njoo zako kwenye CUF hakukubali, juzi alikwenda kwenye Hospitali hii kumpeleka mtoto wake siku ya tarehe 16, Abdalla N'gonda ambaye ni CCM, nadhani alikuwa anashindwa na Mwalim Nyerere tu katika nchi hii kwa u-CCM. Laiti angelikuwa akijitokeza tokeza huku, huyu naamini angepewa nafasi kubwa. Abdalla Ng'onda huyu juzi ile siku ya tarehe 16 Mei, mtoto wale Khadija Abdalla Ali binti yake mwari, huyo tena alipata tatizo la pumzi, saa sita za usiku alikuwa hawezi ku-*inhale oxygen*, akawa anapata tatizo na akapelekwa katika Hospitali ya Chake Chake pale.

Mhe. Spika, alipopelekwa Hospitali ya Chake Chake, Khadija huyu na baba yake mwana CCM Abdalla Ng'onda, alipofika pale Abdalla Ng'onda akatumia uenyeji wake kwa sababu ana *power*, chama chake ndio hicho na akaenda kutaka matibabu akaambiwa ende akapimwe *pressure.* Chake Chake nzima *pressure machine* haikupatikana, unaona na yule mtoto akawa katika mazingira magumu, lau kama ingelikuwa si yule kijana kwamba hana hela kwa sababu Abdalla Ng'onda, ni tajiri siku ya pili akamkimbiza Dar-es-salaam, lakini angekuwa ni mtoto wa Mwasiti binti Juma pale Vitongoji Umangan, naamini angepata tatizo kubwa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sasa tuone hiyo hali siku ile ile ya tarehe 16 alikuja mwizi mmoja alishapigwa, lakini na yeye ni sehemu ya wananchi wa nchi hii alikwenda huko akaiba akakamatwa akapigwa pigwa kidogo kaletwa Chake Chake Hospitali siku ya tarehe 16 Mei, 2014 huyu kijana anaitwa Nassor Ali Salim, sio Jazira huyu, ni katika vibaka vibaka hawa. Sasa huyu alipofika pale ikabidi panatakika aoshewe na nini kufutwa futwa mambo ya *iodine*, ilitafutwa *iodine,* wakahangaika Hospitali nzima haikupatikana, wakakimbilia Vitongoji, haikupatikana, kila pahala ikabidi aoshwe kwa maji avungwe vungwe na ma-*bandage* yale na manini.

Mhe. Spika, sasa hata *iodine* ni tatizo, yaani tatizo lilitukumba katika miaka ya 1980, hapa mimi nadhani Mhe. Mzee Aboud Jumbe bado yuko hai, nadhani anaweza akafahamu fahamu kidogo, naomba serikali iende ikamsikilize yule mzee, utaratibu gani ulikuwa ukitumika. Kwa sababu Dkt. Kingwaba ukimuangalia kitaaluma bora Dkt. Jidawi mara 100, lakini alimudu ku-*handle* kipindu pindu katika miaka ya 1980 vizuri tu pamoja na kwamba ilikuwa ni mara ya mwanzo kutuvamia, lakini mimi kipindi kile tulikuwa tuna wasiwasi Dkt. Kingwaba na *Staff* yake siku zile wakafanya kazi ya ziada pamoja na elimu yao ndogo, kwa sababu serikali ya nchi ilikuwa inawawezesha wawezesheni na hawa wataalamu, tuwawezeshe ili watutibu. Inasikitisha sana mimi sijui wanafanya hivi serikali kwa sababu hawajui au kwa sababu hawa serikali yetu hii, hasa Wizara ya Fedha haijui kama sisi ni maskini hakuna viwanda, kwa sababu nchi zenye viwanda ndio zenye kuwadharau walipa kodi.

Mhe. Spika,lakini leo mlipa kodi akiwa na homa, mlipa kodi akishikwa na shuruwa, mlipa kodi akenda Hospitali hatibiwi, ni mgonjwa ataweza kulipa kodi? *Tax spares* ndio mpaji wa nchi. Ukianza kuwadharau walipa kodi katika nchi maskini kama hii, unadharau uchumi wa nchi yako. Mimi ninafikiri lile wazo langu kwamba naomba tena Waheshimiwa tuliungeni mkono ili bajeti irudi iende ikafanyiwe marekebisho ili wawezeshwe hawa wataalamu wetu waweze kuwatibu wananchi wa nchi hii na hatimaye waweze kulipa kodi ili nchi ipate itononoke kiuchumi.

Mhe. Spika, tatizo jengine lililo kubwa pale Chake Chake na Pemba kwa jumla ni tatizo la madaktari.Pemba nzima wakaazi karibu laki tano wanahudumiwa na madaktari watatu wakiwemo ma-*specialists* wawili na *MB* mmoja unaona. Hebu tufanye hesabu watu laki tano tu ambapo nina hakika wapemba wanazidi laki tano wanaoishi pale Pemba. Tuwagawe kwa madaktari watatu. Kila daktari atawahudumia Wapemba wangapi pale.

Sasa Mhe. Spika, katika hili mimi ninadhani hata Mwalimu alipotunga kitabu chake, akisema kwamba ili tuendelee tunahitaji mambo manne; watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora. Sasa watu ili tupate maendeleo ni lazima tuwajali. Leo Pemba nzima watu karibu laki tano wanatibiwa na madaktari watatu tu, *specialists* wawili na *MD* mmoja. Hili ni tatizo na ikiwa fedha za kuwasomesha madaktari hapana basi ndio nikasema hii bajeti irudi waingize mambo ya kuwa-*train* madaktari waongezeke kule. Hebu Mhe. Waziri ukija uniambie kila watu wangapi wanatakiwa kutibiwa na daktari mmoja.

Mhe. Spika, tatizo jengine pamoja na bajeti finyu muliyonayo Wizaya ya Afya lakini inaonekana kama kitu jeuri jeuri hivi. Sijui jeuri hii inatokea wapi. Dawa zinachelewa kufika pale Pemba na zikishafika hizo dawa zinachelewa kusambazwa katika mahospitali. Sasa hii ni nini. Hicho kidogo tulichonacho tukishakukipata basi kiwafike wananchi. Leo dawa zinafika leo Pemba, zinaweza zikachukua karibu wiki mbili tu zipo hazigawiwi. Sisi tuna-*achieve* ile *millenium goal* ya kuweza kufanya ile wanaita *reduce child morterlity rate*. Ile *millenium goal* hatutaifika kwa sababu hata hao akinamama wanaotaka kujifungua, watoto wanaotaka kupimwa uzito huo, madaktari hakuna.

Kwa hivyo hicho kiwango cha kupunguza vifo vya mama na mtoto havitapatikana pamoja na kwamba mjukuu wangu pale kasema kwamba vimepungua. Lakini hali ni hiyo katika maeneo mengine kabisa kabisa. Mhe. Spika, miongoni mwa watu wa kuwaenzi, kuwapembejea na kuweza kuwafanya wajali kazi zao basi ni hawa madaktari na *clinical officers* pamoja na ma-*nurses*. (*Makofi*)

Mhe. Spika, tatizo tulilonalo pamoja na bajeti ndogo iliyonayo wizara hii katika kipindi kirefu hiki, lakini inaonekana wafanyakazi wenu wakiwemo madaktari, *clinical officers, nurses* ni tatizo kwamba hizi wanaita *night call allowances* hawapewi. Mhe. Spika, mimi ninazo takwimu tangu mwaka 2013. *Clinical officers, nurses* na hawa *doctors* hawajapewa haki yao ya *calls*.(*Makofi*).

Mhe. Spika: Una dakika 5.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, unapochelewa haki ya mtu sio kwamba unamvunja moyo tu, akawa hawezi kufanya kazi daktari, lakini unamdhulumu kwa mujibu wa Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria anasema kwamba, *"The justice delays the justice denied"*. Sasa mimi ninadhani katika hili Mhe. Spika, tusiwadhulumu hawa kwa kuwacheleweshea haki zao. (*Makofi*).

Mhe. Spika, huduma ya makaazi kwa wale vijana wetu ambao wanaomaliza chuo tukawahamishia katika maeneo mengine Unguja na Pemba. Wale wanaomaliza kwenye vyuo kwa mfano *clinical officers* na wengine katika kada ya afya. Hii huduma ya makaazi inakuwaje kuwaje. Maana juzi mmoja nilimsikia Mwakilishi wa Jimbo la Kojani anasema kuwa nimeambiwa nimpatie nyumba nani kule Kojani. Kwanza huku Kojani hizo nyumba zipo za kumuweka huyo daktari?

Mhe. Spika, ninafikiri hawa wangefanyiwa jambo moja. Hiyo *house allowance* waingiziwe kwenye mishahara yao. Lakini leo kule Pemba mumewakwamiza idara, mumewafanya idara wawahudumikie na wakati fungu la nyumba halimo katika wizara. Sasa mimi hawa ninafikiria muwaingizie katika mishahara yao hii ya mambo ya makaazi kule, kwa sababu mtu anaweza akalala Chwale akenda akafanya kazi Kojani. Sio muwalazimishe kuwaweka kisiwani kule, wengine wanakimbia hawakubali kukaa kule.

Mhe. Spika, jengine ni huduma ya chakula. Mhe. Spika, Idara ya Tiba hii inayohudumia hospitali hizi tano, inatoa shilingi milioni mia mbili kwa ajili ya chakula cha wagonjwa, ikiwemo Kivunge, Wete, Chake-Chake, *Vitongoji cottage* na kadhalika. Lakini ninataka nielezwe mgao huu unakuwaje Mhe. Spika, kwa sababu *Vitongoji cottage* hospital wanapata milioni kumi na mbili tu katika milioni mia mbili. Hebu ninataka uje unifafanulie vizuri Mhe. Waziri kwa sababu hili ni tatizo.

Kwa sababu Makunduchi na Kivunge kila mmoja inapata milioni ishirini na tano, na zote ni *cottage hospitals*. Lakini Vitongoji au kwa sababu ipo karibu na bahari huku, naona wanapata milioni kumi na mbili tu. Sasa ninataka Mhe. Waziri ukija hapa kwa umakini mkubwa uje unieleze ilikuwaje Makunduchi na *Kivunge cottage hospitals* wa-*differ* sana na *Vitongoji cottage* hospital kwenye huduma hii ya chakula.

Wale wa Vitongoji hivi sasa hawana chakula wagonjwa ambalo ni tatizo kubwa. Kumbe hii bajeti yao munawabana sana.

Mhe. Spika, bajeti ya mafuta ni tatizo. Juzi nilimpeleka mzazi wangu hapo hospitali ya Mwembeladu, kufika ninaambiwa mzee ngoja kwanza, ikiwa nini tuta-*refer* huyu atahitajika apelekwe Hospitali ya Mnazi Mmoja, unazo shilingi elfu kumi. Ninaulizwa shilingi elfu kumi, nikauliza ni za nini, za *taxi*. Ni tatizo Mhe. Spika, mafuta haya, hii bajeti ya mafuta inakuwaje kwa sababu hivi sasa ukenda hospitali ya Mwembeladu na mzazi ikiwa hutasubiri azae

kabisa yule, ina maana uende na shilingi elfu kumi za kukodia *taxi* kutoka pale Mwembeladu mpaka Hospitali ya Mnazi Mmoja. Mhe. Spika, mambo haya mpaka lini jamani.

Mhe. Spika, nimalizie sasa hivi nimepata ki-*memo* kutoka Mkoani, wanasema inakuwaje kuwaje katika ile Hospitali ya Abdalla Mzee kunakuwa *cost sharing* katika mambo ya wagonjwa wanaokwenda kupima *typhoid*, wanafanya *three thousands T-shillings.* Wanafanya wanafanya *cost sharing*. Lakini hawapewi risiti. Mhe. Spika, kwanza wizara inajua hilo kuna *cost sharing* ya *typhoid* pale. Kama inajua hizo fedha za *cost sharing* zinakuja au ndio zinabakia pale pale au ndio zinaingia mifukoni mwa watu tu. (*Makofi*).

Baada ya hayo Mhe.Spika, kwa heshima kubwa na unyenyekevu wa hali ya juu, ninawaombeni sana Waheshimiwa Wawakilishi hii bajeti irudi kwa mtoto wangu pale, halafu ifanyiwe maboresho ndio iletwe tena tuipitishe, lakini kinyume na hivyo tuikataeni hii. Hawa hawatofanya kazi vizuri, haziwatoshi pesa. Tuirudishe Wizara ya Fedha hii. (*Makofi*).

Mhe. Spika, ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Ahsante sana. Nimkaribishe sasa Mhe. Hussein Ibrahim Makungu, baadae Mhe. Fatma Said Mbarouk na hatimaye Mhe.Mohamed Haji Khalid.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Mhe. Spika, ahsante sana. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kuwa sote tupo katika hali ya uzima na afya njema mchana huu wa leo.

Mhe. Spika, ninakushukuru pia kwa kunipa nafasi hii kuchangia hotuba ya Wizara ya Afya kuhusu makadirio ya matumizi na mapato kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Pia nimpongeze Mhe. Waziri kwa kazi yake aliyoifanya kutokana na changamoto nyingi anazopambana nazo kwenye Wizara yetu hii ya Afya. Niwapongeze watendaji wote wa wizara hii kwa kazi yao na umakinini wao mkubwa.

Mhe. Spika, pia nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati hii Mhe. Mgeni Hassan Juma na wajumbe wake wote kwa hotuba yao nzuri sana na imefafanua mambo mengi sana katika ripoti yao.

Mhe. Spika, niendelee kwa kumshukuru sana Mhe. Waziri kwa kuliona hili la mafaniko kwa mwaka 2013/2014 katika kitabu chake kwenye ukurasa wa 3 kifungu nambari 3.

Kwa kuwaangalia hawa ndugu zetu kuweza kuwapatia posho maalum au *risk allowance*. Kwa kweli Mhe. Spika, suala hili ni kubwa na hawa watendaji wetu wanaumia sana kwa kuwahudumia wagonjwa, kwani wagonjwa wanakuja wengine hujui na maradhi gani, unaweza mgonjwa kaathirika lakini mtendaji naye akaathirika. Kwa hivyo wana-*risk* maisha yao kwa hali ya juu lakini posho lao kwa muda mrefu inakuwa hawalipati la *risk allowance*. Kwa hivyo Mhe. Waziri kwa kuliona hili ninakupongeza sana.

Ukitazama sio kwa mjini tu hata kwa vijijini posho hili kwa kweli wanakuwa hawalipati la *risk allowance*. Hivyo ninakushukuru sana Mhe. Waziri kwa hilo na ulisimamie kwa hawa watendaji wetu.

Mhe. Spika, mimi nitoe mfano, kuna siku moja aliumia mgonjwa kwa ajali, akafikishwa hospitali ya Al-Rahma ya pesa pale sio ya bure, ni mfano halisi. Lakini mgonjwa tangu asubuhi alipofika pale na mimi nilikuwepo, alikuwa ni mwananchi wangu wa jimbo langu, nilikuwepo pale na nikakukubali kulipa gharama zote za matibabu za hospitali ile ya Al-Rahma ili mgonjwa apate matibabu yake mazuri na iwe salama. Lakini jambo la kusikitisha Mhe. Spika, hakupata huduma yule mgonjwa mpaka mchana, jioni, usiku lakini mtaalamu wa mifupa ambao tunawahitaji sana hapa Zanzibar, mtaalamu yule hakuweza kupatikana kwa Al-Rahma pale mpaka kufika saa tatu usiku mgonjwa yule hajapata huduma yoyote ya miguu yake.

Nikaambiwa mtafute daktari huyu mpigie simu umuombe aje hapa Al-Rahma aje kumtizama mgonjwa wako. Kwa kweli nikafanya hivyo nikampigia simu bingwa yule na ninamshukuru *Doctor* Shaibu lakini alikuwa siye yeye, alikuwa ni *doctor* mwengine ambaye simjui lakini bingwa pia wa mifupa lakini jina lake nimelisahau ningempongeza sana *doctor* yule. Alikuja na akamtizama mgonjwa yule na kumuandikia dawa.

Kwa kushangaza hospitali kama ile ya Al-Rahma, hospitali ya pesa Mhe Spika, tunakwenda kulipa pesa nyingi lakini *specialist* amekufa hayupo hospitali. Hivyo ninamuomba Mhe. Waziri hili aliangalie kwa hospitali za kulipia pesa hizi, kazi yao na mafaniko yao katika kuwahudumia wagonjwa hawa kwa matibabu, ma-*specialists* hawa wawepo kwenye hospitali. Kweli Hospitali ya Mnazi Mmoja tuna mapungufu lakini wanasaidia kuja huku hospitali za binafsi ili kuja kufanya kazi zao.

Wanafanya kazi kule mchana, usiku wakihitajika huku wanakuja kuhudumia na huku kwa sababu Mhe. Spika, kwa kweli maslahi yao wahudumu hawa ni kidogo sana, na ukitizama kwa kweli daktari huyu kimataifa awahudumikie wagonjwa wanne mpaka sita kwa siku. Lakini kwa hapa Zanzibar anawahudumikia wagonjwa hawapungui 38 au zaidi kwa siku.

Mhe. Spika, sasa naomba hili suala liangaliwe vizuri na Mhe. Waziri hawa mabingwa wetu ni muhimu sana katika nchi yetu. Lakini niseme kuna wafanyakazi kwenye kitabu chako Mhe. Waziri 42 wapo masomoni katika fani mbali mbali, hasa madaktari 7 wanaosomea fani mbali mbali za udaktari kila aina ya ugonjwa. Lakini cha kusikitisha Mhe. Spika, hawa madaktari wakishakusoma wanakuja hapa Zanzibar lakini mafao yao madogo.

Mtu anafanya kazi pale Hospitali ya Mnazi Mmoja doctor mzima, lakini mshahara wake mdogo na kasoma miaka saba nje, hawezi kutumika pale kwa maslahi madogo. Hivyo daktari yule huwa anakwenda kuhangaika nje anafanya kazi zake, anakuwa na hospitali yake, inakuwa kwa kweli akili yake inachoka sana. Tuchukulie mfano mzee wetu *doctor* Ali Amour. Utakuta Hospitali ya Mnazi Mmoja anafanya kazi pale lakini ikifika mchana saa nane anakwenda hospitali yake kufanya kazi kwa kuingiza mapato zaidi ili kuweza kujikimu na maisha yake. Hivyo Mhe. Waziri naomba ma-*specialists* uwaangalie na uwalipe vizuri *otherwise* kila siku utasomesha wanafunzi na watakuja hapa na kuondoka na kwenda nchi za nje kwa ajili ya maslahi yao mazuri zaidi. Hivyo ninaomba tuangalie sana.

Mhe. Spika, pia nimpongeze *doctor* wetu huyu wa Al-Rahma, doctor Jamali kwa kweli anajitahidi sana na ana uwezo hata wa kuondoka kwenda nchi nyengine kufanya kazi kama Tanzania au sehemu nyengine, lakini kwa uzalendo wake aliwokuwa nao, *doctor* yule yupo na kwa kweli anatusaidia hata tukenda pale ushauri mzuri anatupa. Kwa hivyo ninampongeza sana huyu *doctor* Jamali kwa kujitolea.

Mhe. Spika, lakini wale madaktari wanaobakia hapa Zanzibar unakuwa mzigo mkubwa sana kwa wao. Kwa kweli wanatia huruma hawa ma-*doctors* wetu kwani akili yao wanatumia sana na wanachoka sana, saa nyengine anaweza kukuandikia dawa zilizokuwa hata sizo kwa magonjwa unayoumwa. Kwa hivyo naomba sana Mhe. Spika, tuangalie suala hili la hawa madaktari wetu ambao ni ma-*specialists* waweze kukaa na kufanya kazi.

Mhe. Spika, pia nimpongeze Mhe.Waziri kwa kununua hii mashine ya kuchomea taka. Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa muda mrefu ilikuwa haipo lakini sasa ninashukuru imefika na kwa ripoti ya kamati imeanza kazi. Kwa hivyo ninamshukuru sana.

Mhe. Spika, matatizo yapo mengi, sio mashine ile kupatikana ndio matatizo yamekwisha. Ninaweza kusema labda ni asilimia 10 tu ya matatizo ya mashine ya kuchomea taka, lakini vitendea kazi vingi hamna pale Hospitali ya Mnazi Mmoja. Wagonjwa wanafika pale na mimi mwenyewe nimeshashuhudia, hata ile tunayosema machera hamna ya kubebea mgonjwa pale. Unakwenda na mgonjwa wako kwenye *ambulance*, machera zipo mbili au tatu. Hivyo naomba Mhe. Spika, vifaa sio ghali sana. Naomba ujipange na ununue vifaa hivi vingi pale viwe vimekaa pale kwa ajili ya wagonjwa wetu wakifika pale waweze kuhudumiwa vizuri.

Mhe. Spika, haitoshi hayo, vifaa muhimu pia hamna kwenye Hospitali yetu ya Mnazi Mmoja. Vifaa vingi sana vya kufanyia uchunguzi hamna Hospitali ya Mnazi Mmoja. Ukitazama kifaa hiki ni muhimu sana kama *DNA machine*, hata jana Mhe. Mohammedraza Hassanali na Mhe. Jaku Hashim Ayoub walizungumza. Kifaa hiki Mhe. Spika, kweli kina gharama lakini sidhani kama serikali inashindwa kununua kifaa hiki, siamini hata siku moja. Tumeweza kununua meli na mambo chungu nzima kwenye nchi yetu, sidhani serikali ishindwe kununua kifaa hiki Serikali yetu ya Mapinduzi.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri ninakuomba sana suala hili la *DNA machine* ni muhimu na ni lazima tuwe nacho kifaa hiki kwa ajili ya maisha ya wananchi wetu na mambo mbali mbali. Nitoe mfano mdogo Mhe. Spika, kifaa hiki mimi nimekisoma vizuri umuhimu wake, mbali ya kuangalia mambo mengine lakini mambo muhimu sana ukitizama

mama mjamzito anaweza akaja pale kaambukizwa *VVU*, yule mtoto sasa hujui kama kapata yale maambukizo haya au hajapata. Kwa hivyo ile damu unaipeleka Tanzania Bara kwenye Hospitali ya Muhimbili ikatizamwe.

Mhe. Spika, utakuta inachukua muda mrefu, hata itoke kule ije huku hujui mtoto kaathirika au vipi. Kwa hivyo Mhe. Waziri hii mashine ni muhimu sana kwa uchunguzi ili kujua watoto wetu wamezaliwa salama au sio salama.

Mhe. Spika, nije kwenye suala la usafiri la wagonjwa la *ambulance* au usafiri wa kufika kama alivyosema Mhe. Mjumbe aliyepita kufikishwa mgonjwa kutoka hospitali hii kufika mjini. Kama mimi wagonjwa wangu kwanza huwa wanakwenda hospitali ya KMKM. Hospitali ya KMKM ninawashukuru sana, wakifika pale wanaandikiwa waende Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa matibabu zaidi kwa sababu pale vifaa vyao sio vingi sana vya uchunguzi.

Mhe. Spika, kutoka pale mpaka Hospitali ya Mnazi Mmoja inatumia gharama ya mafuta ya *ambulance*. Kweli jimbo letu tuna *ambulance* ya wananchi wa Jimbo la Bububu nimewanunulia. Lakini Mhe. Spika, kuna suala moja Mhe. Waziri wa Afya aangalie kama Jimbo la Bububu wanalo *ambulance* yao kwa wananchi wao, watoke na mgonjwa Kibweni mpaka hospitali ya Mnazi Mmoja unamueka pale bure. Lakini cha kusikitisha majimbo mengine pia wanatakiwa wajitahidi kupata vifaa hivyo vya usafiri, wanapata taabu kufika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Mjumbe kasema hapa unalipa shilingi elfu tano za *taxi*.

Sasa ilikuwa sisi Wabunge na Wawakilishi tujitahidi kwa majimbo yetu kuwanunulia wananchi vifaa kama hivi kuisaidia serikali mzigo wa kuwafikisha. Mimi ninaomba kila jimbo Mhe. Spika, iwe na *ambulance* yake kwa ajili ya wagonjwa wafike haraka sana hospitali. (*Makofi*)

Mhe. Spika, mimi niseme ninatoa mafuta kwa ajili ya *ambulance* ya jimbo langu lakini unakuta mafuta yanakua mengi, wagonjwa wengi kutoka Bububu mpaka Hospitali ya Mnazi Mmoja kweli ni gharama kubwa. Lakini kweli ninamshukuru mfanyabiashara mmoja maarufu sana, anasaidia kila mwezi shilingi hamsini elfu kwa ajili ya mafuta kwa ajili ya *ambulance* hili la jimbo la Bububu. Kwa hivyo ninamshukuru sana na wafanyabiashara wengine waone suala hili kuwa ni muhimu, wasaidie wagonjwa ili kuweza kufika hospitali kwa usafiri mzuri. Yaani wajitolee wasikae nyuma hasa kwenye sekta hii ya afya ni sekta muhimu sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika, inasikitisha huduma ya mama wajazito. Kwa kweli wajawazito wanapata taabu sana, mama zetu hawa wanapofika Hospitali ya Mnazi Mmoja kama alivyosema Mhe. Ismail Jussa Ladhu wanakaa chini, unakuta kuwa mazingira yao sio mazuri, ukenda usiku, alfajiri unakuta wamekaa pale na ukifika pale cha kusikitisha wanaambiwa wachangie. Mimi wananchi wangu wengi huwa wananiambia niwasaidia kuwachangia suala la matibabu ya pale.

Mhe. Spika, mimi sikatai Mhe. Waziri gharama ni kubwa. Nitoe mfano Dar es Salaam ukenda kujifungua hospitali za binafsi unaambiwa kwanza weka shilingi laki nane pale, ukenda hospitali ya *Regence* unaambiwa weka laki nane, ukijifungua kwa *pressure* ni milioni mbili gharama yake. Kwa kweli ninaishukuru serikali lakini Mhe. Spika, wananchi wetu ni maskini hasa Zanzibar.

Mtu umwambie utoe shilingi elfu thalathini hana, atahiyari afe pale lakini pesa hana. Kwa hivyo Mhe. Waziri uweke *special priority* kwa watu kama hawa, mtu aliyekuwa hana uwezo maskini basi achangiwe asaidiwe huduma ile aipate kwa haraka. Kwa sababu kama hujaipata huduma ile kwa muda unaotakiwa unaweza ukafariki.

Mhe. Spika, nasema mimi mwenyewe nimeshashuhudia mwananchi wangu kafariki kwenye *ambulance* kwa kuchelewa kufika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Kwa hivyo, ukifika kule huduma ile ipatikane kwa haraka na vizuri ili wananchi wale tuweze kuwanusuru maisha yao.

Mhe. Spika, nije kwenye serikali sasa. Serikali inajitahidi kujenga majengo mazuri, kwa mfano Hospitali za Wilaya. Kama kamati ilivyosema wameweza kujenga hospitali Mpendae, Kwamtipura, Chumbuni, Rahaleo, lakini vifaa vya kutumia hospitali hizo hamna, utakwenda katika hospitali kama hizi nilizozitaja hakuna *X-Ray machine*, hakuna *ultra sound*, sasa huyo daktari atakutibu vipi, anakupa dawa anabahatisha ugonjwa huo pengine hata wewe huna. Kwa hivyo, nilikuwa naiomba sana serikali bora tupunguze kujenga hayo majengo lakini tuwe na hospitali zenye vifaa vyote vya ukaguzi. Kwa sababu ukitizama Hospitali ya Mpendae gharama yake kubwa, Chumbuni gharama yake kubwa, Kwamtipura, tungenunua vifaa hivi kwa hospitali japo mbili tungepata *X-Ray machine* au *ultra sound*, tungekuwa tuko mbali na wananchi wetu tungeweza kuwafanyia kazi nzuri.

Mhe. Spika, nisikitike zaidi upande mmoja, siku moja nilikwenda Mnazi Mmoja kuangalia mgonjwa wangu nikapanda wodi ya juu ghorofa ya pili kule, kulikuwa kuna joto sana nikamwambia yule mgonjwa hapa si kuna feni hili, lakini lile feni linavyowaka linakwenda kidogo kidogo hujui kama limewekwa namba 5 au 1, yaani bora hata ulizime halina maana yoyote, akasema mafeni yote ni mabovu katika wodi ile.

Mhe. Waziri ninachouliza hii serikali inashindwa kutia hata feni katika Wodi ya wagonjwa? Mimi sidhani hicho kitu, utendaji tu unakuwa haujakaa sawa Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Mheshimiwa unazo dakika tano.

Hussein Ibrahim Makungu: Wagonjwa wanaumwa wanataka kupata upepo imekuwa bora wakae nje wapate upepo kuliko kukaa mle kwenye wodi yao. Kwa hiyo, naomba haya mafeni nimeona na Mhe. Waziri akayakague, apitie japo siku moja au mbili afanye ziara Hospitali ya Mnazi Mmoja, yeye na Mhe. Naibu Waziri watizame matatizo na changamoto hasa katika mambo haya.

Vile vile suala la chakula, wagonjwa hawapati chakula vizuri hata hiki cha mlo mmoja inasikitisha, bora tungesema chakula pia hamna. Kwa sababu mgonjwa masikini hana pesa mfukoni anategemea chakula cha hospitali hapati, sasa basi tuwaambie tu wagonjwa wetu kwamba bwana wee chakula uje nacho mwenyewe hapa. Kwa hiyo, na hili Mhe. Waziri pia aliangalie na apitie, kwa sababu akikaa ofisini anaambiwa tu hawezi kujua, najua Mhe. Waziri ni mtendaji atakwenda kuangalia na ataona hali halisi ya utendaji wa Hospitali ya Mnazi Mmoja ulivyo.

Mhe. Spika, najua tatizo la Wizara ya Afya kwa kweli ni gumu na hakuna vitu ghali kama madawa, lakini tuweze kufanya mambo mengine ya kutafuta fedha za kununulia vifaa, lakini fedha tutazipata wapi. Mimi natoa ushauri katika hii kodi ya petroli kipindi cha nyuma tuliambiwa ukinunua petroli uongeze shilingi mia au mia mbili za kodi ya Mfuko wa Barabara. Mimi naona sekta hii ni muhimu zaidi kuliko hata hiyo barabara tunayoitumia, mimi naomba tuongeze kodi hata kwenye mafuta tuweze kupata kukusanya fedha na kuweza kununua vifaa ili kuipunguzia mzigo serikali yetu.

Mhe. Spika, ukitizama katika sekta hii huduma ya afya inavunja moyo sana kusema kweli, hata hawa washirika wa maendeleo wanarudi nyuma sana kuona kwamba serikali mchango wake wa fedha ni mdogo. Kwa hivyo, hata wawekezaji au hawa wafadhili wetu wanaotusaidia kwa moyo safi na nia njema kwa ajili ya Zanzibar wanavunjika moyo na serikali iko nyuma kusaidia wananchi wake na sisi tusaidie pesa hizi. Kwanza sisi wenyewe serikali tutenge fedha halafu washirika wa maendeleo ndio watusaidie kwa kuona sisi tumejitahidi kukusanya fedha hizi. Kwa hivyo, nawaomba washirika wa maendeleo wasivunjike moyo na serikali ianze kutenga fedha kwa ajili ya kushirikiana na hawa wenzetu ili kuweza kununua vifaa mbali mbali viweze kusaidia.

Mhe. Spika, nitoe ushauri mmoja, kwa nini hawa wafanyakazi hasa wa serikali na wafanyakazi wetu sio wengi wasikatiwe bima ya afya. Kwa sababu ukikata bima ya afya ile bima ndio itamlipia yule mgonjwa gharama zake zote. Mimi juzi nilikwenda Al-Rahma nimeona kuna wafanyakazi wanakuja wa mahoteli ya kitalii wana bima ya afya, hawatakiwi hata kutoa pesa, unapewa kipande chako unasajiliwa ile bima inakulipia gharama zote za afya. Kwa hivyo, naiomba serikali pia kupitia wafanyakazi wake wote iwapatie bima ya afya ili waweze kuondokana na huu mzigo wa kupata matibabu kwa uwezo uliokuwa mzuri kabisa.

Mhe Spika, pia niseme kwamba, ukitizama kama unakwenda kukopa fedha benki sasa hivi unaulizwa unayo bima? kama bima huna unaulizwa umeweka nyumba yako uwe na bima. Sasa namuomba Mhe. Waziri ili waweze alisimamie hilo ili waweze kuondosha haya matatizo waliyokuwanayo ya matibabu kuwa hali zao duni na hawawezi kujilipia.

Mhe. Spika, mimi kwa hayo machache naunga mkono kwa asilimia mia moja bajeti hii, lakini naomba serikali iangalie kwa jicho la huruma na fedha ipunguze bajeti ya wizara nyengine iipe Wizara ya Afya kwa kuondoshea mzigo huu wananchi wetu waweze kupata huduma, kwani huduma hii ni muhimu. Mimi naunga mkono kwenye bajeti hii ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa fursa hii kuchangia Bajeti ya Wizara ya Afya. Pia nimshukuru Mhe. Waziri kwa kutuwasilishia bajeti hii.

Mhe. Spika, niseme kwa kuwa leo ni Ijumaa niwatakie waumini wote Ijumaa Karim na pia nianze kusema kwamba ni jukumu letu sisi humu ndani kusimamia bajeti, vile vile hili ni suala la kikatiba. Baada ya kazi hii jukumu jengine ambalo kapewa mwenzetu la kikatiba ni la Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Mashirika kuhakikisha kwamba fedha hizi za umma zinatumika kama zilivyoainishwa.

Mhe. Spika, ni ukweli usiopingika kwamba Wizara ya Afya ina majukumu mengi na makubwa sana, Sekta ya Afya kama nilivyosema kuwa ni muhimu kwa sababu ndio yenye dhamana ya kuhakikisha kuwa afya ya wananchi wa nchi hii zinakuwa bora na kuimarika siku hadi siku. Kwa hivyo, tafsiri ya bajeti kuwa ni utabiri wa matumizi unaokwenda sambamba na matarajio ya mapato katika mwaka wa fedha. Nakubaliana nayo tafsiri hii na maana nyengine ni dhana ya kusaidia mgawanyo wa rasilimali za serikali, lakini bado tafsiri hizi mbili kwa uelewa wangu mdogo zinanipa mashaka ni sawa na kuwa na ujauzito lakini hujui kwamba utazaa mtoto gani. Hali ya kutokuwa na uhakika wa kukipata hicho tulichokitarajia kukikusanya na kuanza kukitumia, kwa kweli ni tatizo la kutofanikiwa malengo unayojiwekea. Mimi naamini kwamba sekta yetu ni ndogo lakini kuna sekta nyengine ni lazima zipatiwe fedha za kutosha ili kutekeleza majukumu yake.

Mhe. Spika, katika kitabu hiki cha bajeti ukurasa wa 3 mpaka 5 tumeona mafanikio ambayo yamepatikana kwenye wizara hii. Moja ya mafanikio hayo ni kukamilisha kwa jengo la Ofisi ya Mradi Shirikishi wa Afya ya Mzazi na Mtoto iliyopo Kidongo Chekundu.

Mimi naona faraja kusikia kwamba tumepata mafanikio haya, afya ya uzazi na mtoto ni jambo muhimu mbali ya kukamilika kwa jengo hili, lakini ni lazima pawe na mkakati pale ambapo tokea mimba inapotunga mpaka kufikia kujifungua ili kupunguza vifo vya mama na mtoto na hasa vijijini ambako maisha ni duni.

Mhe. Spika, nikienda kwenye ukurasa wa tano wanasema kwamba mafanikio yaliyopatikana ni kuajiriwa kwa wafanyakazi wapya 840 wa kada mbali mbali kama vile madaktari, wauguzi, wasaidizi, wafamasia, madaktari wasaidizi wa meno, mafundi sanifu wa maabara na wengineo. Lakini ajira hizi zimekwenda kiupendeleo kwani kuna vijana wengi ambao walikuwepo pale lakini kwa sababu tu ya kukosa watu wa kuwatetea nafasi zimetoka nje ya pale na mpaka leo wako pale hawajapatiwa ajira. Hili nimuulize Mhe. Waziri si kuwavunja nguvu watu kama wale? Kwani ajira ni kwa vijana wote na hasa ukizingatia kwamba vijana wetu hawana kazi za kufanya, leo wako pale lakini ajira zimetoka wao hawakupatiwa na hata wale waliopatiwa zile ajira nimepata habari kwamba wengi wao wamekimbia. Kama tulivyosema kwamba lazima kuwe na uzalendo, vijana wetu wengine wanafanya kazi kwa moyo lakini tunawavunja moyo sana.

Mhe. Spika, ukurasa wa 10 kuna Kitengo cha Huduma za Macho. Nataka nipongeze kwa kuwa na kambi kubwa ya uchunguzi wa matibabu ya macho iliyofanyika kwa muda wa wiki mbili huko Pemba. Jumla ya watu 2,235 walipatiwa huduma hiyo, kati ya hao walifanyiwa upasuaji. Kwa kweli niwapongeze kitengo hiki cha huduma ya matibabu ya macho kwani bila ya jicho huwezi kufanikiwa, jicho ni kiungo kimoja ambacho Mwenyezi Mungu ametujaalia, kwa hivyo, ni lazima tupate matibabu haya.

Mhe. Spika, nikiendelea ukurasa wa 11 ambapo kuna hayo hayo ya kitengo cha matibabu ya macho kimesema kwamba, kwa upande wa watoto huduma za upasuaji macho zimefanyika kwa kushirikiana na daktari bingwa wa macho wa watoto kutoka Tanzania Bara. Kwa mwaka 2013/2014 ni watoto 8 waliopelekwa Tanzania Bara kati ya watoto 30. Hii ni idadi ndogo kwamba watoto 30 waliopatiwa ni watoto 8, kwa hivyo, hapa panahitaji jitihada ya ziada.

Mhe. Spika, katika kitabu hiki ukurasa wa 13 kuna Kitengo cha Kupambana na Maradhi yasiopewa kipaumbele. Mimi hapa najiuliza haya maradhi yasiopewa kipaumbele ni kwa sababu hayaumi au hayaui. Kwa sababu maradhi ni maradhi tu kwa hivyo, kama kuna maradhi ambayo hayajapewa kipaumbele mimi napata mashaka kwa nini yasipewe kipaumbele.

Vile vile nikiendelea kuna ukurasa wa 17 Kitengo cha Afya ya Wafanyakazi. Uchunguzi uliofanywa wafanyakazi waliobainika na kuathirika kiafya ni jumla ya 106 kati ya watu 8,108, kwa mujibu wa kitabu hiki ni kwamba wameshauriwa kwenda hospitali. Nataka nimuulize Mhe. Waziri kweli hili linatosha? Mimi nilidhani labda Mhe. Waziri atasema wamepata matibabu na hasa ukizingatia kwamba maradhi yenyewe ni hatari. Kwa sababu maradhi ya UKIMWI na maradhi mengine ya Sukari kwa kweli haya ni maradhi mabaya.

Ukurasa wa 18 kuna Kitengo cha Afya Bandarini. Mimi niseme huduma za afya bandarini na Uwanja wa Ndege ni muhimu, wale wageni nao wanaweza kutusambazia magonjwa mbali mbali na hasa maradhi ya kuambukiza. Niwashukuru wananchi kwa muamko wao wa kufanya mazoezi ili kutunza afya zao kwa haya maradhi yasioambukiza, waendelee kufanya hivyo kwani ni bora kukinga kuliko kutibu.

Mhe. Spika, ukurasa namba 34 Idara ya Sera, Mipango na Utafiti. Wizara hii ina miradi mingi kuanzia ukurasa wa 60 kuna Mradi wa Uimarishaji wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Mradi wa Kupandisha Hadhi ya Hospitali za Wilaya na Vijijini, Mradi wa kupandisha Hadhi Hospitali ya Mnazi Mmoja, Mradi wa Kusaidia Kupunguza Vifo vitokanavyo na uzazi na kadhalika. Pia niipongeze wizara na miradi mingi sijui tu kutokana na ufinyu wa bajeti kama kuna ufanisi wa miradi hiyo.

Mhe. Spika, katika changamoto nilizoziona zipo nyingi lakini moja ni kuongezeka kwa maradhi yasioambukiza, ambapo hili wizara ijitahidi kutoa elimu zaidi kwa wananchi namna ya kuweza kuepuka maradhi haya na ku-*balance diet.* Vile vile kuna changamoto za kukosekana kwa fedha hili serikali ijitahidi kwa kukata pua na kuunga wajihi kwa kuangalia vipaumbele.

Mhe. Spika, nitilie mkazo hii Bima ya Afya, lakini hii bima ya afya bila ya kuwa mfanyakazi huwezi kuwanayo. Sasa niulize hawa wengie ambao wengi wa wananchi watakuwa ni watu ambao hawana kazi, hawana ajira. Je, kwa upande wao tunahamasisha nini kwa wananchi huko nje, kwa aliyekuwa mfanyakazi atalipiwa au atakubali mwenyewe kukatwa mshahara kwamba ni lazima awe na bima hii na kwa sababu ni muhimu. Maradhi yanaweza kuja wakati wowote hayana mkubwa wala mdogo, kwa hivyo, ni lazima tuwe na bima hii ya afya.

Mhe. Spika, lakini kuna jambo jengine ambalo nimeliona. Jana ilikuwa ni siku ya usafi lakini nimeona Kikosi cha Polisi na hasa pale Wete Pemba ambako wamekwenda kusaidia usafi. Ni kweli bajeti zetu ni ndogo lakini kuna mambo hayaingii kabisa akilini kwamba tatizo hakuna fedha, nafikiri ni kujipanga. Kwa hili niseme kwamba Mhe. Waziri hata hawa wafanyakazi wa usafi hakuna walioajiriwa. Na kama kuna kundi kubwa la wafanyakazi pale ambao wanajitolea na mpaka leo hii hawajapatiwa ajira. Kwa hiyo niseme Mhe. Waziri hili nalo pia la kuwa na usafi nimeyaona mimi mwenyewe kwa macho magugu ambayo vikosi vyetu vimekwenda pale vimesafisha. Kuna mambo jamani hayataki nguvu kubwa ni wenyewe kujipanga.

Mhe. Spika, kwa kweli Wizara hii ina mambo mengi na mazito. Kwa sababu kama walivyokwisha kusema wenzangu madawa yanahitajika. Kuna mambo ambayo yatakuwa si ya msingi, ni lazima yale yaliyokuwa si ya msingi basi lazima tuwe na vile vipaumbele vya mambo gani ambayo tunayaona haya ni muhimu tuyafanye, na yale yaliyokuwa si muhimu basi tuyaache. Kwanza hii miradi ikiwa mingi, ni bora kuwa na miradi miwili mitatu lakini inatekelezeka, kuliko kuwa na miradi mingi lakini tunashindwa kuitekeleza.

Mhe. Spika, baada ya hayo kwa kuwa wenzangu wameshayazungumzia mengi na kwa bahati na Kamati yenyewe inayoshughulika na wanawake na watoto imesema meng, kwa hiyo mimi naunga mkono bajeti hii sisemi asilimia mia. Kwa sababu ni mtihani kila aliyesimama hapa kasema kwamba Wizara kwa kweli haipatiwi fedha za kutosha. Kwa hiyo sisemi mia kwa mia, nasema naunga mkono kwa zile asilimia ambazo zitakazopatikana maana yake sina uhakika wa hilo. Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi mchana huu kupata nafasi ya kufunga dimba katika kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Afya. Mhe. Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu nakupongeza wewe pamoja na Mhe. Waziri na timu yake kwa kazi nzuri waliyoandaa.

Mhe. Spika, nianze kidogo kwa masikitiko madogo tu. Wakati nakiangalia hiki kitabu kwenye yale yaliyomo niliangalia Hospitali ya Mnazi Mmoja iko wapi. Nikaona kuwa kwenye yaliyomo ipo ukurasa wa 32. Lakini kwenye ukurasa wa 32 nilikuta kuna mambo mengine mapya wala sio Hospitali ya Mnazi Mmoja. Hapa sijui kitabu changu mimi kilikatika vibaya au vyote vipo kama hivyo. Sasa ilibidi niitafute Mnazi Mmoja iko wapi, nikaona ipo ukurasa wa 24 badala ya 32 kama ilivyoandikwa katika kitabu hiki. Mhe. Spika, nikiangalia hapo lakini mengi yapo hivyo, pale ulipoambiwa jambo hili lipo, sipo lilipowekwa, kwa nini, sijui.

Mhe. Spika, nianze na Idara ya Kinga na Elimu ya Afya. Mhe. Spika, Wizara hii ya Afya ina majukumu kwa mtazamo wangu mimi mawili makubwa ya kukinga na kutibu. Lakini kukinga ni vyema zaidi kuliko kutibu, tutibu pale ambapo mambo ya kinga pengine yameshindikana.

Mhe. Spika, kwa mtazamo wangu hii elimu ya kinga kwa jamii kwa kima fulani kama imepungua kidogo. Kwa mfano, kulikuwa kuna maofisa fulani ambao walikuwa wanaitwa RHS sijui kama mpaka leo wapo wanakaa ofisini au vipi, lakini zamani kulikuwa kuna maafisa fulani ambao walikuwa wanatoa taaluma ya kinga kwa sababu sijui wanavyoitwa, hawa ilikuwa ni wadhamini wa kupita sehemu mbali mbali za kibiashara kuona namna biashara zinavyofanywa.

Mhe. Spika, leo ukipita masokoni na mwahala mwengine utawakuta wauza maandazi, wauza samaki wapo wazi, nzi na wengine nao wananunua. Wakati ambao kuna maradhi ambayo yanaambukizwa na vidudu hivi, lakini utamkuta mfanyabiashara ana karatasi yake anapepea nzi waondoke. Sijui hawa watu ambao wanahusika na utekelezaji wa mambo haya siku hizi wako wapi. Hawa watu ni haki yao kufanya biashara kwa sababu ni biashara halali iliyokubaliwa, lakini pia na Serikali ina wajibu wa kusimamia kutekeleza sheria za kiafya. Kwa sababu upo uwezekano katika hali hii kutokea maambukizo ya magonjwa mengine ya mripuko. Sijui Mhe. Waziri katika kipindi hiki wafanyakazi kama wale hawapo tena au wanabaki ofisini, au mambo yamebadilika.

Mhe. Spika, zamani hii elimu ya kinga ilikuwa inatolewa zaidi maskuli na katika vituo vya jamii. Na huko nyuma miongoni mwa magonjwa ambayo Serikali ilimudu kuyapiga vita na ikashinda moja wapo ni ugonjwa wa buba ambao wengi humu hata hilo jina hawalijui kama kulikuwa na ugonjwa unaitwa hivyo. Ugonjwa huu Serikali ilipambana nao na hatimae ukamalizika. Mimi nilikuwa darasani siku moja akaja Afisa wa Afya kutoa elimu katuandikia kwenye ubao sentensi kijipande kidogo sana kuhusu huu ugonjwa ambao umemalizika kabisa, na umemalizika kwa sababu watu wengi wa leo kamwe hawana habari kwamba kulikuwa na ugonjwa huo. Aliandika hivi *"It has been published for general information that treatment will be made for those who are suffering from yaws. This treatment will be provided by the doctors who will visit the villages from time to time. Headman and the relatives of those who are suffering from the disease must do everything in their power to perceive the sick to prevent themselves from inoculation. on the occasion when the doctor comes."*

Walikuwa wakitoa mambo kama haya maskuli kuonesha watu kuwa jamii, wanafunzi wengine waelimishwe ili daktari anapokwenda watu waende wakaonane na daktari kwa ajili ya kupatiwa chanjo za tiba. Nadhani niliambiwa hili darasa la sita miaka kadhaa iliyopita kabla wengine humu hawajazaliwa.

Mhe. Spika, sina hakika kwa tuliosema kuwa ni magonjwa yaliyokuwa hayakupata kupewa kipaumbele ambayo hiyo ni hatari. Kuna elimu gani ambayo Wizara hii kupitia hicho kitengo chake kinachukua kuhakikisha kuwa tunamaliza magonjwa aina hii ili yasitokee tena.

Mhe. Spika, magonjwa yasiyoambukiza hapa yapo mengi lakini nadhani katika kitabu hiki kwenye kusoma soma kwangu nimeona yametajwa kama kisukari, pengine na shinikizo la damu. Magonjwa haya katika visiwa hivi yamekuwa mengi mno hivi sasa. Wakati wa nyuma kuambiwa mtu kuwa ana sukari ilikuwa ni jambo la ajabu sana na watu waliona kuwa haya ni magonjwa ya wakubwa. Leo mtoto mchanga wa miaka 4, 5, 6 wapo wanaougua ugonjwa huu. Mhe. Spika, sijui sababu za ugonjwa huu kuwa mkubwa sana ama magonjwa haya kuongezeka kwa wingi katika visiwa vetu *source* yake ni nini. Hapo zamani ilionekana kuwa ni magonjwa ya watu maalum, leo kuwa ni magonjwa ya kila mtu takriban. Sisi tuliopo katika ukumbi sasa hivi si wengi ambao hawana japo moja katika ama presha au sukari. Sababu yake hasa ni nini?

Mhe. Spika, ni vyema Serikali kupitia Wizara hii ikafanya utafiti juu ya magonjwa haya na ikaweza kutoa elimu kwa watu kuweza angalau kupunguza kasi na ongezeko la magonjwa haya.

Mhe. Spika, nije kidogo katika Hospitali ya Mnazi Mmoja; Hospitali kubwa na Hospitali ya Rufaa. Mhe. Spika, hospitali hii ndio kubwa kuliko zote katika Zanzibar. Ningeomba Mhe. Waziri tuwaelimishe watu ambao katika maeneo yao, katika majimbo yao wakimbilie kutibiwa huko katika hospitali zao za karibu na pale waje wale watu ambao pengine ni jirani na ile hospitali ili kuipa hadhi na heshima ya kuwa ni ya rufaa, au waje watu wale ambao imeshindikana pengine kutibiwa huko kwengine na wale ambao katika maeneo yao hakuna hospitali au dispensari nyengine ndogo ndogo.

Mhe. Spika, cha kushangaza hospitali ile ambayo ni kubwa na ya rufaa tunaivamia, hata mtu ana matatizo madogo pengine anaweza akatoka anakotoka huko mbali, nje ya Mji Mkongwe anaumwa na kichwa tu anakimbilia Mnazi

Mmoja. Huku kavipita vituo kadhaa vya afya kakimbilia pale. Kwa hiyo ule msongamano uliopo pale unapunguza hadhi na utumishi bora wa hii hospitali.

Mhe. Spika, nisije nikafahamika kuwa nazuia watu wasiende pale, lakini twende pale kwa wale ambao hatuna vituo vilivyo karibu na sisi, wale ambao vituo vipo turipoti pale baada ya huko kushindikana.

Mhe. Spika, kulingana na ugumu wa kazi hizi za uuguzi ningemuomba Mhe. Waziri mara kwa mara awaase watu wanaowahudumia wagonjwa wazidi kuwa na lugha laini na nzuri. Ingawaje na sisi tunaokwenda kuhudumiwa mara nyengine tuna lugha ngumu na nzito kwani mara nyengine tunaanza sisi, mara nyengine huwa ni jibu la lugha tuliyopewa. Tuwakumbushe kuwa wakumbuke mafunzo ya *nurse* wa mwanzo *nightingale* wafuate maelekezo yake.

Mhe. Spika, siku moja nilikwenda katika hospitali yangu ya Mkoani kumpeleka mke wangu kwenda kufanya kipimo fulani, nikapeleka lile buku pale, muda mchache akaja mtu mwengine akapeleka, baadae yule mtu mwengine ameshaitwa mwanzo kaingia. Mimi nikafungua mlango nikasema mbona nimekuja mwanzo kuliko huyu na ameitwa huyu mwanzo. Yule kijana akanambia si kazi yako hii. Nikamwambia najua kwamba mimi hii si kazi yangu. Basi nakuomba toka, nikatoka kweli. Baadae akaitwa na mwengine mkubwa fulani lakini sikwambieni ni nani. Nikamwambia mbona mimi unanichelewesha hapa, akanambia yule ni mkubwa. Nikamwambia yule ni mkubwa kuliko mimi. Kwa vyoyote hata kwa umri mimi mkubwa, na kwa huku kama unavyofikiria wewe hata mimi mkubwa kuliko yule, lakini sikumwambia ni mkubwa gani, wala sikutaka ajue ukubwa wangu. Lakini bahati nzuri baada ya yule akahudumiwa wangu mimi.

Sasa yule ameshaondoka lakini mwenzake aliyekuwepo pale ndie aliyemuonesha kuwa na mimi ni mkubwa. Nikatoa kitambulisho changu nikamwambia na yule mwenzako kanitolea maneno, akanambia kama sikuridhika niende nikamshtaki. Nikamwambia mimi nikimshtaki yule huyo mkubwa wake mimi si msemaji wangu, huyo mkubwa wake wa hapa tu, msemaji wangu mimi yupo mbali zaidi nitamharibia huyu. Lakini nakuomba umwambie kumbe yule babu na yeye mkubwa. Na kabla sijaondoka alitoka akamueleza yule mwanamama akaja akasononeka. Nikamwambia mimi sifanyi chochote lakini kwa vile nimevaa kofia mbovu ukafanya ulivyotaka. Kwa hiyo tuwaelimishe wafuate mafunzo ya nightingale.

Mhe. Spika, naomba nimalizie kuwapongeza wananchi wa Mkoa wa Kusini Pemba kwa kuelimisha watu mama wajawazito kwenda kujifungulia hospitali. Mhe. Spika, Wilaya ya Chake Chake kwa mwaka huu ilipeleka watu 3,115. Hospitali ya Chake Chake sio Wilaya, ya Mkoani 2,064 na ya Vitongoji 229, kwa ujumla kinamama wajawazito Mkoa wa Kusini Pemba wapatao 5,408 walikwenda kujifungua hospitali. Mhe. Spika, hawa ni miongoni mwa wachache tu. Kwa sababu watu wa Mkoa huu wanafanya kazi nzuri sana, wengine wanajifungulia majumbani na hospitali ndogo ndogo kama Kengeja, Kiwani na Mkanyageni, hawa hawakuripotiwa humu. Lakini kama wangeripotiwa ni wengi zaidi. Kwa hiyo ningewaomba na wenzetu wengine muige mfano wa Mkoa wa Kusini Pemba jinsi tunavyowaelimisha na tunavyofanya kazi ya kuongeza *population* katika nchi hii.

Mhe. Spika, kwa kuwa muda umemalizika sikuombi uniongeze. Ahsante sana kwa machache niliyozungumza na mimi sijapata kupiga buti wala na huyu sitompiga buti. Nashukuru.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni. Tutaendelea jioni saa 11:00. Ahsanteni sana.

(*saa 6:00 mchana Baraza liliahirishwa hadi jioni saa 11:00*).

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea. Nafasi ya kwanza jioni hii naomba nimkaribishe Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, baadae. Haya tuanze na hayo.

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Mhe. Spika, ahsante sana. Bismillahi Rahman Rahim. Ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii nikiwa ni mchangiaji wa kwanza katika hotuba ya Wizara ya Afya kuhusu makadirio ya matumizi na mapato.

Kabla sijaanza kuchangia hotuba, kwanza Mhe. Spika, naomba nichukue fursa hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Ninampongeza kwa ujasiri wake, umahiri wake na hekma zake. Kwa sababu sasa hivi tumo katika mfumo wa Umoja wa Kitaifa. Mfumo huu ulianzishwa au ulipitishwa na Rais aliyepita Dkt. Aman Abeid Karume na yeye kapokea kijiti cha kuendeleza. Haikuwa rahisi wala si rahisi kuifanya kazi hiyo. Maana ni mfumo mpya na mfumo ambao unahitaji utekelezaji wa hali ya juu, serikali mpya yenye mawaziri kutoka pande mbali mbali za vyama vilivyokuwemo humu na bajeti tunaiona jinsi ilivyo. Kwa hivyo ninampongeza sana mpaka hapa alipofikia leo si rahisi kwa kiongozi mwengine yeyote kufikia *stage* hii.

Pia ninachukua fursa hiyo hiyo kumpongeza Rais aliyemaliza muda wake. Maana katika sekta ya afya alibahatika kuzawadiwa zawadi Dkt. Aman Abeid Karume. Zawadi ya kwanza alipewa ya malaria, zawadi ya pili alipewa na kile Chuo Kikuu cha Marekani ambacho kilimtunukia juu ya juhudi zake pamoja na matokeo mazuri kwa maradhi mbali mbali hapa Zanzibar, hususan ikiwa ni malaria ambayo imepigiwa mfano dunia nzima. (*Makofi*).

Tatu Mhe. Spika, naomba nimpongeze Waziri wa Afya pamoja na Naibu Waziri wake ambaye amekuwa akijibu maswali yote hapa ndani ya Baraza. Naomba niwapongeze watendaji na kusema kwamba hawa watendaji ni majasiri. Maana leo katika sekta ya afya na kufanya kazi na *figures* hizi au na idadi hizi za hesabu hususan kwenye bajeti ni kazi ngumu sana. Hawa watu Mhe. Spika, ni majasiri na wameweza kufanya kazi vizuri na kutokea matokeo mazuri sana.

Kutokana na michango mbali mbali ambayo imekuwa ikitolewa humu na Wajumbe mbali mbali, basi tumekuwa tukiwaoneshea vidole na hii itaendelea, na kwa nini itaendelea Mhe. Spika? Tutamlaumu Mhe.Waziri, yeye atasema fedha hazipatikana za kutosha, hazikuingizwa za kutosha. Ukichukua wastani wa bajeti yote nzima Mhe.Spika, utaona hawajafikia asilimia moja ya kile walichokiomba, wamepata kidogo zaidi, wapo kwenye wastani wa asilimia sitini mpaka sitini na tano.

Hata hivyo wameweza kufanya kazi kwa asilimia moja kutokana na juhudi zao. Tukimuangalia Waziri wa Fedha pia na yeye, tukimbana hapa na yeye atasema kwa hali ya uchumi hii ndio *ceiling* ya mwisho wanayoweza kupatiwa wizara hii.

Ninafikiri katika dunia nzima, tukichukua aghalabu bajeti za Wizara ya Afya ama sekta ya afya zinakuwa kwenye asilimia 15 mpaka 20 humo zinakwenda. Lakini serikali yetu kwa hali yake iliyokuwa nayo inafanya kazi kwa asilimia 3 mpaka 4 ya bajeti yote. Mimi ninawapongeza sana kwa matokeo haya, ni matokeo mazuri.

Mhe.Spika, jengine ninalotaka kusema, hapa yamezungumzwa mengi sana, yamezungumzwa upande wa utendaji, upande wa madaktari. Naomba nirejee tena kusema hawa ni mashujaa. Mhe. Rais hivi karibuni aliwatununia medali mashujaa wa nchi hii. Mimi nilibahatika Mhe. Spika, kupokea medali hiyo mmoja wapo. Nitaomba Mhe. Spika, nikuletee kupitia watendaji wa Baraza uione medali hii. (*Makofi*)

Hii sio kwangu mimi Mhe. Spika, lakini nimepokea kwa ajili ya mashujaa walio wengi. Naomba apewe Mhe. Spika. Wengi miongoni mwa waliopewa medali hii wametangulia mbele ya haki. Namuomba Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein mara ijayo kwa heshima na taadhima na kwa unyenyekevu mkubwa awatunukie nishani hawa waliokuwa hai. Hawa waliotunukiwa waliopita tunaita ni *the fallen heroes*, yaani ni mashujaa waliokwisha kutangulia. Safari hii ninamuomba Mhe. Rais aweke mfumo Mhe. Spika, kupitia kwako wa kuwapa hawa *the risen heroes* ambao wapo hai. (*Makofi*).

Maana ukitoa nishani kama hiyo ukimpa shujaa aliyekuwa hai basi na yeye anajisikia na nitaeleza kwa nini Mhe. Spika, naomba hivyo. Katika sekta ya afya wamekuwa wakifanya kazi ngumu kwa sababu ya ufinyu wa bajeti, wamekuwa wakifanya kazi ngumu sana katika madawa wanayopata na vifaa, wamekuwa wakifanya kazi kwa jitihada zao binafsi watu mwengine na marafiki na watu wanaojuana nao ili kwenda kuomba misaada sehemu mbali mbali. Yametajwa yote katika hotuba ya Mhe. Waziri kutokana na hizi *international organization* mbali mbali ambazo zinasaidia Zanzibar.(*Makofi*)

Mbali ya hivyo Mhe.Spika, hawa wana *qualifications*, ni watu wenye *high qualifications*. Leo hawa wamekaa hapa kufanya yote haya kwa sababu ya uzalendo wao. Sasa sisi tukianza kunyanyua vidole na kuwaoneshea vidole wanasafiri sana, wanakwenda nje sana, wanafanya ubadhirifu, wanakwenda kupeleka watu kutibiwa hospitali za nje kwa maslahi yao. Kwa kweli Mhe. Spika, hatuwatendei haki watu hawa.

Naomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe.Spika, atakapokuja hapo katika majumuisho, basi asafishe majina ya mashujaa hawa ambao wamejitolea kwa mshahara mdogo kutokana na elimu yao ambayo kwa kweli elimu yao wangeamua leo kwenda sehemu nyengine yoyote kufanya kazi, basi ninaamini wangepata mshahara kuliko humu Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanavyopata. Lakini wamejitolea kwa ajili ya nchi hii, wamekaa kwa kipato hicho hicho. Leo sisi tunathubutu kusema kwamba hawa wana maslahi binafsi na kadhalika.

Mhe. Spika, mimi nitaipinga bajeti hii kwa hali yoyote ile mpaka Waziri aje na ripoti maalum ama waraka maalum wa kusafisha majina yao. Aeleze Mhe. Waziri safari ngapi walizokwenda hawa, safari ngapi zimelipiwa na wafadhili au wahisani wa maendeleo, safari ngapi zimelipiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kila safari Mhe.Spika, waeleze tija ambazo zimepatikana katika safari hizo. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nilikuwa ninapitia magazeti haya ya Ikulu ambayo bahati nzuri humu ndani ya Baraza tunaletewa mengi sana na ni magazeti ambayo yanatupa habari, Ikulu yetu inafanya kazi vipi, Mhe. Rais anafanya kazi vipi na ni jambo jema sana.

Naomba sana nimpongeze Mhariri Mkuu Ndugu Hassan K. Hassan pamoja na Mhariri Msaidizi Sheikh Ali Hafidh pamoja na waandishi mbali mbali ambao wamo humu na mpiga picha wao na msanifu wao. Kwa kweli magazeti haya yamekuwa yakituhabarisha na miongoni mwa taarifa mbali mbali zimekuwa zikitolewa katika magazeti haya, moja wapo kubwa ni safari za Mhe.Rais.

Hapa kuna safari ambayo inaeleza ratiba yote ya Mhe. Rais za safari zake ambazo amekuwa akenda nje ya nchi. Safari nyingi amekuwa akifuatana na Waheshimiwa Mawaziri pamoja na watendaji. Nitachukua mfano mmoja tu. Safari ya India na sekta ya afya ilikuwemo na mikataba kadhaa imesainiwa huko. Nitamuomba sana Mhe. Waziri atakapokuja atueleze juu ya mikataba ile iliyosainiwa kule India, hospitali ambazo tunazitumia India.

Mhe. Spika, kuna hospitali ingawa hapa inasemekana kwamba wagonjwa wetu wanawa-*charge* zaidi kuliko wagonjwa wa *private*. Lakini kuna hospitali zinatudai mpaka leo na tumekuwa tukihama kutoka hospitali moja kwenda nyengine Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar; imekuwa ikihama kutoka hospitali moja kwenda nyengine kutokana na *bills*. Tunahama kwa sababu kule kwengine bado hatujalipa. Kwa hivyo Mhe.Spika, nitamuomba sana Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho ili bajeti yake ipite ayatolee maelezo haya na kuwasafisha majina vijana hawa.

Mhe. Spika, ninataka nikupe mfano wangu mimi mwenyewe binafsi ambapo mimi ni mmoja wapo wa mfano hai nilipopata matatizo ya mke wangu alipoumwa ghafla na kupata maradhi ya (*stroke*) kupooza. Basi mashujaa hawa wawili nitaomba niwataje ambao walishughulika usiku na mchana, kuanzia *emergency* kwa sababu mahitaji ya mwanzo kabisa mgonjwa anayohitaji ni yale ya hapo hapo, hawezi kusafirishwa moja kwa moja, haiwezekani.

Pia katika hali kama ile huwezi kumsafirisha kwa sababu hilo shirika la ndege nalo litakukatalia, huwezi kumsafirisha kwa hali yake yule mgonjwa alivyokuwa na mara nyingi inakuwa hawezi kusafiri kupanda *height* ama *attitude* ya juu kutokana na hali yake.

Mashujaa hawa wawili ni *Doctor* Mohammed Saleh Jidawi kwanza, na wa pili ni *Doctor* Jamala. Nilipofika pale hospitali nikawaomba huduma zao, hii Mnazi Mmoja mbovu, mbaya hiyo hiyo, inayoambiwa inanuka, ina vitu vichakavu na kadhalika, lakini hiyo hiyo iliweza kuokoa maisha ya mke wangu mimi Mahmoud Thabit Kombo. (*Makofi*).

Mhe. Spika, madaktari walipofika pale kutokana na hali hiyo hiyo basi huyu mmoja ni Katibu Mkuu Wizara ya Afya; Katibu Mkuu mzima, alivua shati, mimi nimemuona kwa macho yangu, akavaa lile gauni, akaweka ule Ukatibu Mkuu wake pembeni, akaweka makaratasi yake pembeni akamshughulikia na kumtibu moja kwa moja. Bahati mbaya dawa zikawa hazipo zile zinazotakiwa kwa maradhi yale ya *stroke*, kuna sindano ambazo unapigwa tumboni. (*Makofi*).

Mhe. Spika, ninamshukuru sana *Doctor* Jamala usiku huo huo tukafanya jitihada, maana sindano hizo zilikuwa zinatakiwa zipatikane ndani ya masaa 24, usiku huo huo tukapiga simu hospitali ya Hindu Mandal Dar es Salaam. Siku ya pili, dawa hizo zikaingia asubuhi na leo alhamdulillah tumeweza kuokoa maisha ya mke wangu. (*Makofi*).

Mhe. Spika, haya sio kama yamenitokezea mimi tu yamekuwa yakitokezea mara kadhaa, Katibu Mkuu, Mkurugenzi, Mwenyezi Mungu amrejeshee afya yake *Doctor* Malik wamekuwa wakitoka kwenye ofisi zao na kwenda moja kwa moja kuwahudumia wagonjwa. Kwa hali hii tuliyokuwa nayo, kwa mshahara huu wanaopata kwa *deficit* ya bajeti iliyokuwemo kwenye kitabu hiki, hawa kwa kweli ni mashujaa wa nchi hii, hatutakiwi leo kuwanyooshea vidole kwa kusema kwamba wanasafiri sana, wanafanya ubadhirifu wa mali ya umma, wana maslahi binafsi katika hizo hospitali na mengine mengi.

Nitamuomba sana Mhe. Waziri akifika hapa, kwa heshima na taadhima atoe ufafanuzi wa safari hizo walizokwenda katika mwaka huu uliopita na kila safari thamani yake. Fedha zile zimelipwa na nani pamoja na tija iliyotokana nayo safari hiyo. Kwa sababu ninavyoamini mimi katika hotuba ya Mhe. Waziri basi kila safari imezaa tija yake. (*Makofi*)

Mhe. Spika, matokeo kwa bajeti hii iliyokuwepo ndogo; hiyo hiyo ndogo basi matokeo ni mazuri hadi sasa. Idadi wanaotibiwa imekuwa nzuri, idadi ya vifo imepungua, idadi ya vifo kwa wazazi inaonekana kupungua, idadi ya vifo kwa watoto inaonekana kupungua. Tutakuwa hatuwatendei haki katika zama hizi tukiwafananisha enzi hizo za *Doctor* Kingwaba na Marehemu Mzee Thabit Kombo alipokuwa Waziri wa Afya na Ustawi pale. Hatuwatendei haki leo, kwa sababu wakati huo Mhe. Spika, fedha zilikuwepo Zanzibar. Karafuu ilikuwa dhahabu wakati huo, idadi ya watu ilikuwa ni ndogo katika nchi. (*Makofi*)

Mhe.Spika, leo hawa wana-*handle* idadi ya watu zaidi ya milioni moja kuwatibu. Hali ya fedha ndio hiyo. Nitamuomba sana Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban Waziri wa Ardhi na Nishati na mambo mengine yote yanayohusiana nayo, siku ikifika bajeti yake basi afanye haraka ya kuyachimba hayo mafuta angalau tupate pesa za kuwapa hawa watu kuweza kututumikia. Maana karafuu sasa hivi zimekuwa si dhahabu tena kama ilivyokuwa enzi hizo za akina *Doctor* Kingwaba waliokuwa wanatajwa hapa. (*Makofi*).

Mhe. Spika, kwa jitihada yao watendaji wa wizara hii pamoja na Waziri na Naibu Waziri wameweza kujenga majengo mbali mbali, ingawa wafadhili wengine wanakuja wanasema Misikiti na majengo yaliyojengwa miaka 10 au 20 iliyopita bado wanatajwa mpaka leo. Lakini hawa hawatajwi, wamefanya vitu *very recent*; vitu ambavyo vinaonekana wodi mpya zinazojengwa na kubwa zaidi leo kwa mara ya kwanza ninatumai itakuwa kwa mwaka itakuwa mwaka huu, vijana wetu wa Kizanzibari wata-*graduate* na *Doctor of Medicine* ama *MD Degree* hapa Zanzibar.

Hiyo yote inatokana na jitihada ya Rais aliyepita Mhe. Aman Abeid Karume kutokana na ziara yake aliyokwenda Cuba na Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein hakusita kuliendeleza jambo hilo ambapo leo, hawa vijana wata-*graduate* yeye Mhe. Rais akiwa Raia na katika wakati wake. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Una dakika 5.

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Ninayo mengi Mhe. Spika, lakini nitayafupisha.

Upande wa chanjo ya kolera naomba utolewe ufafanuzi kiasi gani tumetoa sisi kama Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kiasi gani kimetolewa na wafadhili wa maendeleo. Upande wa malaria napo pia naomba nipewe ufafanuzi huo huo.

Mhe. Spika, ningependa pia kupata ufafanuzi wa kiasi gani umetugharimu kumsomesha kila daktari na kiasi tumesaidiwa hizo *Universities* nyengine. Ninakumbuka *University* moja wapo ambayo inawasaidia hawa vijana wetu kuwa madaktari ili waweze kuongeza idadi ya madaktari hapa Zanzibar na Mwenyezi Mungu atawajaalia moyo wa uzalengo waweze kujitolea kama hawa wanaojitolea sasa hivi. Ninataka kujua kiasi gani SMZ imetoa na kiasi gani tumesaidiwa hivyo vyuo vikuu vyengine kama vile mfano kule Cuba.

Mhe. Spika, kuna mashirikiano ya vyuo vyengine mbali mbali duniani ambavyo yamekuwa yakifanyika, kama vile *Auckland University* ambayo imeelezwa hapa. Ningependa Mhe. Waziri angeweka jadweli, limo moja humu nimeliona ukurasa wa 78, hapana 81. Lakini imeekwa *in general*, kuna *DANIDA* wametajwa, *UNFPA*, na wanatoa fedha nyingi kwa kweli hawa.

Mimi ningeomba ipatikane jadweli ya mfadhili wa maendeleo ama mshirika wa maendeleo anatoa kiasi gani na kwenye mradi gani, na vipi tunafaidika kwenye mradi ule na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mchango wake upo kiasi gani ili haya mambo yapate kuonekana Mhe. Spika. Kwa sababu hawa tunapowashutumu au kuwalaumu au kuwaoneshea vidole, kuna mambo mengine yanakosekana humu. Ndio maana tunakuwa hatupati kujua.

Kuna mambo mengi, kuna ile *project hope* ambayo imetajwa katika ukurasa wa 81, kuna vituo hivi vidogo vidogo. Kwa hivyo Mhe. Spika, nitaomba sana haya yote yatajwe na tuweze kuyajua. Hao madaktari wetu wangapi jumla yake watakao-*graduate* na watapangiwa vituo gani na utendaji wao utaelekezwa wapi zaidi.

Mhe. Spika, lakini kwa kumalizia mimi katika Jimbo langu la Kiembe Samaki au jimbo letu; maana hili Baraza la Wawakilishi lipo katika Jimbo la Kiembe Samaki hapa, tuna vituo vitatu vya afya; Cha kwanza kabisa ni kituo cha Chukwani ambacho kinazalisha watoto saba wastani kwa siku. Ni kituo kikubwa kwa kweli, watu saba *new born babies seven a day* wanazalishwa pale Chukwani. Nitaomba nijue Mhe. Waziri kafanya ziara mara ngapi kwenye kituo muhimu kama kile ndani ya miaka hii ya Serikali yetu ya Umoja wa Kitaifa tokea achaguliwe yeye.

La pili ninamu-*offer* mimi kufanya ziara naye pamoja, kwa sababu nilibahatika kutembelea kituo hicho nikaona changamoto zilizokuwepo pale na wanafanya kazi nyingi za kujitolea. Kuna mama mmoja pale wa Kijerumani anajitolee sana, kwa sababu nimemuuliza mpaka mshahara wake, akaniambia mshahara wake anaopewa ndio hicho hicho kikia cha mbuzi, lakini wanajitolea zaidi, nitaomba nifanye ziara naye katika kituo hicho cha Chukwani. Nitamuomba pia anieleze ni mara ngapi kakitembelea kituo cha Afya cha Mbweni pale Matrekta. Vituo vyote hivi viko katika hii *PHCU*, kituo cha Matrekta pale ambacho kinahudumia watu wengi, wakishindwa huwa wana- *refer* kupeleka Mnazi Mmoja.

Kituo chengine kiko eneo la Kisima Mbaazi, njia ya kwenda uwanja wa ndege wa zamani. Kituo kile kiko katika hali mbaya mheshimiwa, naelewa kuna ufinyu wa bajeti lakini tunaweza kushirikiana na kusaidiana kwa mambo mengi, kwa sababu sote tuko kwa ajili ya uzalendo wa nchi yetu, tuko kwa ajili ya uzalendo wa kuendeleza sekta hii na tuko tayari kwa sababu wanaopata tiba pale wengi ni kutoka Jimbo la Kiembe Samaki. Lakini wako wengi pia wanaohudumiwa kutoka nje ya Jimbo la Kiembe Samaki.

Tutakapokuwa tumeshafanya hivyo, hatutokuwa kama wengine tukaja kusema humu kwamba yeye kafanya hiki na hiki, huo ni wajibu wetu. Inatia aibu sana na ningeomba sana serikali nzima Mhe. Spika, kupitia kwako wawe wakatae hii misaada mingine, maana tunakuja kudaiana humu na sio jambo zuri, ni aibu kwa serikali. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Mhe. Saleh Nassor Juma nimeipenda sana nukuu yake, ukiwadharau walipa kodi wa nchi ndio umedharau uchumi wa nchi, hiyo ni nukuu nzuri sana. Naweza kusema ni nukuu ya leo hiyo kubwa niliyoipata. Ukiwadharau walipakodi wa nchi ndio umedharau uchumi wa nchi nzima. Sasa leo walipa kodi wanalipa pesa zao, tukianza kuchukua pesa huku na huku tunanyooshewa vidole na ikinyooshewa serikali vidole ndio sisi sote, maana sisi ndio tunasimamia serikali. Mtu akijenga Msikiti inakuwa kila mwaka ni habari ya Msikiti huo huo unazungumziwa, sasa haya mambo yatakwenda mpaka lini.

Mhe. Spika, mimi naomba Mhe. Waziri atakapokuja atueleze hayo niliyoomba kuhusu safari mimi naona ziendelee kama zina tija, na naamini zina tija kwa sababu kila safari inakuja na matokeo yake. Hizi semina zina tija ziendelee.

Mhe. Spika: Muda umemalizika.

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Mhe. Spika, nitaomba sana Mhe. Waziri akija na mengine sijamaliza nitampa kwa maandishi, nitaomba majibu ya yote hayo ambayo nitaomba, la sivyo pataruka vumbi kidogo. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante sana naomba sasa nimkaribishe Mhe. Subeit Khamis Faki, afuate Mhe. Asha Abdu Haji, na hatimaye Mhe. Suleiman Hemed Khamis ajitayarishe.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kwa jioni hii ya leo kunipa fursa na mimi kuchangia kidogo katika hotuba hii ya bajeti ya Mhe. Waziri wa Afya.

Mhe. Spika, kwanza kabisa napenda nianze pale alipomalizia rafiki yangu Mhe. Mahmoud Thabiti Kombo, alipozungumza kwamba tusilinganishe wakati wa Dkt. Kingwaba na wakati huu, kwa sababu kipindi kile ilikuwa fedha za serikali zipo nyingi na sasa hivi fedha za serikali hatuna.

Ni kweli lakini kama nimemfahamu vizuri Mhe. Saleh Nassor, alikuwa anawatetea wale madaktari, alikuwa hawakandamizi ana watetea kwa kusema kwamba wao wana uwezo mkubwa wa kufanya kazi na nchi hii matatizo ya maradhi na ikabaki rehma ya Mwenyezi Mungu tu yakamaliza. Sasa yeye alikuwa ana watetea kwamba Wizara ya Fedha iwape fedha Wizara ya Afya ili waweze kupata dawa za kututibu. Ndivyo alivyonukuu Mhe. Saleh Nassor, kwa hivyo yeye alikuwa ana watetea na mimi bado nawatetea kwamba madaktari wetu wana uwezo wa kufanyakazi masaa 24, lakini fedha wanazopewa katika bajeti yao ni ndogo, hazitoshi. *(Makofi)*

Mhe. Saleh Nassor Juma alithubutu kusema kwamba anatushawishi wajumbe wote hapa kwamba tuzuwie bajeti hii ili irudi ikarekebishwe waongezewe fedha, hana nia ya kuwa tuzuwie bajeti ya serikali ili irudishwe. Ili ziongezwe fedha kwa sababu bajeti ya Wizara ya Afya ni wizara muhimu sana na ndio uti wa mgongo wa wananchi wote wa Zanzibar. Pia mimi nathubutu kusema kwamba bora irudi ili waongezewe fedha bajeti hii ili tuweze kutibiwa wananchi wa visiwa hivi na ni walipa kodi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mhe. Spika, madaktari wetu wanafanyakazi. Mhe. Mahmoud Thabiti Kombo, alisema kwamba Katibu Mkuu pamoja na wengine wanavua magwanda wakawatibu wananchi. Pia na sisi tunaye daktari kama huyo, Afisa Mdhamini wa hospitali yetu ya Pemba na yeye anavua magwanda akawasaidia watu. Kwa hivyo, na yeye tunamsifu kuwa anafanyakazi, anavua magwanda yake licha Uafisa Mdhamini wake akawasaidia wagonjwa wanapokuja na matatizo.

Kwa hivyo madaktari wetu wanafanyakazi, lakini sasa wawezeshwe na kuwezeshwa kwao ni kupewa fedha ambazo ni bajeti ambayo inakidhi haja ya kusaidia nchi yetu.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nataka nilizungumze. Nafikiri siku za nyuma tulikuwa tunapiga kelele karibu wawakilishi wa majimbo yote, kama vituo vyetu ya afya madaktari waliopo ni wachache hawatoshi. Hao wauguzi pamoja na wahudumu hawa wadogo wadogo wanaopelekwa sio madaktari bingwa. Tulikuwa tunapiga kelele kwamba hawatoshi, lakini kwa bahati nzuri wakatueleza kwamba kuna wanafunzi wanaosoma wakimaliza watagaiwa katika vituo vya afya ili kusaidia. Ni kweli waligaiwa na waliletwa, ingawa katika kipindi kilichopita waziri Babu Juma alituambia kwamba tuwasaidie majumba wale vijana ili wapate kukaa.

Mhe. Spika, lakini kulikuwa kuna tabia moja ambayo ilikuwa imeshajengeka, sio nzuri. Wanapangiwa madaktari kwenda kufanyakazi hasa vituo vya Pemba, lakini wakishapangiwa wakishakwenda madaktari hawa wanarudi wanakimbia, hawakai katika vile vituo wakafanyakazi. Sasa nilitaka aniambie Mhe.Waziri atakapokuja je, ni vijana wangapi ambao walipangiwa katika vile vituo wakakimbia wakarudi na kuja zao Unguja kwa sababu wamepangiwa Pemba.

Je, kama wamerudi walipewa adhabu gani ya kuonywa, kwa sababu wengine wasiendelee kufanya hivyo. Kama itakuwa hakuna basi pia atatueleza ni vizuri sana tupate kujua, lakini kama kuna waliokimbia wakarudi je, walipewa adhabu gani na ni wangapi.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nataka nilizungumze, kwanza napenda nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Afya, wizara yake pamoja na watendaji wake wale wakubwa kwa kuona kile kilio chetu tulichokuwa tukipiga kelele sana kuhusu Hospitali yetu ya Micheweni, kwamba wodi za kulaza wagonjwa hazitoshi. Namshukuru Mhe. Waziri kilio kile kama alikiona na sasa hivi wako wanaendeleza kutujengea zile wodi za kulaza wagonjwa na ile wodi ya wazazi *Alhamdulillah* tunashukuru.

Vile vile kuna maabara ya kuridhisha ipo, kwa sababu ni jengo zuri, basi na vile vifaa vya kufanyia kazi vya maabara viwepo. Namsisitiza Mhe. Waziri kama kuna upungufu wa vifaa, basi atupelekee ili ile maabara isiwe ni jengo zuri tu, lakini iweze kuanya kazi vizuri.

Jambo jengine ambalo nataka nimueleze Mhe. Waziri ajuwe kwamba Hospitali ile ya Micheweni haihudumii Wilaya ya Micheweni tu, inahudumia mpaka Wilaya ya Wete, kwa sababu kuna watu wanatoka Kiungoni, kuna watu wanatoka Pandani na sehemu mbali mbali, wote wanakuja kule Micheweni.

Kwa hivyo, namuomba Mhe.Waziri alitueleza kwamba atatuwekea *theatre* ambayo itakuwa wagonjwa wanapasuliwa pale pale Micheweni. Lakini *theatre* ilioko sasa hivi ni *theatre* ya kupasulia watu wa majibu tu, kama mtu ana jibu basi atakwenda kutibiwa, lakini ugonjwa mwengine wowote bado haijafanya kazi yoyote. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri watujengee *theatre* ambayo itakuwa inapunguza usumbufu kwa wagonjwa wa Micheweni, kuchukuliwa Micheweni na kupelekwa Wete au Mkoani, jamani ni mbali sana Wete na Mkoani.

Kwa sisi tuliopo Micheweni mgonjwa kama ni mzazi au kama ni mgonjwa kapindwa na mshipa wa ngiri mara moja, basi kumchukua Micheweni mpaka ukimpeleka Wete basi hiyo ni Rehema ya Mwenyezi Mungu, kwa sababu bado yule mja wake anataka abakie tu, lakini kwa kweli ni mbali sana.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri watujengee wanatujengea wodi ya wagonjwa kutuongezea, kwa hivyo na hiyo *theatre* watujengee kabisa katika kipindi hiki hiki, wamalize kabisa ng'ombe mzima, wasichukuwe mkia, wale ng'ombe mzima kabisa watumalizie. Kwa sababu wapo madaktari wanaoweza kidogo kupasua mishipa na mambo madogo madogo wanaweza kufanya, wanaweza kupasua hata mabusha. Mhe. Spika, kwa sababu bado *theatre* haijawekwa, basi namuomba sana Mhe. Waziri aone kama kuna haja ya hili suala nalo kutumalizia.

Jengine Mhe. Spika, ambalo nataka nizungumze kwa suala hilo hilo la Micheweni ni uzio. Mhe. Spika, ile hospitali wanalala wagonjwa na kwa bahati nzuri vijana wetu wengi, wengine wanakula unga, wengine wanavuta mabangi; ndio huo huo unga na wengine wana matatizo ya kila aina. Kwa hivyo, Mhe. Spika, siku moja atakapoingia pale mtu aliyepata ugonjwa wa kichaa wa wazimu basi atakuja kuwakimbiza wagonjwa wote waliomo mule, watakuja kutoka mbio mpaka watu ambao hawawezi.

Kwa hivyo, naomba sana tujengewe uzio, tena uzio wa kudumu. Kwa sababu mlituambia kwamba hospitali zetu mnataka kuzipandisha daraja ziwe za Wilaya na naona kwamba kuna mfano wa kupandishwa kweli daraja kuwa za Wilaya.

Kwa hivyo, haya matumaini yaliopo ni pamoja na huo uzio tujengewe, kwa sababu uzio uliopo sio, mtu akienda kuushika hivi anaweza akauangusha huko akaingia ni waya tu zile. Kwa hivyo, serikali ifanye jitihada ili tujengewe uzio ile hospitali yetu ya Micheweni iwe na uzio wa kudumu, sio ule wa waya wa kusukuma tu.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nataka kuzungumzia ni kitengo cha lishe. Mhe. Waziri ametueleza huku kuhusu kitengo hiki cha lishe jinsi wanavyotoa matone kwa watoto kwa ajili ya kuwakinga na hayo matatizo ya maradhi. Kitengo hiki kinafanyakazi vizuri, lakini kuna kitu kimoja ambacho kilikuwa kikifanywa, kuna watoto hawa ambao wana mtapia mlo.

Siku za nyuma kitengo hiki walikuwa wanatoa lishe, yaani walikuwa wanatoa unga wa lishe, sijui kama walikuwa ni wao madaktari au kulikuwa na taasisi ambayo ilikuwa ikisaidia, lakini hivi sasa kwa muda mkubwa suala lile limeondoka na wale watoto waliokuwa wakisaidiwa sasa hivi ule msaada haupo tena kwa muda mrefu. Sasa namuomba Mhe. Waziri atakapokuja anieleze je, tatizo hilo limeondoka kwa sababu ya huo upungufu wa fedha au kuna matatizo gani ambayo yanazuwia mpaka ikawa suala lile limeondoka.

Mhe. Spika, wizara hii sitaki nichangie mambo mengi, naomba Mhe. Waziri avione vituo vyetu vya afya vilivyoko Micheweni kama kilichoko Kiuyu na kilichoko Maziwa Ng'ombe, kwamba na hivi pia vinasaidia na kama unavyojua Micheweni ilivyo. Naomba atuangalie sana kwa jicho la huruma kule Micheweni kwa sababu kama unavyojua Micheweni ilivyo.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, naona sauti zinapaa zaidi kuliko sauti ya mjumbe anayechangia. Sasa tumuachie nafasi ili apate kuchangia na tumsikie vizuri. Mhe. Subeit Khamis Faki, endelea.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, baada ya machache hayo labda nizungumzie moja kwa kumalizia. Mhe. Spika, kuna kitengo hiki cha Chakula, Dawa na Vipodozi. Mhe. Spika, suala hili tumeshalizungumza sana na hata jana tuliliuliza kwenye maswali na leo hii nalitilia mkazo zaidi. Mhe. Spika, kitengo hiki ambacho kinachunguza basi kinatakiwa kifanye kazi kwa umakini sana, kwa sababu baada ya vituo hivyo ambavyo vinavyosajiliwa, dawa hizi za kienyeji zimetapakaa na ni nyingi zaidi na hizi dawa bado hazijafanyiwa vipimo tukaona kama je, zinastahiki

na hazina madhara kwa binadamu? Dawa hiyo moja utaambiwa inatibu magonjwa mia moja, maana utaambiwa dawa hii moja inatibu kila ugonjwa hiyo hiyo moja.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, nawaomba kitengo hiki kifanye kazi na nawauliza zaidi kuhusu hiki kitengo hiki cha dawa za asili. Je, kwa mwaka mmoja kinapita mara ngapi madukani kuchunguza hivi vyakula, kwa sababu watu wengi wanapata matatizo. Kuna matatizo yanajitokeza ya kila aina, kuna matatizo ya ugonjwa wa *stroke*, viungo vya miguu, watu watafunika miguu na halafu miguu inakosa nguvu. Kuna ugonjwa wa uziwi kila mara nasema, kuna ugonjwa watu wanakosa nuru za macho; hawaoni. Sasa sijui tunasababishiwa na vyakula au ni mabadiliko ya tabia nchi au ni matatizo gani.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri hebu mufanye utafiti ni matatizo gani, au ni mabadiliko ya tabia nchi ndio yanayotuuwa. Wafanye utafiti ili kujua matatizo haya yanayojitokeza hasa yanasababishwa na kitu gani na kama hawajafanya utafiti basi atueleze Mhe. Waziri ni lini wizara yake itajikita kufanya utafiti kwa maradhi haya madogo madogo ambayo sio ya kuambukiza ambayo yanajitokeza.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri wajipange ili kufanya utafiti tujuwe ni tatizo gani linalosababisha hivyo. Mhe. Spika, baada ya hayo machache, namuomba Mhe. Waziri akija atupe ufafanuzi. Lakini mimi naunga mkono hoja yake mia juu ya mia, pia nawaomba wenzangu kama kuna mpango wa kuwa tuirudishe basi tuirudishe ili iongezewe fedha. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante sana, naomba sasa nimkaribishe Mhe. Asha Abdu Haji, baadae Mhe. Suleiman Hemed Khamis na hatimae Mhe. Marina Joel Thomas ajitayarishe.

Mhe. Asha Abdu Haji: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi jioni hii kuchangia bajeti ya Wizara ya Afya. Mhe. Spika, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya njema jioni hii.

Mhe. Spika, namshukuru Mhe. Waziri kwa kuweka kitengo cha kupambana na maradhi yasiyoambukiza, kama vile kichocho na matende. Mhe. Waziri katueleza kwamba kipindi cha mwaka 2013/2014 jumla ya wananchi ambao wamechunguzwa na 1,902 na watu ambao wamegundulika ni 1,249, ambapo maradhi haya ya kichocho ni sawa na asilimia 65.7.

Mhe. Spika, kwa upande wa matende, watu 112 walichunguzwa na hakuna hata mmoja aliyegundulika na maradhi haya ya matende ni faraja kubwa. Lakini kwa upande wa kichocho ni asilimia kubwa ambayo imegundulika. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri afanye utafiti wa maradhi haya na pia atowe elimu wilayani, maskulini na hata majimboni katika maeneo ambayo yamegundulika na maradhi hayo.

Mhe. Spika, maradhi mengi ambayo yanapewa kipaumbele ni kama vile uziwi, kupooza miguu na hata kupopotoka miguu, kiuno na macho kutokuona. Kwa vile maradhi haya ni mengi, ningemuomba Mhe. Waziri afanye utafiti ili tujuwe maradhi haya yanasababishwa na nini au chakula ambacho tunakula. Kama alivyosema Mhe. Subeit Khamis kwamba chakula tunachokula, ni mabadiliko ya tabianchi ama ni sababu gani ambayo inatuletea maradhi haya ambayo yameenea sasa hivi katika nchi yetu.

Mhe. Spika, Hospitali ya Makunduchi ni Hospitali ya Wilaya; hospitali ile nawapongeza sana kwa huduma zao, lakini kuna tatizo moja la daktari wa *X-Ray* ambae ni mmoja tu. Hilo ni tatizo kwa sababu hospitali ile ni ya wilaya, kukitokea dharura daktari yule akiwa hayupo basi inakuwa ni tatizo. Mhe. Spika, ikitokezea kesi yoyote na daktari yule hayupo basi inabidi moja kwa moja mgonjwa yule asafirishwe na kupelekwa mjini, wakati mwengine mgonjwa yule hana uwezo, basi inabidi pale ulipie gari na kila kitu, mwananchi wakati mwengine inamshinda huduma ile.
Kwa hivyo, ningeiomba wizara ifanye kila jitihada kwa hospitali ile iweze kuweka madaktari wa *X-Ray* angalau wawili.

Mhe. Spika, naupongeza sana mradi wa mradi wa HIPS kwa Makunduchi umeleta manufaa sana na naupongeza sana mradi huo.

Mhe. Spika, naiomba Wizara iwapatie malipo ya *arias* zao za nyumba wafanyakazi hawa wa afya, nasema tena Wizara ya Afya ndio kinga yetu tunawafanyia kila kitu, kila jambo mtu akiugua lakini wafanyakazi wake mshahara wao ni mdogo, ningeiomba wizara ijitahidi sana itakapopandisha mishahara Wizara ya mwanzo ionekane Wizara ya

Afya kwa wahudumu maana yake hapa kila tukisema kwamba waongezewe mishahara tunataja madaktari. Ningeiomba kwamba madaktari na wahudumu, maodali na wafanyakazi wote waongezewe mishahara yao ni midogo tena midogo.

Mhe. Spika, naunga mkono bajeti hii mia kwa mia ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuweza kutoa mchango wangu kwa Waziri wa Afya ambaye nampongeza kwa kazi yake kubwa pamoja na watendaji wake wote.

Vile vile napenda nitoe mchango wangu wa Awali utakaohusika na homa ya mbu au homa ya dengue iliyoingia mara hii Mhe. Spika. Mbu huyu mara hii ameleta tafrani kubwa sana katika nchi ya Zanzibar kwa mara ya mwanzo watu kutafirika na kuwa na wasi wasi mkubwa na kwamba taarifa zilikuwa zinazungumzwa baina ya mtu na mtu au watu na watu, jambo ambalo pengine mtu hana *idea* nalo, hajui mwanzo wala mwisho lakini watu wanalizungumzia na lililomo mjini linazungumzwa. Kwa kweli hili lilileta wakati mgumu kwa watu wa Zanzibar.

Huyu mbu kwetu sisi ni mgeni, kwa mara ya kwanza kusikilikana pamoja na kuonekana umbo lake jipya lenye vidoa doa vyeupe ambaye ni tofauti na yule tuliyezoeya kumuona.

Mhe. Spika, mbu huyu anasababisha homa kali sana kama wale mbu wa kawaida lakini vile vile mbu huyu ana kawaida ya kumwaga virusi kwa wingi ambavyo vinaenezwa kwa nguvu zake alizonazo na katika aina ya mbu anayeitwa *aedes* hatujui kama ni neno la Kitaliana au Kiingereza au neno gani lakini hiyo ni aina ya mbu mwenyewe.

Kwa mujibu wa taarifa zilizomo humu ni kwamba watu walilazwa wengi hospitali ya Mnazi Mmoja kutoka maeneo mbali mbali, kwa mfano Mwerea walipatikana watu watatu, Kwamtipura mtu mmoja, Daraja Bovu mtu mmoja, Kama mtu mmoja, Dar es Salaam mtu mmoja na Fuoni mtu mmoja jumla ya wagonjwa waliolazwa hospitali ni wanane.

Baada ya uchunguzi mrefu na kuonekana aina gani ya homa ikagundulikana kwamba ni mtu mmoja tu ambaye ndiye aliyeathirika nae ni kutoka Daraja Bovu. Kwa hivyo watu wa Daraja Bovu Mhe. Spika, ndio ishara ambazo zimeonekana mbu huyu anakotoka na yalipopatikana maradhi hatujui kama mbu kweli alikuwepo au yeye mwenyewe amekuwa-*imported* maradhi haya kutoka sehemu nyengine Dar es Salaam maana watu wanasafiri kila siku.

Kwa hivyo naomba nimuulize Mhe. Waziri mbu huyo ambaye ameingia Zanzibar anatoka nchi gani? Tunataka tujue, je tiba yake mbu huyo ipo? Tena hiyo tiba yenyewe ni sahihi na ikiwa haipo gharama yake itakuwa kiasi gani na kwa hapa Zanzibar tuseme kama mbu hao wapo ni maeneo gani yanayoshukiwa kuwa yanaweza kuonekana mbu wa aina hiyo? Hayo ni masuala yangu ambayo nilitaka Mhe. Waziri atakapokuja hapa anieleze anakotoka, na gharama zake ikiwa dawa hazipo.

Mhe. Spika, baada ya hilo nataka nirukie sehemu nyengine kwenye jengo jipya la wagonjwa wa akili ambalo hii ni hospitali imejengwa pale Wete na inavyoonekana hao wagonjwa wa akili siku hadi siku idadi yao inaongezeka na sijui kama Wizara ya Afya imewahi kufanya utafiti wa aina yoyote kuona nini sababu za wagonjwa hao wa akili kuwa wengi katika nchi ya Zanzibar yaani Pemba na Unguja.

Kwa hivyo nataka nimpe suala langu dogo tu kumuuliza Mhe. Waziri je, kuna utafiti wowote uliofanywa kujua idadi ya wagonjwa wa akili waliopo Unguja na Pemba? Vile vile kuweza kujua idadi ya hawa maana hawa inasemakana wana kitu fulani wanachokitumia ndicho kinawasababisha kupata ugonjwa wa akili na kuna wengine wanakuwa wana maradhi ya wale watu wanaotumia madawa ya kulevya wanakuwa ni aina nyengine ya watu, lakini wote hao wanakutana huko huko mara nyengine na hupewa dawa ili waje katika hali nzuri.

Sasa nataka Mhe. Waziri kama kuna hesabu ipo aweze kunieleza kama utafiti umefanywa aina ya watu hawa wenye ugonjwa wa akili ambao wanavuta bangi, watu wa aina hiyo ni wangapi tuliokuwa nao Unguja na Pemba, ili tuweze kutofautisha baina ya wagonjwa hawa na wagonjwa wale wa dawa za kulevya.

Vile vile nataka kujua kutoka kwake hii hospitali iliyoko Wete kwa nini hospitali hii mpaka leo bado haijalaza wagonjwa wa akili kama vile hospitali iliyopo hapa Unguja, isipokuwa kwa kwenda kuchukua dawa tu? Sasa tunataka kujua kwa nini hospitali iko tayari labda kuna sababu za msingi na hatujazijua bado sababu gani kwamba watu hawa bado hawajalazwa.

Mhe. Spika, baada ya hilo sasa nataka niingie kwenye maradhi yasiyoambukiza; kwa hali ilivyo hapa Zanzibar sasa hivi masuala mazito ambayo yametukabili mbele yetu ni masuala haya ya maradhi ya kisukari na maradhi ya shindikizo la damu. Haya maradhi mawili ni mazito sana kwa Zanzibar, kwa kweli jamii kubwa iliyopo hapa sasa hivi inakabiliwa na matatizo haya mawili na maradhi haya Mhe. Spika, ni ya muda mrefu sana na kwa kweli siku hadi siku jamii ya Zanzibar inazidi kuengezeka kwa idadi ya wagonjwa hao waliyonayo.

Kwa hivyo Mhe. Spika, hili si suala la kupuzwa ni suala la msingi na suala muhimu sana kwa sababu jamii ndiyo inayopata matatizo; kwa kifupi tu kwa kipindi hiki cha karibuni kwa utafiti wa mara moja na uchunguzi wa mara moja Wizara imefanya jitihada kubwa sana za kuchukua watu aina mbali mbali na kuwafanyia uchunguzi na ikaonekana kwamba idadi ya watu 1,800 wana kisukari. Kwa hivyo idadi hii Mhe. Spika, pamoja na wagonjwa wa presha ni maradhi makubwa sana na idadi kubwa sana ya watu wa maradhi haya na lazima yapatikane ufumbuzi wake.

Wanasema kunusuru au kuhifadhi ni bora kuliko kutibu kwa sababu kutibu ni gharama kubwa sana, lakini kukiwa na njia ya kuweza kudhibiti baadhi ya mambo mengi na sisi hapa Unguja mara nyingi tunashindwa kudhibiti na matokeo yake tunaingia katika hasara ya kutafuta madawa na madawa ni ghali siku zote, kwa hivyo haya maafa mawili si ya leo wala sio ya jana ugonjwa wa kisukari na ugonjwa wa presha hapa Unguja kila mahala yameenea.

Kwa hivyo tunauliza Mhe. Waziri mpaka sasa hivi hatua nzito ni zipi zilizochukuliwa na nataka niseme kwamba maradhi haya katika mwili wa binadamu yanaleta uchovu mkubwa sana na siha yao inapotea kila wakati, sasa tegemeo la wagonjwa hawa wa kisukari na wagonjwa wa presha wanaitegemea Wizara kwamba itawasaidia, kwa sababu maradhi haya yanahitaji kitu hivi ni mahusiano makubwa baina ya yeye mgonjwa na hospitali yake na mgonjwa yeyote siku zote anategemea hospitali.

Kwa sababu maradhi haya tatizo lake na gharama yake ni kubwa sana sasa mara nyingi mgonjwa huwa anaitegemea hospitali kwa kuweza kumpa msaada kwa sababu yanahitaji fedha, na watu wetu wengi ni masikini na maradhi haya hayana matajiri tu mpaka hao masikini.

Kwa upande wa pili ukichunguza utakuta Wizara ya Afya inaonesha haina uwezo wa kukamilisha shida ya magonjwa haya kwani sekta pekee ya afya haiwezi kumudu mambo haya, ni ngumu. Sasa ikiwa Wizara inafikiria hapo kwamba kwa upande wake ina shida kuweza kuyakamilisha sawa sawa inaonekana pale ni matatizo kwa sababu hawawezi kuyamudu, basi nimuombe tu Mhe. Waziri ajaribu sasa kuzungumza kwa upana zaidi na kwa mashirikiano na wizara nyengine au Wizara ya fedha ili kufanya hiki kama ni kitengo maalum kiweze kupata fungu lake la kuweza kuwasaidia watu hawa. Bila ya kufanya hivyo watu wetu hawa tulionao ambao wenye maradhi ya kisukari na maradhi ya presha peke yao hawayawezi lakini na yeye Wizara apate fungu la kuweza kuwasaidia. Kwa hivyo nimuombe tu Mhe. Waziri katika jitihada zake aweze kuzungumza na Waziri wa Fedha, ili aweze kuwekewa kifungu chake maalum cha kuwasaidia wagonjwa aina hiyo.

Mhe. Spika, kidogo nina masuala ambayo nilitaka nimuulize Mhe. Waziri, baada ya kuwaunganisha hawa wagonjwa hawa wa kisukari au presha kutokana na shida zao kwa sasa hivi utaweza kuwasaidia kiasi gani ili kupunguza hilo tatizo? Kwa sababu gharama ni kubwa tunataka vile vile tudhibiti maradhi ili yasiongezeke. Kuna sababu zake za kufanya hivi kwani kila kitu kina sababu zake, ikiwa maradhi haya yapo lazima kutakuwa na sababu sasa je, hizi sababu ambazo hata yakatokezea maradhi haya watu wanazielewa? Ikiwa haya maradhi yanatokana na vyakula je, wameshaarifiwa ni aina gani ya vyakula watumie ambavyo ikiwa ni mgonjwa wa sukari takribani ni vyakula vyote asile kwa sababu hakuna chakula hakina sukari, ukila ugali una sukari, ukila wali una sukari, muhogo una sukari, ndizi ina sukari, chungwa lina sukari, embe ina sukari, *fruits* zote zina sukari, mbali hii tunayofanya na tunayokula *Artificial sugar* ambayo imetengenezwa kutoka katika miwa pia nayo ndiyo mbaya zaidi. Hii mimi nikitaka nimwambie Mhe. Waziri hebu jaribu kuzungumza na watu hizi soda zinatumaliza.

Mhe. Spika, ukichukua soda ya *coca cola* kama utaipeleka kwenye kiwanda basi robo yake ni sukari tupu mbali ya sukari yake ya vijiko viwili vya asubuhi, vijiko viwili vya usiku, kiasi gani sukari anayotia katika mwili wake

ambayo ni *Artificial Sugar* na hii yote inafanywa na binaadam, mbali ya hii ya *Natural* ya matunda ndizi, embe, papai hiyo ni *Natural* ambayo kidogo ina tahafifu. Wanatakiwa wale kidogo kidogo lakini hii nyengine iliyokuwa haina *control*, na masoda yamejaa tele hapo mjini je, maradhi hayajaongezeka? Sasa hapa mimi ndio ninataka kumuuliza Mhe. Waziri hivi vyakula ambavyo nilivyovizungumza na inaonekana wagonjwa wa sukari wanaongezeka siku hadi siku je, jitihada gani zinafanywa ili kupunguza ugonjwa huu.

Mhe. Spika, hawa wagonjwa wa presha wapo nao vile vile sijui Mhe. Waziri kawsaidia kiasi gani hawa ambao wanahitaji kupata *balance diet* sio tena mtu apige ugali mtu wa pili haonekani, huo ugali wake chungu inafikia kama hivi. Ugali unatakiwa ukunje ngumi yako hiyo ndio kiwango cha ugali ule sio mbiwi siku ya pili hivi sukari tayari inaingia na wali hali kadhalika sio mbiu kubwa, kila kitu kidogo. Sisi kwa kawaida yetu tukila mpaka sahani igeuke upande wa pili ndio tuone mambo yatakuwa mazuri, kwa hivyo haya yote yanatuongezea sukari kwa wingi kwa hivyo hapana *balance diet.*

Pia halafu hatuna mazoezi wengi ya viungo. Je, hapa Wizara inachukua hatua gani kuwaambia watu mazoezi ya viungo lazima yapatikane kila siku kila wakati alfajiri mazoezi ya viuongo, na wakati wa kulala ukishaamka usiinuke moja kwa moja ukiwa juu ya kitanda kidogo ufanye mazoezi mikono na kila kitu hivi unyooshe viungo vyako kabla ya kuondoka, sio ukurupuke tu na uruke moja kwa moja wende zako ukakoge hapana, lazima ufanye zoezi la viungo. Kwa hivyo mazoezi pia ni muhimu sana.

Vile vile tuangalie kwenye sehemu ya *obesity* watu wanaambiwa vipi, tumbo linafika kule yeye mwenyewe yuko huko nyuma tumbo likiwa kubwa kila kitu tayari, sukari itakuwemo, presha itakuwemo na upigaji wa moyo utaongezeka vile vile. Kwa hivyo maradhi mengi yanatokana na sukari chanzo cha maradhi yetu ni sukari, kwa hivyo hii sukari tunaizungumza vipi Mhe. Waziri hii, sukari ni tamu na kila mtu anaitaka lakini *source* ya maradhi yetu ni sukari.

Kwa hivyo hapa watu wetu tunawasaidia vipi hasa hawa wenye *obesity* wakifanyiwa vipimo hapa kwenye ukanda tumbo liko kule kiwango kimepita anaambiwa baba nenda kafanye zoezi punguza uzito, uzito umekuwa mkubwa sasa, kwani ule uzuri wa mtu kuwa na tumbo kubwa, ndio unaondoka, hatutakiwi ku-*over load* bwana, tuweke *balance diet* tumbo liwe aste aste, lisiwe kubwa sana na soda tusinywe kwa wingi tupunguze.

Mhe. Spika, limebakia moja ambalo nataka nimwambie Mhe. Waziri matatizo haya ya ugonjwa wetu wa sukari pamoja na presha; tukiangalia haya yapo kila mahala mjini yapo na shamba yapo, lakini kwa uchunguzi na utafiti niliouwona kwamba hawa watu wanapata shida hospitali zetu zilizobakia ndogo ndogo haziwezi kukidhi haja au mahitaji ya wagonjwa wa sukari na presha kwa sababu dawa zao hazipo. Kwa hivyo je, Mhe. Waziri hapa tunawasaidia vipi watu wetu hawa?

Jengine Mhe. Spika, nataka nizungumzie juu ya ugonjwa wa saratani, serikali inajitahidi sana kufanya uchunguzi.

Mhe. Spika: Mheshimiwa muda wako umemalizika.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Ahsante dakika mbili tu namalizia. Serikali inajitahidi kufanya uchunguzi.

Mhe. Spika: Muda wako umemalizika na tunaambiwa sisi wenye matumbo tujitahadhari.(*Kicheko*)

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Spika, naunga mkono hoja ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uzima, naomba nitoe mchango mfupi kiasi ili kumsaidia Mhe. Waziri kwa lengo la kuboresha matumizi ya Wizara hii.

Mhe. Spika, niende kwenye uchambuzi wa bajeti ambao Mhe. Waziri ametueleza kwenye kitabu chake kwamba mwaka 2013/14 Wizara hii ilipangiwa kukusanya 924,000,000/= na hadi Machi, 2014 wamekusanya milioni 443.8 sawa na asilimia 48.

Mhe. Spika, kazi za kawaida Wizara hii walitengewa bilioni 21.32 ambapo *OC* ni bilioni 5.8 lakini hadi Machi, 2014 wamepata *OC* bilioni 1.5 sawa na asilimia 26 ya bajeti ya mwaka 2013/14. Na mishahara Wizara hii

tumeambiwa walitengewa bilioni 14.02 hadi Machi, 2014 wameingiziwa bilioni 13.5 sawa na asilimia 66.4. Sasa hoja yangu ya kwanza mishahara ambayo Wizara hii walitengewa ni bilioni 14 na hadi Machi, zimeingia 13.5 asilimia 96.4 wana kasoro ya 0.4 bilioni.

Sasa hoja yangu ya kwanza kwa muda ambao ulibakia wa miezi 3 kwa kuwa fedha hizi tayari zimetumika kwa asilimia 96.9 je, mishahara hii ilipatikana wapi, kama ilitoka kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina nani kaidhinisha na kwa utaratibu gani.

Tatizo jengine Mhe. Spika, kwamba hivyo kwa taratibu za kiutendaji unapopeleka *OC* asilimia 26 mbele ya Wizara husika, na kwa mujibu wa taratibu za utendaji hapa ni dhahiri kwamba haya ya *OC* hayakufikia ufanisi wa utendaji kazi. Kwa maana kwamba wafanyakazi wa Serikali wa Wizara ya Afya waliendelea kupewa mshahara kama ni stahiki yao ya msingi ambayo Wawakilishi hiyo hatuna tatizo nalo, lakini kwa asilimia 26 ya *OC* iliyopatikana *automatically* kwamba hapa kazi ya afya haikufanyika, sasa wanaojenga hoja kwamba hii bajeti irudi na irekebishwe tena kwa kweli wana hoja ya msingi kabisa.

Na mimi ni miongoni mwa watu ambao wanaounga mkono hii bajeti kwa kweli pamoja na *ceiling* iliyowekwa na Wizara ya Fedha, lakini wanaposema irudi kwa maana ya kwamba wakifanya *reallocation* ya vifungu vyengine, vifungu ambavyo havina umuhimu zaidi kuliko vifungu vya *OC* viende kwenye vifungu vya *OC* ili wafanyakazi wa Wizara ya Afya wafanye kazi kwa ufanisi, ili wananchi wa Zanzibar wapate maslahi yaliyokusudiwa.

Mhe. Spika, ukweli ulivyo SMZ walitwambia kwamba watachangia bejeti ya maendeleo bilioni 6.33 wastani wa milioni 527.5 kwa mwezi. Hadi Machi, 2014 wamechangia 1.77 asilimia 28 kwa wastani wa milioni 197 kwa mwezi. Maana yake kwa mwezi SMZ haikutoa Wizara ya Afya milioni 324. Sasa ufanisi ni dhahiri kwamba hapana na wale wanaosema kwamba Wizara ya Afya haitimizi malengo kwa msingi huo kwamba bajeti yao haifikii hata nusu ya bajeti ya iliyotengwa.

Zanzibar na sisi ambao tunashangaa ni kwamba Serikali Kuu; Wizara ya Fedha wanaotwambia kwamba uchumi umepanda mapato yameongezeka tunataka tuyaone kwenye vifungu vya Wizara mbali mbali kiuhalisia.

Sasa unapomwambia mwananchi kwamba uchumi umepanda mapato yameongezeka, lakini Wizara ya Elimu mfano wa Wizara ya Afya haifikii hata asilimia 30 ya matumizi yake ya maendeleo *automatically* hapo pahala hapana kitu ambacho kimepatikana. Ama uchumi ulipanda fedha hazikupelekwa, ama uchumi ulipanda lakini fedha watu wametumia kwa misingi ambayo siyo sahihi. Kwa hivyo Mhe. Spika, kuna kila sababu na hoja ya msingi kwamba bajeti hii irudi Wizara ya Afya chini ya Mhe. Waziri wakafanye *reallocation* ya hivi vifungu, ili tupate ufafanuzi wa matumizi sahihi kwa vifungu ambavyo vinawagusa watu.

Kwa mfano Mhe. Spika, Hospitali ya Mnazi Mmoja ambayo ndio hospitali kubwa ndio hospitali ya rufaa imetengewa bilioni 8.2 kwa mwaka huu lakini bilioni 6.6 ni mishahara ni bilioni 1.6 tu ndio *OC*. Asilimia 80 ya fungu la bilioni 8 ya Mnazi Mmoja ni mishahara ya wafanyakazi ambao Wawakilishi hii hatuhoji hatuna tatizo. Maana yake nini, maana yake Mnazi Mmoja wametengewa asilimia 20 ya *OC* ndio watu watibiwe kwa asilimia 20. Na nina hakika mwisho wa mwaka watapatiwa asilimia zaidi ya 45, 50. Maana yake nini, maana yake kwamba madaktari wataendelea kulipwa lakini mwananchi wa kawaida, mnyonge wa Mungu aliyeumwa hatopata huduma ya tiba kwa msingi huo.

Kwa hivyo Mhe. Spika Mhe. Waziri ninamuomba sana akubali kwamba hii bajeti wakae na Kamati ya Ustawi wa Jamii wafanye *reallocation* ya vifungu ili safari zile za nje, matumizi ya magari, mafuta na mambo mengine ili wazielekeze Mnazi Mmoja ili wananchi wanapotoka mashamba kama ni hospitali ya rufaa waweze kupata huduma ya matibabu katika msingi huo.

Si kwa maana kwamba Wawakilishi wanawachukia sana wafanyakazi, lakini mfanyakazi bila ya nyenzo hapana kazi. Na mfanyakazi si kama kwa maana kwamba apewe mshahara, mshahara ni haki ya msingi ya mfanyakazi, lakini ulimpa nini ili aweze kufikia hayo malengo ya kazi aliyotengewa?

Asilimia 20 ambayo imetengwa Mnazi Mmoja ni dhahiri kwamba Wazanzibari wataendelea kufa na ndio maana Mhe. Spika, Mhe. Waziri ukurasa wa 65 amekiri kwamba vifo vya wagonjwa waliolazwa Mnazi Mmoja vimeongezeka. Amekiri kwamba Wazanzibari waliolazwa Mnazi Mmoja ni 27,654 lakini watu 822 wamefariki, na

amekiri kwamba hili ni ongezeko la vifo Mnazi Mmoja. Kwa sababu nini, kwa sababu tayari wataalamu wapo lakini nyenzo za kufanyia kazi hapana. Kwa hivyo Wawakilishi wanapohoji kwamba serikali haielekezi nguvu kwa wananchi wake kiafya tuna hoja ya msingi lazima irudi, ili Kamati ya Ustawi wa Jamii wakae na Waziri wafanye *reallocation* ili wananchi wa Zanzibar wasiendelee kufa bila ya sababu ya msingi.

Mhe. Spika, mimi ninayo hoja, na nachambua kwamba vifo vya akina mama na watoto vimepungua sawa ninakubaliana na wewe Mhe. Waziri vimepungua, lakini nataka nimwambie Mhe. Waziri afanye utafiti miezi 4 mfululizo hivi sasa watoto wengine katika mahospitali yetu wanapata ulemavu, kwa mfano Mkoani pale kwa miezi 4 watoto waliozaliwa zaidi ya watoto 8 wamepata ulemavu, kwa nini? Kwa sababu huduma za afya pale zipo lakini wakunga ambao wanahudumia mama wale wajawazito kwa kweli ni wakunga ambao wametoka vyuoni *fresh from school* lakini hawana uzoefu wa kazi. Na ndio Maana unapowahoji wale akinamama wanaojifungua wanatwambia kwamba mimi nilipokosa nguvu badala ya kusaidiwa pole pole basi imetumiwa nguvu hatimaye mtoto ameumia.

Mnazi Mmoja pale kuna watoto zaidi ya 30 wamekwenda kwa sababu mabega yametoka, kwa nini? Kwa sababu mama kakosa nguvu mkunga aliyepo yeye tayari ana *degree* yake lakini hana busara ile ya wakunga wa jadi, kwa hivyo ametumia nguvu mtoto ameumia mikono, wengine vichwa vimepondeka.

Kwa hivyo lazima Mhe. Waziri utwambie ni lini sasa utawashirikisha wakunga wale wa jadi ili waweze kutoa mafunzo ya busara wakati wa kujifungua, ili watoto hawa wadogo wasipoteze viungo na hatimaye kufariki.

Mhe. Spika, hoja nyengine ambayo ninataka niseme yupo mama huyu naomba jina lake nisilitaje lakini Mhe. Waziri baadae nitakupa, mwezi wa Februari mwaka huu alienda hospitali ya Mnazi Mmoja akapiga *ultra sound* pale, akaambiwa kwamba mama huyu ana tatizo la mimba nje ya fuko.

Madaktari wakamshauri kwamba aende *operation* na kazi hiyo ikafanywa, baada ya *operation* daktari aliyekuwa anamuangalia akasema kwamba huduma ile ya *operation* ilikuwa haistahiki. Kwa hivyo alipasuliwa wakati *ultra sound* ilisema uongo. Mimba ile haiko nje ya fuko huku tayari akiwa amepasuliwa. Sasa Mhe. Waziri hivi Wawakilishi ndio wanahoji kwamba Mnazi Mmoja imepoteza nguvu, *ultra sound* imemwambia daktari kwamba huyu mama ana ujauzito nje ya fuko, mtaalamu wa upasuaji akampasua. Baada ya kuchunguzwa kwa kina mimba ile iko sahihi haiko nje ya fuko na hadi hii leo, yule mama amepata *operation* bila ya matarajio, kwa nini? kwa sababu *ultra sound machine* imetoa majibu ya uongo kwa daktari, hatimaye imefanya kosa vitu hivi ndivyo ambavyo Wawakilishi wanasema, kwamba hospitali ya Mnazi Mmoja, na ni kwa sababu ya nyenzo hakuna na fedha hakuna, hatimaye Wazanzibari wanapoteza maisha kwa sababu tu ya ukosefu wa *OC* na vifaa vya hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Spika, niende masuala mengine niseme kwamba maslahi ya wafanyakazi yanasimamiwa kwa upana wake na nimpongeze sana Mhe. Rais kuongeza maslahi ya wafanyakazi, lakini nimwambie Mhe. Waziri kwamba bado Wizara yako inaonesha Idara ya Utumishi na Uendeshaji kuna upendeleo wa maslahi.

Mtakumbuka Baraza hili Mhe. Spika, Kamati yangu ya Ustawi wa Jamii iliyopita ilitetea maslahi ya Mkurugenzi mmoja, na wewe Mhe. Waziri ukaahidi kwamba suala hilo utalifuatilia na ulifuatilia. Taarifa ambazo tunazo mpaka Katibu Mkuu Kiongozi aliagiza kwamba yule mama apewe haki yake, kwa bahati mbaya Wizara yako imekataa kumpa haki yake. Kwa hivyo mfanyakazi ambaye anadai miaka 17 nyuma hakupewa haki yake, mfanyakazi ambaye anadai juzi kwa sababu ni familia ya mkubwa tayari mumemlipa. Huyu wa zamani miaka 20 pesa hamna, huyu wa juzi kwa sababu ni familia ya mkubwa mumemlipa haki yake.

Mhe. Waziri lazima utwambie lini utamlipa haki yake huyu mama, na tukisema hivi muache kutumia siasa. Huyu mama amekopesha taaluma yake miaka 17 nyuma, mkakiri mbele ya Kamati mtamlipa, serikali ikaji-*commit* mkasema mtalimlipa, mmeacha kumlipa, lakini mfanyakazi mwengine ambaye yuko ndani ya Wizara hii hii kwa sababu tu ni sehemu ya bosi mumemlipa pesa zake zote, ni upendeleo ambao sisi Wawakilishi hatukubali, lazima leo utueleze lini pesa zake tutamlipa. Na mimi kwa kutumia kanuni ya Baraza la Wawakilishi hapa natoa shilingi ya mshahara wako ili nihakikishe kwamba pesa za huyu mama zinalipwa katika mwezi huu.

Ninawaomba Wawakilishi wenzangu mnielewe kwamba huyu mama anaidai Wizara hii miaka 17 nyuma pesa haikupatikana lakini anayedai juzi pesa nyingi pesa zimepatikana. Ukichunguza kwa sababu yeye ni sehemu ya wakubwa. Mhe. Spika, ninazuia fungu katika mshahara wa Waziri ili nipate ufafanuzi haki ya huyu mama ipatikane.

Ni haki yake ya msingi ambayo mmeji-*commit* mbele ya Baraza, mkaji-*commit* mbele ya serikali kwamba mtamlipa lakini mmeshindwa kumlipa.

Mhe. Spika, nikitoka hapo sasa niende kwenye suala zima la wagonjwa nje ya nchi. Mhe. Spika, sisi hatukatazi watu kutibiwa nje ya nchi lakini tunayachunga matumizi ya fedha za umma.

Mhe. Spika: Mheshimiwa una dakika tano.

Mhe. Hija Hassan Hija: Na nimekiri kwamba serikali iliwatengea milioni mia tano (500,000,000) kwa matibabu ya nje lakini mmetumia bilioni mbili (2,000,000,000) kwa matibabu ya nje ya nchi, maana yake nini, maana yake kwamba wameongezeka, sasa mimi binafsi naomba mchanganuo, tuwajue Wazanzibari hawa waliokwenda nje ya nchi mkatumia bilioni mbili. Kwa hivyo, Wawakilishi na mimi binafsi naomba mchanganuo huo utwambie ni wagonjwa wangapi hawa waliokwenda nje ya nchi, kwa majina tuwajue, ndio hapo Wawakilishi watajenga hoja kwamba kweli Wazanzibari wanahudumiwa, lakini mkitwambia leo kwamba wamekwenda nje ya nchi wametumia bilioni mbili, kujua majina hayo tuweze kupata ufafanuzi.

Mhe. Waziri mimi nakuomba sana ulete mchanganuo nijue majina ya wagonjwa wetu ili tulinganishe matumizi ya bilioni mbili kwa wagonjwa ambao mmwapeleka kwa kipindi cha mwaka 2013/14.

Mhe. Spika, niseme tu kwamba mwaka jana Mhe. Spika, nakumbuka Baraza hili lilizungumzwa sana, habari za kitengo cha macho, na Mhe. Waziri ninakumbuka alikuwa mkaidi sana. Wawakilishi wanasema jengo bovu lakini Wizara inasema jengo ni zima, lakini nasikia walihama na wamehamia Kibweni. Kwa hivyo ni ushahidi dhahiri kwamba hoja za Wawakilishi zilikuwa sahihi kwamba jengo bovu, lakini kwa sababu mtu hataki kukubali ukweli anapinga tu. Sasa kama ni zima kwa nini mkahamia Kibweni. Kwa hivyo Wawakilishi wanavyozungumza hizi hoja zipimeni na muzitafakari vizuri.

Mhe. Spika, Wizara hii kwa kweli ina ufinyu wa bajeti lakini mengine hayahitaji bajeti, mengine yanahitaji moyo, busara na nidhamu ya watendaji wa serikali. Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi kwa ushauri wangu hatuwezi kuitengea Mnazi Mmoja hospitali ambayo ndio roho ya Wazanzibari bilioni 1.6 ya *OC*, nina hakika mwisho wa mwaka watapata hawa asilimia 40 mpaka 45.

Ushauri wangu Kamati ya Ustawi wa Jamii wakae na Waziri muangalie vifungu gani ambavyo vimenona havina umuhimu sana, mubadilishe mupeleke Mnazi Mmoja ili Wazanzibari wakitoka mashamba wanusuru maisha yao.

Baada ya hapo Mhe. Spika, siungi mkono hotuba hii mpaka Mhe. Waziri leo ataponambia lini yule mama pesa zake atalipwa, na kwa nini wakamwacha yule anayedai zamani, huyu anayedai karibu akalipwa pesa zake zote. Ahsante sana.

Mhe. Marina Joel Thomas: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Afya ya Mhe. Juma Duni Haji.

Mhe. Spika, kwanza ninampongeza Waziri kwa kazi nzuri ambayo ameifanya ya kutuletea hotuba hii pamoja na Katibu Mkuu, Wakurugenzi, na Watendaji wote na wafanyakazi wote wa Wizara ya Afya.

Mhe. Spika, mimi nitaanzia katika mradi wa kumaliza malaria. Kwanza pale napenda kuipongeza serikali kwa dhati kabisa kwa jitihada kubwa ambayo mmeifanya kwa kupunguza asilimia kubwa maradhi haya ya malaria kupitia mradi huu wa kumaliza malaria.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 53 wameeleza kwamba kuna jumla ya nyumba 51,546 katika Wilaya zote isipokuwa Wilaya ya Mjini zimefanikiwa kupigwa dawa. Hii ni hatua kubwa Mhe. Spika, kwa kufanya kazi hiyo ila tu ninaiomba isiridhike na matokeo hayo, izidi kutoa elimu ya afya ili kudhibiti vizuri maradhi haya.

Pia Mhe. Spika, mara nyingi miradi mbali mbali ambayo inafadhiliwa na wafadhili mbali mbali ikiwa imo katika ufadhili inakuwa endelevu na mizuri, lakini baada ya mfadhili kuondoka mara nyingi miradi yetu mingi inakuwa haiko endelevu. Mhe. Spika, hapa ni kuiomba tu Wizara ya Afya ijitahidi mradi huo ikifika muda wake wa kumaliza, wafadhili wakijiondoa ninaiomba Wizara ipange mikakati mizuri ili mradi huu uwe endelevu. Kwa

sababu tukisema wafadhali wakiondoka na sisi tuka-*relax* tukasema aa malaria hamna, kwa kweli itakuwa si vizuri na inaweza baadae pengine yakaibuka kwa kasi kabisa.

Kwa hivyo ninaiomba serikali wafadhali wakiondoka katika kufadhili mradi huu Wizara ijipange iendeleze mradi huu ili kupunguza matatizo ya malaria ambayo yanasumbua sana wananchi wetu.

Mhe. Spika, nitakwenda katika vituo vilivyopandishwa daraja ambapo katika ngazi ya Wilaya kuna vituo kama vinne ambavyo vimepandishwa daraja huko Mpendae, Kwamtipura, Rahaleo na Chumbuni.

Mhe. Spika, ni vizuri kupandishwa daraja vituo lakini tuangalie na vifaa ambavyo vilivyomo katika vituo vile vimetoshelezeka ili kupandisha daraja. Kwa sababu imeeleza kupandishwa daraja lakini kuna pia uhaba wa vitendea kazi, upungufu wa madawa. Kwa hiyo, nilikuwa naiomba wizara au serikali kwa jumla iviangalie vituo hivi ambavyo wanavipandisha daraja kuhakikisha kwamba madawa yanapatikana katika vituo hivyo, na vitendea kazi mbali mbali kama *machine* ziwe zinapatikana ili iwe na hadhi ile ya daraja ambayo imepandishwa.

Mhe. Spika, ukiangalia katika Kituo cha Rahaleo pale nje wakati wa mvua kituo kile kinatuama maji mengi sana, hivyo inaleta usumbufu hata kwa wale wagonjwa ambao wanakwenda katika kituo kile. Namuomba Mhe. Waziri aliangalie hilo.

Mhe. Spika, pia nitazungumza katika suala zima la maposho ya wafanyakazi, mimi nitazungumza kijumla jumla tu Mhe. Spika.

Mhe. Spika, wenzangu wamezungumza kuna malalamiko mengi tu kuhusu maposho ya wafanyakazi, pengine marekebisho ya mishahara. Hapa nilikuwa naiomba tu serikali iwaangalie wafanyakazi hao wa Wizara ya Afya wenye kudai maposho yao, wenye kudai marekebisho ya mishahara yao, wenye kudai stahiki zao basi iwapatie ili wapate moyo na ari ya kufanya kazi. Kwa sababu Mhe. Spika, kazi hii ya Wizara ya Afya ni kazi ya huduma, kazi inayotaka ujasiri, kazi inayotaka kujitoa. Kwa hiyo, kama hawa wafanyakazi wahatolipwa stahiki zao, hawatolipwa maposho yao, pengine kama kuna marekebisho ya mishahara hawajafanyiwa kwa kweli watakuwa wanavunjika moyo kufanya kazi zao kwa vizuri. Kwa hiyo, naiomba tu serikali iwaangalie wenye kudai stahiki zao wapatiwe, wenye kudai maposho yao wapatiwe ili wafanye kazi zao kwa ufanisi na kwa moyo wa dhati kabisa.

Mhe. Spika, wenzangu wamezungumza kuhusu uingizwaji wa fedha za bajeti. Kwa kweli wizara hii bajeti yake ni ndogo na mimi naomba niungane na wenzangu kuomba kwa serikali iweze kuwaongezea bajeti wizara hii. Kwa sababu wizara ina majukumu mengi na ni wizara ambayo inaangalia maisha ya watu na uhai wa watu. Kwa hiyo naiomba serikali iliangalie suala hili ili iongeze hii bajeti ili huduma mbali mbali ambazo zinazohitajika katika wizara hii ziweze kupatikana na kuweza kuwasaidia wananchi wetu na vijana wetu.

Mhe. Spika, nitazungumza katika Bodi ya Chakula na Vipodozi. Hapa kumeelezwa katika *page* ya 44 Bodi ya Chakula na Vipodozi imefanya ukaguzi katika sehemu mbali mbali na takwimu humu wamezionesha hapa. Wamekagua maduka, vyakula vya jumla, vyakula vya rejareja, mahoteli na mabucha. Lakini hapa nilikuwa naomba Mhe. Spika niiombe Bodi hii iwe na uaminifu zaidi, kwa sababu kuna wafanyabiashara wengi ni wajanja Mhe. Spika bidhaa zao wanabadilisha ile tarehe ya kubadilika muda wanaweka tarehe nyengine. Kwa hiyo, nawaomba wawe makini sana katika hili, na wakiwa makini katika hili ina maana wataweza kusaidia wananchi wetu kuepukana na maradhi mengine ambayo si ya ulazima, maana yako ambayo yanasababishwa na vyakula ambavyo vimepitwa na wakati na vipodozi mbali mbali ambavyo vimepitwa na wakati baadae vinaweza kuleta athari katika jamii yetu.

Mhe. Spika, nitakwenda katika haya maradhi mapya yaliyoingia ya *dengue*. Mhe. Spika, hapa niipongeze serikali kwa sababu maradhi haya yalipoingia tu imejitahidi kutoa elimu yake, na kubwa hapa nisisitize tu niiombe zaidi Wizara ya Afya izidi kuendelea kutoa elimu ya afya ili kuona haya maradhi hayatoweza kuendea zaidi, kwa sababu tukikaa kimya tukisema tusiendelee na kutoa elimu inawezekana ugonjwa huu ukazidi kuendelea. Kwa hiyo, naiomba wizara kupitia vitengo vyake mbali mbali vizidi kutoa elimu ya afya kwa jamii, ili wazidi kuelewa kwamba ni sababu gani, ni kinga gani ambazo zinaweza zikasaidia ili kuzuia maradhi haya yasienee kwa nguvu zaidi.

Mhe. Spika, la mwisho labda nizungumzie kiujumla kuhusu maradhi haya ya Ukimwi. Mhe. Spika, serikali imejitahidi katika hili kwa sababu ukiangalia miaka ya nyuma maradhi ya ukimwi ukimtajia mtu una ukimwi tu basi hapo hapo ameshakuwa anapata hofu. Mwanzo yalipoingia maradhi ya ukimwi hata yale matangazo yake yalikuwa

kidogo ya kutisha, maana yake unaweza ukaambiwa ukimwi unaua, kwa hiyo mtu akienda kupima ukimwi tu akiambiwa una virusi vya ukimwi basi ameshakufa zamani. Kwa hiyo, kwa kitengo hiki cha ukimwi kupitia Wizara ya Afya imejitahidi sana kutoa elimu ya afya, kwa sababu sasa hivi watu wengi wanaelewa ukimwi ni maradhi kama ya kawaida tu. Mtu anatembea, anapiga dozi zake hana wasi wasi wowote, tofauti na siku za nyuma ambapo elimu ya afya ilipotolewa ilikuwa kila mmoja ukimwambia ukimwi watu wanaogopana, lakini sasa hivi watu wanatembeleana, watu wanauguzana, watu wanapata elimu ya kutosha kabisa katika suala zima la maradhi ya Ukimwi.

Kwa hiyo, hapa naipongeza sana serikali kwa jitihada kubwa ambayo wameifanya, penye sifa lazima serikali tuipongeze na penye changamoto lazima tuiambie serikali. Kwa hiyo, naipongeza sana serikali kwa jitihada kubwa ambazo imechukua kwa kupitia Wizara hii ya Afya kwa kutoa elimu katika sehemu mbali mbali na hatimaye kupunguza maradhi mbali mbali ambayo yanasumbua wananchi wetu. Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, naunga mkono asilimia mia moja.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia makadirio na matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2014/2015.
Mhe. Spika, kwanza sina budi nimshukuru Waziri wa Afya kwa juhudi zake za kuishughulikia hospitali yetu kwa hali nzuri na ya kisasa. Nikiendelea pamoja na Naibu Waziri kwa mashirikiano yao mazuri kuendesha wizara hii kwa pamoja.

Mhe. Spika, nikichangia katika ukurasa Nam. 25 fungu Nam. 6 kuhusu Hospitali ya Mnazi Mmoja. Kwa kweli Mhe. Spika, Mnazi Mmoja anayeifahamu sasa lazima tuishukuru sana kimaendeleo, vifaa vingi ambavyo zamani vilikuwa hatuvioni sasa hivi vipo, madaktari wakuu wa sehemu hizo ni watu wenye sifa sana, kwa sababu wanatekeleza wajibu wao na wanajali sana wananchi wa nchi hii hasa wakiwa wanapokuwa wagonjwa wa hali mbaya kabisa.

Mhe. Spika, madaktari wakuu huwa mara nyingi wanajitolea wenyewe kwa fani zote ambazo wanazifahamu. Lakini penye sifa na matatizo yapo kwa kweli madaktari wa kati kati ambao wao sifa zao zimepungua sana kwa sababu ni wakali sana kwa wagonjwa. Hivyo utamkuta mgonjwa anasikitika kila wakati kuwa daktari anamuomba lakini anashindwa kumuhudumia. Isipokuwa haoni kwamba kiongozi wake mkuu anapita sehemu ile ndiyo huweza kumshughulikia mgonjwa wakati mwanzo alikuwa anamuona lakini hamshughulikii hadi apate amri kwa daktari mkuu. Hilo linatoa sifa ya Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Spika, upande wa madaktari wakuu nawapa sifa zote, lakini upande wa kati kati inabidi madaktari hao wajirekebishe hasa kusaidia wagonjwa wa hali ya chini. Mhe. Spika, hospitali yetu anaweza kutibiwa mtu labda yule anajulikana sana, kiongozi ama ana pesa zake nyingi ndiye anayeheshimika lakini wagonjwa wa hali ya chini wananyanyasika sana. Ukienda hospitali utasikia hasa mgonjwa anasema mimi nitafika hata kwa Mhe. Duni mwenyewe nimueleze jinsi mnavyotunyanyasa.

Mhe. Spika, hayo mimi nimeyakuta kwa jicho langu kuhusu kumuona daktrai anamnyanyasa mgonjwa hadi mimi nilimwita nikamwambia huyu mama unamuona mtu mzima, unamwita bibi, je sisi katika fani zetu tunamuheshimu sana bibi kuliko hata baba au mama. Kwa sababu huyu ndiye aliyemzaa baba au mama, usimnyanyase kutokana na uzee wake, muhudumie kama inavyopaswa kutokana na wadhifa wako ambao ulionao hapa kutibia wagonjwa. Mhe. Spika, hospitali yetu ni nzuri lakini inahitaji marekebisho ya madaktari wa sehemu za kati kati.

Mhe. Spika, nikitoka hapo nichangie ukurasa wa 45, fungu Nam. 12 kuhusu bodi ya ushiriki wa hospitali binafsi. Mhe. Spika, hivi sasa tunaelewa kwamba hospitali zetu hazitoshelezi kutibu wananchi ambao ni wengi sana hasa vijijini, na ndiyo sababu zikawekwa hospitali za binafsi katika vijiji vyetu na zipo hivi sasa zinahudumia. Lakini katika hospitali zetu za serikali utakuta mgonjwa anaumwa lakini anapata matibabu, na saa nyengine hospitali pale dawa hazipo anaambiwa kwamba aliyempeleka mgonjwa nenda mjini kanunue *drip* au kanunue sindano ya *tetanus* aje atibiwe mgonjwa.

Mhe. Spika, hilo ni suala gumu sana unapomuweka mgonjwa kwamba mtu aende mjini apande gari, gari lenyewe ni la kudandia akachukue dawa ya *tetanus* ama akachukue *drip* akija mgonjwa huyu kweli atakuwa bado yuko hai au amekufa. Mgonjwa huyu atakutwa katika hali mbaya zaidi kuliko vile alivyomkuta. Kwa hiyo, Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri ahakikishe kwamba anaruhusu vituo binafsi ambavyo hizi *pharmacy* ndogo ndogo kuuza madawa ziwepo karibu na hospitali zetu hasa za upande wa mashamba.

Mhe. Spika, tuna matatizo makubwa sana kwamba ndugu zetu ambao wana ujuzi wa kuuza madawa katika Mikoa yetu au katika majimbo yetu kukataliwa kuweka fani hizo ili kuwasaidia wananchi. Ndiyo utakuta katika hospitali zetu ambazo za mashamba, kwa kweli wagonjwa wengi wanateseka na inabidi wengine wanafariki kabisa kwa sababu hawapati wapi watanunua dawa za kuwasaidia wananchi.

Mhe. Spika, nikichukulia katika Jimbo langu la Koani zipo hospitali nyingi lakini *pharmacy* ndogo ndogo za kuuza madawa zinashindikana. Na utakuta sehemu nzuri kama sehemu ya Mwera kuna hospitali nzuri na kubwa ambazo ni za serikali lakini dawa kununua kwake ni shida. Unguja Ukuu katika jimbo langu kuna hospitali nzuri ya serikali, lakini utakuwa sehemu ya kuuzia madawa hapana, na madaktari ambao wana uwezo wa kuuza madawa ambao walikuwa ni wastaafu katika hospitali zetu na wanatajika wanakataliwa kupata nafasi ya kuuza madawa.

Utaambiwa kwamba daktari yule hana fani ya kuweza kuuza madawa, lakini alipokuwa serikalini alikuwa anaheshimika na anafika kuweza kufanya operesheni za watu mbali mbali. Lakini badala ya kutoka nje na kuwa mstaafu haheshimiki na anakataliwa kuweza kupata hatma ya ajira ndogo ndogo ambayo siyo fani yake aliyoizoea.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri akija anihakikishie kwamba anafungua *pharmacy* ndogo ndogo na kukubaliwa wananchi wetu kuuza madawa ili kuweza kusaidia wananchi wetu hasa katika majimbo yetu ya mashamba.

Mhe. Spika, niweze kuchangia ukurasa wa 55 kifungu Nam. 3 kuhusu kustawisha sifa za wananchi wa Zanzibar. Mhe. Spika, kuna matatizo makubwa sana ya wananchi wetu, kwani wanapata maradhi ambayo hayatibiki, na kwa sababu vifaa vingi vya kuwatibia wananchi wetu hapana, na sisi tunasema Zanzibar ni nchi. Sasa kama Zanzibar ni nchi kweli tutaweza kushindwa kuweza kuweka mashine muhimu za kutibu wananchi wetu. Mhe. Spika, utakuta wananchi wetu wa Zanzibar wanafariki kutokana na maradhi ya figo ambazo hivi sasa inatakiwa angalau *dialysis* moja hapa Zanzibar. Utashangaa kwamba nchi nzima hakuna *dialysis* ya kuweza kusaidia wananchi wetu kupunguza sumu katika figo.

Je, tutasema kweli hii nchi inasaidia wananchi, kwani utakuta hospitali ya Muhimbili chumba kimoja kuna *dialysis* 15. Vile vile katika hospitali za binafsi kama *TMJ* watu wote wa Zanzibar wanakwenda huko kuna *dialysis* 20 katika chumba kimoja. Mhe. Spika, iweje serikali yetu ishindwe kununua *dialysis*, hivyo akija Mhe. Waziri aniambie kwa nini Zanzibar imeshindwa kuweza kuwa na mashine ya *dialysis* ambayo ni muhimu sana kwa wagonjwa wa nchi hii.

Mhe. Spika, kwa kweli Mhe. Waziri kama fungu lake ni dogo atueleze ili aweze kuwa na fungu, ama aseme kwa nini anasababisha wananchi wa Zanzibar kufa bila ya hatia. Na kwa nini isiwekwe mashine ambayo ni muhimu sana kwa wananchi wetu ili kuhakikisha maisha yetu yanakuwa mbele, kila mwananchi hata akiumwa na figo anakwenda kwa mganga. Kwa vile anapoteza uwezo wa fedha zake na kusingizia kwamba yule mtu ameuliwa kutokana na kuumwa, kumbe vile hakupata vipimo vya kuweza kuhakikisha anaumwa nini. Mhe. Waziri akija anihakikishie kwa nini hakuna *dialysis* Zanzibar yote. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika, nikitoka hapo nichangie kifungu Nam. 55, fungu Nam. 3 kuhusu walinzi wa hospitali yetu ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Spika, hospitali ya Mnazi Mmoja hivi sasa kuna walinzi ni vizuri sana kuweka walinzi, lakini namshauri Mhe. Waziri aweke walinzi ambao wana fani yasije kutukuta wengi ambayo yalimkuta Mhe. Jaku ambaye alikuwa hana hatia, kumbe walinzi wale hawana ujuzi wa kuweza kuwa walinzi.

Mhe. Spika, hivi sasa kuna ulinzi wa *security* ambayo inalinda hospitali ya Mnazi Mmoja, kwa kweli kampuni hiyo haina uwezo wa kulinda wala haina fani ya kulinda, kwa sababu walinzi wake wote wanaokotwa mitaani na kuweza kulinda pale.

Mhe. Spika, usifikiri kwamba mtu amevaa kanzu na tasbihi kweli wote ni mashekhe, mtu akishavaa ile *uniform* anasema yeye ni askari lakini hajui kuzungumza lugha nzuri, ya kuweza kumridhisha mtu aliyekwenda kukagua wagonjwa, mara nyingi wanatumia nguvu na mabavu kwa kuwa wamevaa *uniform*.

Kwa kweli wale siyo walinzi, na namwambia Mhe. Waziri ahakikishe kampuni hii zaidi ya wiki moja iwe imejirekebisha ama iondoke kabisa katika hospitali ya Mnazi Mmoja, si hivyo sitotoa shilingi yangu kuichangia Wizara hii ambayo ni wizara nyeti ambayo tunaitegemea. Lakini kwa vile inaweka watu wazembe katika ulinzi pale

siyo sehemu ya kutembea hata mtu akienda hospitali basi anaenda pale kwa shida tupu, anapokwenda Forodhani kule anaenda kwa starehe, lakini anapokwenda hospitali uhakikishe mwenyewe anakotoka ameshachanganyikiwa, ikiwa yeye anaenda kukagua, ama ni mgonjwa mwenyewe. Mimi nataka Mhe. Waziri anihakikishie kampuni hii ina usajili kutoka wapi na ameipata wapi hata ikaweza kuwekwa pale na kuweza kulinda wagonjwa pamoja na wananchi wanaokwenda kuwakagua wangonjwa.

Mhe. Spika, nataka Mhe. Waziri anihakikishie kampuni hii ni ya mtu binafsi ama ni ya serikali. Mhe. Spika, kwa leo sitokuwa na mengi sana isipokuwa namuhakikishia Mhe. Waziri anapokuja hapa anihakikishie mafungu yote ambayo nimeyazungumza, nitaondoa shilingi yangu kama hatohakikisha kwamba mashamba katika hospitali kunahakikishwa ziko *pharmacy* za watu binafsi ambazo ndiyo tunazitegemea.

Kama Unguja Ukuu kuna Dk. Ramadhani ambaye ni mstaafu, anasaidia sana wananchi na tunamtegemea sana katika Jimbo la Koani, anaondoka anaweza kwenda hata India kwenda kupeleka wagonjwa, hivyo tunamtegemea sana, iweje leo anataka kufungua sehemu anakatazwa kwamba hana cheti cha fani ya kuweza kuweka *pharmacy* pale.

Mhe. Spika, huyu mtu ana uwezo na anafaa kwa sababu alikuwa polisi na ana vyeo vingi sana na vikubwa, alitegemewa kulihudumia Jeshi la Polisi kuhakikisha kwamba wagonjwa wote ambao alikuwa anahudumia hata operesheni iweje sasa amekuwa mstaafu asipewe fani ile ya kuweza kuendesha maisha yake au ajira yake ndogo ndogo.

Mhe. Spika, namwambia Mhe. Waziri anihakikishie mtu huyu tunamtegemea katika Jimbo la Koani, anaanzia Uzi Ng'ambwa hadi kufikia Bungi, Pete, Cheju, Unguja Ukuu Kaipwani, Kaebona, Tindini; tunamtegemea sana, hivyo ahakikishe kwamba amemruhusu kuweza kupata cheti cha kuweza kuweka hospitali yake binafsi kwa kuwasaidia wananchi.

Ahsante Mhe. Spika, nitaisaidia kama Mhe. Waziri atahakikisha kwamba masuala niliyompa ameyatatua. Ahsante sana.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Spika, kwa heshima kubwa nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara Afya, wizara ambayo ni muhimu sana katika maisha yetu.

Mhe. Spika, vile vile naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake wa hotuba hii. Na vile vile naomba nitumie nafasi hii kuwapongeza sana madaktari wote, wahudumu na wafanyakazi kwa namna ambavyo wanahangaika kusaidia kututibu wakati tunapoumwa.

Mhe. Spika, kwa kweli umuhimu wa wafanyakazi wa Wizara ya Afya au Sekta ya Afya huuoni mpaka pale unapoumwa. Naomba niipongeze wizara kwa namna inavyojitahidi sana kusomesha wataalamu wetu, hii lazima tuwapongeze kwa sababu ni kazi nzuri wanayoifanya, jambo ambalo linatusumbua ni kuwadhibiti madaktari wetu baada ya kurudi masomoni.

Mhe. Spika, taarifa niliyoipata ni kwamba madaktari zaidi ya 100 wa Kizanzibari wamesomeshwa na baada ya kurudi wameondoka Zanzibar katika vipindi tofauti. Mhe. Waziri tutizame madaktari hawa 100 wamehama wamehamia nje na wanatoa huduma huko wakati sisi wenyewe Wazanzibari tunaomba madaktari kutoka China au Cuba, kwa kweli hili ni tatizo kubwa. Kwa hivyo, naomba serikali itufahamishe imeshindwa nini kuwalipa hawa wataalamu wetu na kuwafanya hadi wadhalilike na kuhama katika nchi yao. Hili ni tatizo kubwa, serikali isipokuwa makini ikashughulikia maslahi ya wataalamu wetu basi tutasomesha vijana hata 1,000 lakini itakuwa ni sawa sawa na kuingiza maji katika pakacha. Naomba hapa serikali iwe makini sana.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu nije katika ukurasa wa 75, kiambatanisho Nam. 1. Kwanza nataka nitoe masikitiko yangu sana kwa namna kiambatanisho hiki muhimu kilivyokosa kufafanuliwa zaidi. Ni vizuri viambatanisho hivi vifafanuliwe ili wananchi na sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tupate kupima.

Mimi kidogo nimejaribu kufafanua, ingawa Mhe. Waziri ikiwa nitakosea atakaposimama atatufahamisha zaidi. Katika kiambatanisho hiki tumeambiwa wagonjwa waliolazwa Hospitali ya Kivunge ni 2,465; wagonjwa waliokufa

75 sawa na asilimia 3. Mhe. Waziri hapa hakutuwekea asilimia wala ile jumla ya wagonjwa na ingelikuwa ni rahisi sana kufahamu.

Vile vile wagonjwa waliolazwa katika Hospitali ya Chake Chake ni 7,514; wagonjwa waliokufa 138 sawa na asilimia 1.8 ambapo hapa kila wagonjwa 100 waliolazwa katika hospitali hiyo karibu wagonjwa wawili wamepoteza maisha.

Hospitali ya Mkoani wagonjwa waliolazwa ni 4,219; waliopoteza maisha ni 57, sawa na asilimia 1.3. Micheweni waliolazwa ni 2,831; waliopoteza maisha 39 ambapo ni sawa na asilimia 1.4. Makunduchi ni 1,998; waliopoteza maisha 12 ambapo ni sawa sawa na asilimia 0.6.

Mhe. Spika, kwa ufafanuzi huu naomba nipate maelezo ya Mhe. Waziri, ni nini sababu ya kutofautiana vifo vya wagonjwa baina ya hospitali na hospitali. Kwa mfano, kila wagonjwa 100 waliolazwa Kivunge wagonjwa 3 walipoteza maisha, lakini katika Hospitali ya Makunduchi kila wagonjwa 100 waliolazwa haifiki hata mgonjwa mmoja aliyepoteza maisha. Hospitali hizi zote ni *Cottage Hospitals,* nini siri ya tofauti hii ya idadi, namuomba Mhe. Waziri anifahamishe. Makunduchi kuna madaktari wazuri, kuna dawa nzuri au kuna vifaa vizuri? Namuomba Mhe. Waziri akisimama anifahamishe. Vile vile katika Hospitali ya Chake Chake kila wagonjwa 100 karibu wagonjwa wawili (2) wamekufa. Je, Mhe. Waziri ni sababu ipi wakati hospitali nyengine hali sio mbaya.

Pia hapa namuomba Mhe. Waziri anifahamishe kiwango cha Shirika la Afya Ulimwenguni, ni kiwango kilichowekwa cha wagonjwa wanaolazwa na kufa kiwango hicho ni kipi cha kupima mafanikio. Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja anifahamishe. *(Makofi)*

Vile vile kiambatanisho Nam. 2 nacho hakijawekwa katika ufafanuzi wa kutosha. Mimi mahesabu niliyoyafanya ni kwamba katika kila wazazi 1000 waliojifungua hospitali ya Chake Chake wazazi 4 wamepoteza maisha, lakini katika hospitali ya Vitongoji na Makunduchi hakuna hata mzazi mmoja aliyepoteza maisha. Hili ni jambo zuri na tunamuomba Mwenyezi Mungu kwa kweli atusaidie kila anayekwenda kujifungua pale atoke salama. Namuomba Mwenyezi Mungu awalaze mahala pema hawa wenzetu waliotangulia.

Mhe. Spika, hoja yangu hapa nini, sababu za takwimu hizi. Je, Wizara ya Afya imefanya utafiti? Iweje hospitali moja watu wanakufa wengi na hospitali nyengine hali inakuwa nzuri, namuomba Mhe. Waziri atueleze pana nini hasa kinachosababisha hivyo.

Mhe. Spika, katika kiambatanisho hiki cha 2 kuna jambo muhimu limekosekana kuhusu takwimu za watoto waliopoteza maisha wakati wa kuzaliwa. Hii nafikiri Mhe. Waziri angelitueleza, kwa sababu kilichoelezwa hapa ni wazazi wakati wa kujifungua waliopona na waliokufa, lakini vile vile na watoto huwa wako wanaozaliwa wakiwa hai na wengine huwa wanapoteza maisha. Kwa hiyo, hapa Mhe. Waziri sijui hana takwimu hii au wametuficha tu, ikiwa anayo namuomba atupe ili tuweze kupima kwa kulinganisha Shirika la Afya Ulimwenguni.

Mhe. Spika, naomba niende katika kiambatanisho Nam. 12 ukurasa wa 86. Hapa kuna kasma ya 601 Kinga Unguja, pia kuna kasma ya 901 Kinga Pemba. Mheshimiwa fedha zilizopatikana hapa ni asilimia 18, hii kwa kweli ni asilimia ndogo sana, namuomba Mhe. Waziri aukumbuke msemo wa Kiswahili unaosema kwamba "*kinga ni bora kuliko tiba*". Maana ya msemo huu hapa ni lazima tujipange kuwekeza katika kukinga tusisubiri gharama kubwa ya kujitibu. Hili ni jambo zuri na lazima Wizara ya Afya ilizingatie. Mara nyingi misemo ya wazazi wetu ni misemo yenye maana sana, kwa sababu gharama za tiba ni kubwa ukilinganisha na gharama za kinga.

Mhe. Spika, naomba nimalizie kuhusu Vituo vya Afya. Mara nyingi Mhe. Waziri au Naibu Waziri wanaposimama hutwambia kwamba vituo vya afya ni vingi na tusiendelee kujenga tena vituo hivyo. Kwa niaba ya wananchi wa vijiji vya Vikunguni namuomba nimwambie Mhe. Waziri kama wananchi wale wanapata shida sana, kwa sababu jiografia yake vijiji vile vimezungukwa na mabonde, hawezi mtu wa Vikunguni kwenda hospitali mpaka aende hospitali ya Gombani ambapo kuna mito, siku za mvua ni shida, na mimi binafsi nina kumbukumbu za watu wawili kupoteza maisha katika mito ile.

Vile vile ukiacha hapo lazima mtu aende Vitongoji ambako ni masafa makubwa, au akiacha Vitongoji aende Jeshini au hospitali ya Chake Chake. Barabara yetu ya Vikunguni kwenda Chake Chake Mhe Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano ajitayarishe aje atujibu. Hivi sasa kwa sababu kumepita mvua mgonjwa lazima apakiwe kwenye gari

ya ng'ombe, kwa kweli ni jambo la kutudhalilisha sana wanawake, mgonjwa hufika kuumwa na uchungu apakiwe kwenye gari ya ng'ombe wakati mwengine anajifungulia njiani. Hili ni tatizo, ingawa Mhe. Spika, nampongeza sana Mhe. Waziri pamoja na wizara yake kwa kuliona hili suala na wakaamua kupeleka *mobile clinic* katika kijiji cha Vikunguni, ambapo wajawazito na watoto huwa wanapata huduma ya kupima mwezi mara moja. Hili nampongeza.

Mhe. Spika, lakini tatizo lililopo hapo wanapopimiwa wajawazito wale ni sokoni, na itabidi nitumie Kiswahili cha Kipemba na Mhe. Mahmoud Thabit Kombo kasema anakijua sana Kiswahili cha Kipemba. Soko liko mbele hapa pana nyumba na huku kuna nyumba, ule uchochoro uliokuwepo mbele pamewekwa mlango wa kumba, humo ndimo wajawazito wanamopimiwa. Wengine wanaujua mlango wa kumba ni kuti lililosukwa ambalo mtu akipita akiamua kukutizama atakuona tu. Sasa hiyo ndio hali waliyonayo wananchi wa Vikunguni.

Mhe. Spika, wananchi hao kutokana na unyonge na umasikini wao pamoja na sisi ambao wametuchagua kuwasemea tumejitahidi kujenga jengo pale Vikunguni, lakini kwa kweli jengo lile tayari limeshaezekwa lakini bado matengenezo mengine. Sasa hapa naiomba serikali kwa jitihada ile na aibu wanayoipata wanawake watwambie watatusaidia nini wananchi wa Vikunguni ili wapate angalau kile chumba kimoja cha kufanyiwa vipimo wasifanyiwe nje.

Mhe. Spika, nafurahi sana kumuona Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kuwa yupo, kwa sababu atayasikia au atakisikia hiki kilio cha wananchi wa Vikunguni. Kwa kweli lile ni jambo la kusikitisha, na wananchi wa kule ni wanyonge sana, lakini wamejitahidi tukishirikiana pamoja mpaka ikafikia hatua ile. Sasa naiomba serikali pamoja na Wizara ya Afya angalau ijitahidi kuweka kile chumba wapate kufanyiwa ile huduma, angalau wiki mara mbili mpaka hapo itakapokuwa tayari ile hospitali au kituo kile kishamaliza.

Mhe. Spika, baada ya maelezo yangu hayo machache, na naamini serikali imetusikia nakushukuru na naunga mkono bajeti hii.

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Ahsante Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu na pia nakushukuru na wewe kwa kunipatia nafasi hii ya kuzungumza machache niliyonayo.

Mhe. Spika, kwanza niwapongeze wafanyakazi wa afya akiwemo Waziri na watendaji wake wote Unguja na Pemba, hiki ndio kioo cha wananchi na kila siku tunakisemea.

Mhe. Spika, nikianza mimi nitazungumzia Hospitali ya Chake Chake. Hospitali hiyo tunaita hospitali mama kwa sababu iko *center* kwa watu wote tunaotumia hospitali ile. Lakini nimwambie Mhe. Waziri tuna kilio kikubwa hospitali ya Chake Chake kwanza huduma, pili madaktari wa aina zote, kwa sababu ukiwa una matatizo lazima daktari umfuate nyumbani. Hiki ni kilio kikubwa cha kila siku, tunaomba tupatiwe madaktari ili kuweza kutuhudumia akinamama na watoto na hata wanaume nao ni wanadamu wanaumwa, akipindwa na mshipa akipelekwa pale daktari hayupo pengine anataka apate huduma za dharura haraka haraka hawezi kutibiwa.

Halafu niipongeze serikali kwa hii Hospitali ya Chake Chake kwa kupata vifaa, tukapata magodoro na mabetishiti ya kulalia wagonjwa. Napongeza kwa sababu ni jambo ambalo tulikuwa tukilipigia kelele siku nyingi, namuomba Mwenyezi Mungu atujaalie baada ya hicho kidogo tulichokipata kiweze kuongezeka zaidi ya hapo.

Hospitali ya Chake Chake niliizungumzia mara moja nayo kuhusu miundombinu. Miundombinu ya Chake Chake kwa wale watu ambao ni wagonjwa nayo pia ifikiriwe, kwa sababu kuna watu wenye miguu yao wanaweza kwenda pale, wakimtaka daktari na wakafika haraka, aliyekuwa mgonjwa hajui mlango gani apitie kumuona huyo daktari. Tunaomba Hospitali hii iweze kusadiwa kwa dhati kabisa.

Wenzangu nimewasikia wakizungumza hapa kuhusu madaktari wa mifupa. Madaktari hawa kama sisi watu wenye ulemavu na wale wanaopata ajali ni muhimu sana. Katika hospitali ya Chake Chake tunacho kitengo chetu cha watu wenye ulemavu, wanaohudumia watu kama hawa pale tuna daktari Shaibu, daktari Khamis, daktari Mzee wa Wete na hawa ni watu waliokuwa wamejisomesha, maana daktari Mzee ni wa siku nyingi na alichukua likizo bila ya malipo kwenda kusoma muda wa miaka mitatu, alirudi hivi karibuni.

Naiomba serikali watu kama wale waweze kuwatupia jicho kwa mafao yao ikiwa wanadai, mafao yao walipwe pamoja na mishahara. Kwa sababu ni watu wanaojituma sana, madaktari wanajituma, kukaa usimpe posho ni sawa

sawa na kutaka kumdhulumu ile roho yake na imani yake asiweze kuwasaidia wagonjwa. Maposho ni muhimu walipwe na mafao mengine.

Mhe. Spika, hapo hapo Chake Chake tuna kitengo cha maabara kiko Wawi. Ni kitengo muhimu sana kwa kuchunguza maradhi mbali mbali na tunakifuatilia sana. Lakini kitengo hiki kina kilio cha muda mrefu, wale wanaofanya kazi pale wana madai ya maposho yao hawalipwi kwa sababu gani na hawa tunawapa mzigo? Tunaiomba serikali iweze kujitahidi sana watu hawa kuweza kuwapa kipaumbele kwa sababu elimu na afya ni kitu kizito sana, huyu mwenye elimu ndiye huyu huyu anayekuja huko kwenye afya. Sasa tukiwadharau watu hawa itakuwa ni matatizo tena ni makubwa sana, na penye uzuri hapakosi na changamoto, Chake Chake changamoto zipo.

Changamoto za Chake Chake wajawazito wanapokwenda kujifungua wanapata matatizo, mama mjamzito akienda pale anachukua vifaa vyake vyote akiwa ni masikini hana basi anapata matatizo. Naiomba serikali kwa sababu vifaa vya kujifungulia ni muhimu, pale ukifika mpira unauziwa shilingi 2000, kitanda akishinda kutwa mama mjamzito au akilala alipe shilingi 2000, anunue jik, *gloves* na hata sabuni.

Mimi naiomba serikali haya mambo mengine madogo madogo waweze kujikita kuweza kuwapunguzia wananchi wao matatizo, yule mwenye uwezo atapeleka aliyekuwa hana uwezo asidhalilike. Halafu watendaji wetu wa kazi tukiwapa sifa wengine kweli wana sifa nzuri, lakini na wengine Mhe. Waziri akae nao, madaktari wengine ni majeure; anautizama uso wa mtu ndio amchangamkie, uso ukiwa umejifinya kidogo ameshafinya na yeye wake. Tunafanya nini, na muuguzi hadi awe na pembejeo juu ya mgonjwa, na mgonjwa ndio atakapopata faraja kwa yule anayemfanyia huduma. Tunaomba kwa sababu ukienda kwenye mahospitali ya wenzetu mgonjwa ni mali anawaniwa, kwa nini sisi tufanye kama hivi hapa Tanzania kwetu.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo nizungumzie Hospitali ya Mkoani. Kwanza naipongeza hospitali hii kwa miundombinu ya kufikia watu kama sisi. Hospitali ya Mkoani ni tambarare, unatembea vyumba vyote utakapoingia, lakini napo pana changamoto zake. Mimi hivi karibuni nilipeleka mgonjwa, labda iwe hii changamoto imeondoka kwa hii miezi mitatu. Ukifika pale ilikuwa unampeleka mgonjwa huduma ni tabu. Unataka maji atundikiwe mgonjwa unaambiwa kanunue nje ya hospitali. Ina maana hizi hospitali zetu hata yale maji ya dharura ikiwa umefika kwa muda pale hapana lazima tununue. Na kwa nini daktari akwambie kanunue kwenye hospitali ile pale. Anajua vipi yeye kuwa yale maji yapo, au ile hospitali wana-*deal* nayo yale maji kuwa pale yapo sisi tununue. Naomba madaktari hospitali ile kwanza ya Mkoani ni hospitali sisi tuliyoitegemea watu wa Pemba kama ndio hospitali yetu kuu ya mambo mbali mbali tunaikimbilia, huduma ziwepo.

Mwaka juzi hapa tuliilalamikia vyoo vilikuwa ni vibovu; mafunza, mambo chungu nzima, lakini yale yakarekebishwa. Tunaomba na haya mambo madogo madogo yaliyopo yarekebishwe, kwa sababu nimekwenda mimi kuangalia wagonjwa muda huu wa karibuni, vitanda ni vibovu, magodoro ni mabovu. Basi ikiwa magodoro ni mabovu hospitali tuweze kutafuta angalau yale magodoro tunayowapa watoto kwenda wakakaa *boarding*, tuweke mpaka tutakapopata mfadhili. Tumeshazoea kuwa wafadhili ndio watufadhili.

Lakini mimi nawapongeza sana kwa sababu ni watu wanaojituma, ni watu wanaohudumia watu, na vile vile na wao ikiwa watakuwa na matatizo ya kuwa hawapati mafao yao, watu hawa walipwe kuwaondolea matatizo madaktari ili tuweze kunufaika wananchi.

Mhe. Spika, wengi wamesema kuwa bajeti ya Waziri wa Afya ni ndogo, pesa hazitoshi. Lakini ukizitizama pesa kwenye mafungu, kuna mafungu yaliyokuwa si ya muhimu yana pesa nyingi, kuna mafungu yaliyokuwa ni ya muhimu yanakasimiwa pesa zake ni kidogo. Ikiwa itakuwa hii bajeti haitoshi basi irudishwe kwenye Kamati, wakaifanyie kazi Kamati kisha ndio ije tena, hilo si tatizo, ili kuweza kuwapa hawa wenzetu kipaumbele cha kuweza kupata bajeti itakayotosheleza, tusiwanyime. Kwa sababu hapa tulikuwa tukipiga kelele sana kwa bajeti ya Mhe. Zainab Omar Mohammed, alitwikwa mzigo, tukaja tukaitizama bajeti na yeye ni kidogo ikawa tunapiga makelele. Sijui muda huu ambao sikuwepo pengine yeye fungu lake liliongezwa, lakini tunasema bajeti hii ya Wizara ya Afya iweze kusaidiwa.

Mhe. Spika, halafu mimi nina kilio kikubwa cha Hospitali ya Mnazi Mmoja. Hospitali hii ni hospitali tunayoikimbilia sana sisi Waheshimiwa na hata wenzetu waliopewa rufaa kuja pale. Ni kwa sababu miundombinu ya pale ikawa si rafiki ya watu wengine. Ukienda pale ikiwa mgonjwa yupo juu ile lifti kwa nini ikiwa ni mbovu haitolewi tukawekewa nyengine. Kila siku mimi napiga kelele nikienda nikimtizama mgonjwa pale nina hamu

nimwone mgonjwa lakini namalizia chini kwa sababu miundombinu iliyopo si rafiki ya watu kama sisi. Tunaiomba sana Serikali miundombinu yote iwe inaweza kufanya kazi ili yapatikane yale mahitaji.

Halafu tunazungumza hapa kuwa kumeingia maradhi haya ya huyu mbu anayetafuna watu wakapata homa. Hapa palikuwa na mradi wa Malaria na walifanikiwa sana muhula uliopita Waziri wake alikuwa ni Mhe. Sultan Mohammed Mugheiry, Serikali iliyopita ya Awamu ya Sita na wakaweza kutokomeza kidogo maradhi haya ya malaria, lakini baadae amekuja kurithi babu yetu na yeye vile vile tunamshukuru sana mambo haya yamepungua kwa nguvu.

Sasa tunaiomba Serikali kupitia kwa Waziri na yeye aje atueleze hapa amefikia wapi kuweza kupata dawa ya mbu huyu angalau kinga ya kukinga watu wake, maana wameshaipata hii habari kuwa kuna mbu katili. Kwa sababu akiingia huyu kwenye nyumba atawaathiri watu wote. Kuna tabia ya kuwa watu hawatumii vyandarua hata ikiwa vimo ndani. Akimuuma huyu anaondoka anakwenda kumuuma mwengine na mwengine itakuwa nyumba nzima watu wanapata matatizo. Tunaomba Serikali kuwa makini, wenzetu tayari wanajipanga kutafuta kinga kwa mnyama huyu aliyeingia asiyejulikana kwao. Tunaomba na Zanzibar Serikali ilione, maana hatujui madhara yake ni ya kiasi gani na kwa muda gani.

Mhe. Spika, pia katika mahospitali tunaomba vyandarua, Hospitali ya Chake Chake haina vyandarua. Mimi naomba Mhe. Waziri hilo ulione wagonjwa wapate vyandarua. Kwa sababu maradhi yasikusumbue na mbu aliyekuwepo pale akakusumbua. Tunajua hospitali zetu hali zake zilivyo. Tunaomba Serikali itusaidie sana.

Mhe. Spika, kwa hayo machache nakushukuru na nawashukuru watendaji wote na naiunga mkono hotuba ya Waziri. Mwenyezi Mungu ajaalie maneno tuliyoyazungumza hapa atakabaliwe iweze kupata manufaa kwa kuweza kutusaidia. Ahsante.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Ahsante sana Mhe. Spika, awali ya yote kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia jioni hii kuweza kusimama hapa nikiwa mzima, lakini pia nichukue nafasi hii ya dhati kabisa kukushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia bajeti hii muhimu sana ya Mhe. Waziri wa Afya ambayo inamgusa na inamlenga mwananchi moja kwa moja.

Mhe. Spika, lakini pia nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Afya pamoja na watendaji wake kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kutekeleza majukumu yao, lakini kazi ambayo wanaifanya katika mazingira magumu mno ya ufinyu wa bajeti.

Mhe. Spika, bajeti wanayoingiziwa kwa kweli hairidhishi hata kidogo. Mhe. Spika, nimpongeze sana Mhe. Waziri pamoja na bajeti hii ndogo, finyu, lakini anajitahidi kutekeleza majukumu yake pamoja na watendaji wake.

Mhe. Spika, niiombe sana Serikali kama wenzangu waliochangia karibu wote wamesema kwamba huu uwasilishaji wa bajeti kuu kwa kweli ubadilishwe, baada ya kuchangia bajeti kuu ya Serikali mwanzo, basi sasa tuiweke mwisho kama wenzetu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanavyofanya.

Mhe. Spika, nasema hivyo kwa sababu inafika wakati tunachangia mambo ya msingi lakini matokeo yake hakuna linalokuwa. Kwa sababu bajeti kuu ya Serikali tayari imeshapita na hatuwezi kubadilisha mambo. Kwa hiyo mimi naiomba Serikali na pale Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ananisikia kwamba na sisi tuwe na utaratibu kama wenzetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Spika, nikiendelea nije katika Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja. Mimi niipongeze sana Wizara hii kwa kuona umuhimu wa kuifanya hospitali hii kuwa ya rufaa. Hili kwa kweli ni jambo la kawaida, wenzetu dunia nzima sasa hivi hakuna nchi ambayo haina hospitali kuu. Hii ni kwa sababu zile hospitali ndogo ndogo zinaposhindwa na mambo basi iwepo hospitali kuu ambayo iweze kutatua yale matatizo yanayoshindikana.

Sasa Mhe. Spika, nia ni nzuri sana ya Serikali ya kuifanya hospitali hii ya Mnazi Mmoja kuwa hospitali ya rufaa. Lakini inaonekana kwamba Wizara ilipoamua kuifanya hospitali hii kuwa ya rufaa mimi niseme kwamba pengine haikujitayarisha vizuri. Kwa sababu unapoamua kuifanya hospitali ya rufaa lazima uwe umejipanga, uwe na vifaa vya kutosha katika hospitali ile, lakini pia zile hospitali ndogo pia ziwe na madaktari wa kutosha.

Mhe. Spika, nasema hivi kwa sababu nina mifano ya kutosha. Hivi karibuni mimi nilipita Hospitali ya Mnazi Mmoja, kwa bahati pale mlangoni nikaona msongamano mkubwa wa wagonjwa. Nikauliza mbona wagonjwa wanazuiwa. Nikajibiwa kwamba wanazuiwa kwa sababu sasa hivi kuna utaratibu wa kwamba wagonjwa waende hospitali zao za karibu ili waweze kupata huduma na kuepusha msongamano katika Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Sasa Mhe. Spika, wagonjwa wale wale wanalalamika kwamba wanakwenda katika hospitali zao za karibu katika maeneo yao, lakini hatimaye wanapofika kule aidha daktari anakuwa hayupo, na kama daktari yupo basi inakuwa dawa za kutosha hakuna. Hatimaye basi mgonjwa yule inambidi arudi katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Mhe. Spika, hilo ni tatizo, nimuombe Mhe. Waziri haya mambo ayarekebishe ili tuwaondoshee wananchi wetu usumbufu.

Mhe. Spika, jengine hata hapo Hospitali ya Mnazi Mmoja mapungufu yapo. Hivi karibuni nilikuwa na mwenzangu mmoja alikuwa ana mgonjwa pale amelazwa. Sasa kwa bahati kukawa na vipimo anahitajika kuvifanya vidogo vidogo tu. Lakini hatimaye akaambiwa aende hospitali ya binafsi kwenda kufanya vipimo vile kwa sababu pale hakuna. Sasa Mhe. Spika, mimi naamini sote tunafahamu kwamba wagonjwa asilimia kubwa ambao wanapata matibabu pale katika Hospitali ya Mnazi Mmoja sio wote wenye uwezo. Sasa mgonjwa unapomwambia aende hospitali ya nje kufanya vipimo kwa kweli vinahitaji awe na pesa mfukoni. Sasa sidhani kama wagonjwa wote wana uwezo wa kuwa na pesa mfukoni kwa wakati ule.

Kwa hiyo Mhe. Spika, pamoja na kwamba bajeti ndogo, bajeti finyu, lakini basi hata vipimo hivi vidogo vidogo Mhe. Waziri vinatushinda. Hebu Mhe. Waziri jitahidi pamoja na bajeti ndogo lakini hivi vipimo vidogo vidogo tuweze kuvitatua. Hii Hospitali ya Mnazi Mmoja ni hospitali kubwa kwa Zanzibar, kwa hiyo ikiwa vipimo hivi vidogo vidogo havipatikani hilo ni tatizo. Naomba sana Mhe. Waziri jambo hili uweze kulitatua, na naamini kwamba Babu Duni ni msikivu sana na muelewa.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu nije ukurasa wa 61 katika mradi wa kupandisha hadhi hospitali za wilaya na vijiji. Mhe. Spika, mimi niipongeze sana Wizara kwa kupanga hii miradi mbali mbali ya kuhakikisha kwamba hospitali zetu zinahudumia wananchi wetu ipasavyo, lakini pia kupunguza malalamiko kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, pia matatizo yapo katika hizi hizi hospitali zetu ndogo ndogo ambazo za wilaya na vijiji. Nije katika Hospitali ya Mahonda. Hivi ninavyokwambia sasa hivi Mhe. Spika, Hospitali ya Mahonda ni kiza umeme umekatwa. Hata kama kuna mgonjwa atapelekwa wa *emergency* au mzazi anahitaji huduma basi atazalishwa kwa tochi. Sasa kweli Mhe. Spika, usalama utakuwepo kwa mzazi yule, kuna mzazi ambaye atazalishwa kwa tochi. Inawezekana kuwa zamani ilikuwepo hiyo, lakini mimi naamini Serikali tumepigania kwa nguvu zetu zote kuhakikisha kwamba mzazi anajifungua katika uzazi salama. Na uzazi salama ni ikiwemo mzazi kujifungua kwa taa ili mkunga anapomzalisha mwananchi yule aweze kumwona vizuri na kumhudumia ipasavyo.

Mhe. Spika, nimuombe Mhe. Waziri umeme ule uliokatwa katika Hospitali ya Mahonda akalipe ili wananchi wa Mahonda waweze kupata huduma kama inavyotarajiwa. Haya ndio yale yale niliyoyasema kwamba matatizo haya madogo madogo Mhe. Waziri ujitahidi kuyatatua.

Pia labda mimi nitoe wito kwa Waheshimiwa Wawakilishi. Waheshimiwa Wawakilishi tumepewa Mfuko wa Jimbo, sasa tunapoona katika majimbo yetu yanatokea matatizo kama haya tuyarekebishe tusingoje hospitali zetu zikakatiwa umeme, tuisaidie jamani serikali. Waheshimiwa Wawakilishi tusingoje Serikali tu tuokoe jahazi.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu nije katika ukurasa wa 10 Kitengo cha Huduma za Matibabu ya Macho. Mhe. Spika, nikipongeze sana kitengo hichi. Katika ukurasa wa 11 Mhe. Waziri anatwambia kwamba anashirikiana na Kitengo cha Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha cha Wizara ya Elimu, kumeanzishwa mpango maalum wa kuwafundisha walimu jinsi ya kuwapima wanafunzi wao uwezo wa macho kuona. Mhe. Spika, mimi niipongeze sana Serikali kwa kujua kwamba tuna wanafunzi wengi wana matatizo ya macho, lakini pengine wao wenyewe hawajitambui kama wana matatizo. Kwa hiyo kuamua kuwafundisha walimu kujua elimu ya macho kwa kweli wamefanya jambo zuri sana na ninaomba Mhe. Waziri mambo kama haya mazuri wawe wanayaendeleza.

Mhe. Spika, kwa kumalizia nije katika Kitengo cha Malaria. Mhe. Spika, Mhe. Waziri ametwambia hapa kwamba mradi huu wa kuondosha kabisa malaria wamefanya mipango mizuri na mahsusi kuwa sasa hivi wanawafikia wananchi nyumba hadi nyumba kwenda kuwacheki vimelea vya malaria.

Mhe. Spika, mimi niipongeze sana Wizara hii, kwa sababu sote tunafahamu kwamba wananchi huwa wana kawaida ya ukaidi. Sasa tunapowafuata katika majumba tukahakikisha kwamba tunawaangalia na tunawapima. Na ametwambia hapa katika kitabu chake kwamba asilimia ndogo sana ndio wamekuta wana vimelea vya malaria japo hawana dalili za malaria. Mhe. Spika, nipongeze sana lakini nimuombe Mhe. Waziri akaze buti kwa hili. Kwa sababu bado malaria yapo nchini kwetu pamoja na kuwa imepungua kwa asilimia kubwa, hata saa nyengine yapo matatizo yanatokea mtu anaweza kwenda hospitali ana dalili zote za malaria lakini anapopima anakutikana hana malaria.

Mhe. Waziri ingawa katika kitabu chako hichi umetwambia kwamba si kila homa ni malaria. Umetwambia hapa ulipokuwa unasoma. Lakini ukubaliane na mimi kwamba pamoja na ulivyosema hivi, kwamba sio kila homa ni malaria, lakini ninataka kukuhakikishia kwamba malaria bado ipo pamoja na kwamba imepungua kwa asilimia kubwa. Kwa hivyo nikuombe sana Mhe. Waziri ukaze buti kama ulivyotwambia kuwa mradi huu utaondosha malaria kabisa. (*Makofi*).

Mhe. Spika, kama nilivyosema awali kwamba mchango wangu utakuwa si mkubwa sana, kwa sababu ninaamini kwamba michango mingi imetolewa na Wajumbe, lakini kwa kuwa hii wizara ni muhimu sana kwa wananchi wetu na Taifa hili, kukaa kimya tu bila ya kusema neno lolote itakuwa sijawatendea haki wale walionichagua.

Baada ya hapo Mhe. Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Ahsante sana. Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Hamza Hassan Juma ambaye ninafikiri atatumalizia muda, lakini kama muda utakuwa umebaki kidogo basi Mhe. Rufai Said Rufai.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, na mimi nikushukuru kunipa nafasi hii nikaweza kuchangia wizara hii muhimu, wizara ambayo ndio kimbilio la wanyonge au la wananchi wa nchi hii.

Mhe. Spika, mimi ninataka nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri lakini pia na kumpa pole. Kwa sababu kwa kweli mjomba wangu huyu tumemtwika mzigo mkubwa sana na mzito kweli kweli. Tunaona namna gani yeye na watendaji wake wanavyojitahidi siku hadi siku kuweza kuboresha tiba kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, mimi nataka niwashauri wenzangu kwamba kuendelea kulaumu tu kila siku na kila pahala tutakuwa hatuitendei haki serikali yetu, lakini vile vile hatowatendea haki wananchi wetu. Sasa mimi nadhani wenzangu walionitangulia wamezungumza sana kuhusu ufinyu wa bajeti ya wizara hii. Kama tunajitambua kwa kweli kama wizara ambayo tunahitaji kuitetea kwa nguvu zetu zote iweze kupata pesa za kutosha, basi ni Wizara ya Afya.

Kwa sababu hii pamoja na ujanja wako wote, ukianza kupiga chafya tu basi kimbilio lako unakimbilia katika hospitali yetu au katika hospitali zetu hasa za serikali. Sasa kwa mara ya kwanza ninataka nimuombe sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, yeye ndiye kiongozi wa shughuli za serikali humu Barazani, lakini ndiye aliyekabidhiwa dhamana ya Mawaziri wote. Kwa hivyo ninarejea tena kwa mara ya kwanza ninamuomba sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, bajeti hii tuiahirishe irudi Jumatatu. Kamati ikakae tena, kwa sababu Mhe. Spika, nimejaribu kuangalia na hili nimelizungumza hata tulipokuwa kwenye Kamati ya Wenyeviti, tulipokuwa tunapitisha bajeti ya serikali kwamba mfumo tunaoendelea nao Zanzibar bado hautusaidii kuweza kuisimamia vizuri serikali. (*Makofi*).

Wenzetu Tanzania Bara mfumo waliouanza tumehisi umeanza kuisaidia serikali lakini umeweza vile vile kulipa Bunge kuisimamia serikali. Sasa tatizo kwamba bajeti kila mmoja anasema bajeti finyu lakini hatuna namna ya kuifinyua hii. Hii ndio imeshakuwa finyu, itakuwa finyu. Sasa utaratibu huu tutakwenda nao mpaka lini na wizara nyeti kama hii. (*Makofi*).

Mhe. Spika, mimi naomba pamoja na ufinyu wa hii bajeti kutokana na mfumo tuliokuwa nao, kwa sababu zipo wizara nyingi ambazo kuna shughuli tunaweza kuziakhirisha, fedha zikaingia katika bajeti ya Wizara ya Afya, tungeliweza kufanya hivyo. Lakini sasa kwa kuwa bajeti kuu ya serikali tumeshaipitisha na ile ndio *rubber stamp*. Kwa hivyo huku utacheza humo humo, humo ndani tu unamnyokoa huyu unamrejeshea huyu, lakini bado ufinyu wa bajeti unakuwa upo pale pale.

Mhe. Spika sasa mimi nilikuwa naomba kuna vifungu nimejaribu kuviangalia katika hii bajeti ya Wizara. Lakini kwa kuwa asubuhi nilikuwa sipo, lakini nilijaribu kumfuatilia Mhe. Mahmoud wote wawili walizungumza vizuri katika vifungu, walishauri vizuri.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu alizungumza vizuri katika vifungu na mimi nime-*quote* vifungu vingi humu, ingawa nilikuwa sijavimaliza ambavyo ninahisi kwamba tukiweza kwenda kufanya marekebisho, kuna fedha ambazo nyingi zipo katika utawala zikenda katika huduma.

Mimi ninaamini Mhe. Spika, wananchi wetu watapata huduma bora pamoja na ufinyu huu uliokuwepo lakini wananchi wetu watapata huduma bora. Yale mambo mengine ambayo kama wizara, watawala wanaweza kuyabana kidogo, na tumejaribu kuangalia kuna fedha nyingi tunaweza tukaokoa. Zaidi ya karibu si chini kwenye milioni 300 mpaka milioni 400.

Mhe. Spika, zipo, tumeshaziona ndani ya wizara hii. Sasa kama nilivyokuwa nasema na tunakubaliana na Mhe. Waziri kwamba mwakani hii bajeti ataileta mapema ili sasa tuanze kuchanganua, tuangalie je, katika zile programu ambazo zilizopewa vipaumbele, ili sasa tujue ni namna gani tunaweza tukaboresha huduma za afya kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, hili limetokezea kwa sababu gani. Hata mfumo wa vitabu vya bajeti safari hii, umekuja vipande vipande. Bajeti Kuu ya serikali tumeletewa *draft* ambayo iliyokuwa bado haijaandikwa kitabu. Lakini *draft* yenyewe ilikuwa kama ni *summary* na zaidi *total* ya ile bajeti kuu na zile wizara.

Kwa hivyo tulikuwa hatujui katika vifungu, katika wizara mbali mbali mwaka uliopita vilitengewa kiasi gani zikapatikana kiasi gani na mwaka huu zilitengewa kiasi gani zikapatikana kiasi gani. Kwa hivyo kwa kweli hata mfumo ule, kwa kweli unakuwa hautusaidii sana kuja kuishauri vizuri serikali.

Sasa mimi nadhani Mhe. Spika, ili lipate kuingia kwenye *hansard* na pamoja na vile walivyovizungumza wenzangu, nitajaribu kuvizungumza tu baadhi ya vifungu ambavyo nahisi tunaweza tukavifanyia marekebisho ili fedha zikaendelea katika huduma zaidi kuliko katika mambo ya Utawala.

Mhe. Spika, nilikuwa nimejaribu kuangalia katika ukurasa huu wa 24 wa kitabu cha bajeti. Kwa sababu Mhe. Spika, tukizungumza yote ya maneno hospitali gani, hospitali gani lakini mwisho inamalizia kwenye hii bajeti yenyewe. Lakini najaribu kuangalia katika vile vifungu ambavyo nilivyojaribu kuviangalia. Kwa mfano, kama kasma ukurasa wa 378 wa kitabu chetu cha bajeti, sio kitabu kile cha Mhe. Waziri alichokisoma, lakini nilikuwa najaribu kuangalia katika yale mafungu ambayo tumelikuwa tumeyapitisha.

Kwa mfano kama kwenye Hospitali ya Mnazi Mmoja. Kuna vitu kidogo vimenishangaza sana, sasa labda pengine Mhe. Waziri anaweza akaja akatusaidia maelezo baadae. Katika Hospitali ya Mnazi Mmoja katika hizi kasma 2205001 na kasma 220506. Hizi kwa muda karibu miaka mitatu kulikuwa kuna ziro ziro nyingi. Lakini hapa tumeekewa karibu bajeti ya milioni 74, vifaa vya kuandikia *stationery*.

Halafu kuna vifaa vya usafishaji, karibu milioni 93. Sasa vile vile Mhe. Spika, tukaja kuangalia kasma 220905 imetengewa milioni 162 ambazo ni chakula, ambazo mimi kwa hisia zangu nahisi hizi fedha ni kidogo, ambazo Mhe. Jaku Hashim Ayoub mara nyingi huwa anazipigia kelele masuala ya chakula katika hospitali zetu. (*Makofi*).

Sasa hapa ninaamini, tukiweza kufanya *reallocation* au kwa sababu sio *reallocation*, kwa sababu bado bajeti hatujapitisha, tukaweza kurudi, kamati ikaweza kurudi tukashauri baadhi ya vifungu waweze kupunguza fedha, ninaamini hoja ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub itakuwa haipo tena. Kwa hivyo kuna fedha nyingi Mhe. Spika, lakini vile vile nimeangalia kasma ya 26383 ambayo kuna karibu milioni 38, hizi pia tunaweza tukafanya marekebisho.

Halafu vile vile kuna eneo jengine, kwa mfano kwenye Idara ya Kinga kifungu 0601, kasma 263164. Hapa kidogo nimesikitishwa na sitokubaliana na kasma hii, kwa sababu mwaka uliopita zilitengwa karibu milioni 20 kwa ajili ya maradhi ya mripuko. Bajeti ya mwaka huu kuna ziro. Ina maana leo ikija ikitokezea maradhi ya mripuko tutakuja kufanya nini? Mhe. Maalim Saleh Nassor Juma alizungumza, alimsifu sana Doctor Kingwaba Mhe. Spika, nilikuwa sipo hapa Barazani, lakini akili, kiwiliwili, mawazo, fikra zote zilikuwepo Barazani. (*Makofi*).

Mhe. Spika, nilimsikia alivyomsifu Mhe. Doctor Kingwaba, na kwa kweli alikuwa ni mtu ambaye aliyejenga sana jina. Mimi mwenyewe hilo jina nilipokuwa mdogo nilikuwa ninalisikia tu kwa zile sifa. Lakini alizungumza kwamba aliweza kudhibiti maradhi ya kipindupindu kwa sababu fedha zilikuwepo. Sasa leo maradhi ya mripuko kuna ziro.

Sasa leo kumetokea dengue tu juzi, tafrani hapa. Je, leo hii tumeekewa ziro Mhe. Spika, sasa hii kidogo kasma hii sitoweza kuikubali. Kwa hivyo sio kama ninataka yaongoke baadhi ya mafungu yapunguzwe sehemu nyengine, lakini hata yale mafungu ambayo ninahisi muhimu hayakutiliwa fedha, yaingizwe. Kwa sababu mambo ya mripuko ni mambo ya *emergency*, wakati wowote inakuwa yanatokezea na Idara ya Maafa pesa hawana.

Mhe. Spika, lakini vile vile ninawashukuru katika Idara ya Tiba fungu 0701. Mwaka uliopita *overtime* ilikuwa ziro, safari hii alau wameekewa milioni 15. Haya ndio tunayoyataka kwa sababu daktari anapofanya kazi muda wa ziada, inabidi alipwe vizuri. Sasa ndio maana nikasema hii bajeti mimi nadhani na wala haitokuwa si ajabu wala aibu kurudi Kamati ikaenda ikakaa tuweze kufanya *adjustment* ili kuiboresha vizuri, kumsaidia Mhe. Waziri, lakini vile vile na wananchi wetu waweze kupata huduma zilizokuwa bora.

Lakini vile vile kuna kasma 220201 mwaka uliopita kulikuwa kuna milioni 1.8, safari hii kuna milioni 9, karibu laki tano katika suala la chakula na vinywaji na viburudishaji. Lakini vile vile kwenye eneo jengine kasma 220501 ambapo kulikuwa karibu milioni 13 mwaka uliopita, lakini mwaka huu kuna karibu milioni 12. Kwa hivyo bado zipo fedha Mhe. Spika, tunaweza tukazichezesha ndani ya bajeti hii hii ya wizara, tukaweza kusaidia sana kuweza kuboresha.

Vile vile katika Idara ya Uendeshaji na Utumishi, kuna suala kwenye posho maalum limeongezeka sana. Bajeti ya mwaka juzi ilikuwa ni milioni 200 na *something*, bajeti ya mwaka uliopita milioni 407 na bajeti ya mwaka huu bilioni 1 na milioni 23. Sasa maeneo kama haya tunaweza hapa tukapata katika fungu hili tu, tunaweza tukapata si chini ya milioni 22, tukaweza kui-*adjust* tukazipeleka katika maeneo mengine.

Mhe. Spika, katika maeneo ambayo niliyazungumzia hata Pemba katika Idara ya Tiba nimeangalia fungu 0801 Idara ya Tiba Pemba, nimeangalia kasma 220801. Mwaka uliopita walitengewa kama laki tano lakini mwaka huu kuna karibu milioni 21. Sasa ndio maana nikasema kuna fedha humu tunaweza tukazi-*adjust*, hazitoki ndani ya wizara, zitaingia ndani ya wizara lakini yale maeneo ambayo tumehisi ni *priorities* katika kujenga afya za wananchi yetu.

Mhe. Spika, kwa kweli nilikuwa ninaendelea kuangalia katika vifungu, na mimi hili tutawasaidia katika Kamati, na wala sisi wala hatuna haja ya kututaja twende nini. Lakini sasa kamati zetu Mhe. Spika, Mjumbe yeyote yupo huru kwenda kwenye Kamati kwenda kusaidia mawazo. Na Mhe. Spika, katika hili kwa kweli tutajitahidi tutawasaidia wenzetu ili kuweza kupanga vizuri vifungu, na wenyewe Wizara ya Afya kwa kuwa watakuwepo tutawauliza, je hii hamuoni ni muhimu zaidi kuliko hivi. Mimi ninaamini watendaji wao ni wasikivu, ni watu ambao tuliofanya kazi kwa mashirikiano ya pamoja. Ninaamini kwa kweli tutaweza kukubaliana sana katika hili.

Mhe. Spika, katika vifungu kama nilivyosema ninakubaliana na vifungu vile alivyovitaja Waheshimiwa wale niliowataja. Kwa hivyo vile vile viingie katika *hansard* ya kwangu vile vile. Hivyo sasa hivi naomba moja kwa moja niende katika michango ya jumla jumla.

Mhe. Spika, kidogo hapa nina masikitiko na mradi ambao Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, lakini pia na washirika wa maendeleo. Mhe. Spika, kwa kweli kuna mradi huu wa kuimarisha huduma za afya wilayani. Tena mimi ninashangaa sana na hili laiti kama ningelijua mwanzo, kwa sababu Tume ya Mipango ipo ndani ya wizara ninayoisimamia mimi, Afisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora. Lakini vile vile kwenye bajeti kuu ya serikali, mimi ndiye Mwenyekiti vile vile ninayesimamia wizara hizi,lakini vile vile Tume ya Mipango ipo kwangu.

Hili laiti kama ningelijua mwanzo Mhe. Spika, kwa kweli nisingekubaliana mradi huu ukafutwa. Mhe. Spika, kama tunavyozungumza hospitali zetu sasa hivi zina uhaba sana wa madawa na vitendea kazi mbali mbali na huduma mbali mbali. Mradi huu Wizara ya Fedha, samahani sio Wizara ya Fedha, kwa sababu hivi Mipango ipo Afisi ya Rais Ikulu, kwamba mradi huu tena tayari mradi upo karibu miaka miwili ambao wametia saini Wizara ya Fedha, Wizara ya Afya, lakini wametia saini washirika wa maendeleo.

Kwa hivyo kuna *memorandum of understanding* hii hapa Mhe. Spika, kutokana na muda sitoweza kuisoma. Lakini huku nyuma nikaangalia kuna saini mpaka za hawa washirika wa maendeleo, ambao wao wamekubali kusaidia kutoa huduma za afya vijijini, ambapo mradi huu kwa kuwa umefutwa. Kwanza tumekiuka MoU, tumekiuka ile *contract*, lakini vile vile kuna fedha karibu bilioni mbili ambazo zingeliingia katika kuimarisha huduma za afya katika wilaya zetu.

Leo hapa tunakwenda kui-*adjust* bajeti ili huduma zipate vizuri. Leo tunakwenda kuziacha fedha karibu bilioni mbili, nje ya bajeti, yaani hizi bilioni mbili nje ya fedha za serikali. Tena serikali humu wao walikuwa wachangie milioni mbili. Yaani imekuwa kama tumetega asali hapa, tumetega urimbo ili ndege anase. Serikali imeondoa kuchangia milioni mia mbili ili kupata bilioni mbili.

Mimi nadhani Mhe. Spika, hili suala sio sahihi na sijui watendaji wa Wizara ya Afya walipokwenda katika Tume ya Mipango, sijui walishindwa nini katika kuitetea hoja hii. Sasa Mhe. Spika, mimi naomba sana, na sijui tutafanya nini, kwa sababu Tume ya Mipango ile miradi yote ya maendeleo ya washirika wa maendeleo wameshaileta na tumeshaipitisha.

Sasa Waziri wa Fedha hayupo lakini Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Ikulu yupo ambapo Tume ya Mipango ipo mikononi mwake, tushakiuka mkataba na washirika wa maendeleo, tutafanya nini ili huu mkataba tuurudishe, ili kujenga imani kwa hawa, tena hawa wenzetu wakija kusikia kwamba bajeti ya Wizara ya Afya imepatiwa katika baadhi ya kasma imepatiwa asilimia 30, 25, lakini kuna fedha ambazo walikuwa wachangie wao, wamezuiwa, serikali imekataa. Mimi nadhani watakuwa hawatuelewi.

Sasa mimi ninaomba sana hili labda Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Ikulu na Mhe. Waziri wa Fedha siku hiyo vizuri akawepo na hizi *hansard* zetu, namuomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Waziri wa Fedha awepo, ili basi watusaidie kuna hoja gani ambayo serikali waliamua kuufuta mradi huu.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo vile vile niende katika tiba asilia. Mhe. Spika, hivi sasa katika matangazo mbali mbali, kuna matangazo ambayo yanatoka katika vyombo vya habari na tunaona kwenye televisheni vile vile.

Vituo vya tiba asilia sasa hivi vinazidi kama uyoga na hili mimi silipingi kwa sababu hata tulipokwenda China Mhe. Spika, kule tuliambiwa zile hospitali ambazo ni *herbalist* ziko nyingi kuliko hospitali za serikali, na kwa sababu zinatoa tiba nzuri. Kwa hivyo, na hapa kwetu sio kama tunawavunja moyo. Mhe. Spika, katika maswali na majibu niliwahi kumsikia Mhe. Waziri alisema kwamba kuna nyengine wanatoa tu matangazo lakini bila ya kukubaliana au bila ya kibali cha Wizara ya Afya.

Mhe. Spika, suala la afya Waziri wake hapa ni mmoja tu, ni Waziri wa Afya; na huyo ndiye aliyekabidhiwa na serikali, zinapotokea hospitali nyengine za tiba asilia kama uyoga, kama Waziri wa Afya hajazipa baraka zake basi Mhe. Spika, litakalotokezea kwa tiba watakayoipata watu wetu kule zikiwaathiri basi wale watakimbilia Hospitali ya Mnazi Mmoja au hospitali zetu za serikali.

Kwa hivyo, mimi naiomba serikali, nafikiri ile Bodi ya Madawa ina uwezo wa kufunga *pharmacy*, bodi ile sijui nguvu yake ikoje katika hizi hospitali binafsi na nani anatoa kibali cha hospitali hizi au nani anatoa leseni za hospitali hizi.

Hatuzikatai kama nilivyosema, lakini zirudi zisimamiwe na Wizara ya Afya. Mheshimiwa siku hizi kuna dawa kwenye chupa, hayo maradhi yaliyoandikwa wewe mwenyewe unavutiwa kwenda kuinunua, maana yake mlolongo wa maradhi unaweza ukasema, sasa hii tena hakuna haja ya kwenda kupima malaria na mambo mengine. Kuna mambo mengine wala huna haja ya kwenda kupima, ukiyaona tu unajua hapa sasa kidogo shughuli ndio hivyo, kwa hivyo zile dawa unaweza kuzisoma zikakuvutia, lakini je, dawa zile zenye mlolongo wa maneno mbali mbali, hakuna hata *TBS*.

Mhe. Spika: Hebu Mhe. Hamza Hassan Juma malizia kuna maneno mawili matatu ili tuyazungumze.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Haa! Du! Sasa Mhe. Spika, mimi nadhani hilo nimeeleweka, lakini pamoja na hayo nawashukuru sana Wizara ya Afya hasa kwa kutoa msaada kwa kituo chetu cha hospitali ya Kwamtipura na

ninawaomba waendelee. Waheshimiwa Wajumbe wengine basi waige mfano wa Kwamtipura. Jengine hospitali kubwa nzuri kama zile, ili wizara ivutiwe kuja kutoa huduma vile vile.

Sasa Mhe. Spika, kwa kuwa umeniomba nikupe nafasi na wewe kidogo, na kwa kuwa na mimi nilikuomba kwa unyenyekevu sana ukanipa, basi naomba nikupe hizo dakika na wewe uweze kutupa mambo mazuri.

Mhe. Spika, hotuba hii sisemi kama naikubali, kwa sababu nilimuomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais tuirudishie kwanza Kamati ikafanye kazi, Jumatatu tuje na wizara nyengine, ili tuje tumalize hiyo wizara tuiunge mkono. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Spika: Haya. Ahsante sana. Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kuna wazo hili kwamba ili kumsaidia Waziri wa Afya, pengine bajeti hii ingerudi kwenye Kamati, kuna wazo hilo. *(Makofi)*

Ila naomba nitahadharishe tu kwamba taratibu hazitaturuhusu kuja kufika pahala tukasema kwamba serikali iongeze fedha, ila ndani yake ya bajeti hii utaratibu huo unaweza ukafanyika. Sasa hili ni suala ambalo liko kwa upande wa serikali na hasa Wizara ya Afya namna walivyojipanga na vifungu vyao, tukiona jambo hilo linafaa basi tunaweza tukakubaliana hivyo, ili Kamati pamoja na Waziri wakae kupitia hivyo vifungu ambavyo tunaona labda kwa umuhimu wa huduma ya afya labda baadhi ya vifungu vinaweza vikarekebishwa. Lakini sasa jambo hili likifanyika inabidi wakati huo huo iwe tunakaa pamoja na watendaji wa Wizara ya Fedha.

Kwa sababu gani, kwa sababu hii maana yake tunarekebisha ule mfumo mzima katika Wizara hii ya Afya kuhusu zile kasma mbali mbali. Kwa hivyo, Wizara ya Fedha itabidi tuwe pamoja ili kile kitakachokubalika hatima yake basi na wao wawe na kumbukumbu, kwa sababu wakati wa kuja kutoa fedha katika mafungu hayo mbali mbali, itabidi iendane na hayo marekebisho ambayo itakuwa tumeyafikia.

Sasa labda nisikie tu kutoka kwa Mhe. Waziri wa Afya juu ya wazo hilo yeye anasema nini juu ya jambo hilo la bajeti hii kurudi kwenye Kamati. Na kamati yake bila shaka ni Kamati ya Ustawi wa Jamii. Wale ambao watakuwa na mawazo, wanaweza wakakaribishwa katika hiyo kamati. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwanza naomba niwashukuru Wajumbe wote waliochangia bajeti hii na kuona matatizo yalivyo. Pia naomba nikushukuru Mhe. Spika, kwa kuzingatia mawazo ya Waheshimiwa Wajumbe. Mimi sina pingamizi tukirudi kwenye Kamati pamoja na Wizara ya Fedha na wale Wajumbe wengi waliokuwa na mashaka ya baadhi ya vifungu, wakaja wakatusikia.

Mhe. Spika, nina tabia huwa nashindwa kuficha ukweli, naogopa nisitoke hapa nikawa na kinyongo, wakati ninalo la kusema ambalo ni sahihi. Tatizo sio ufinyu tu wa bajeti, tatizo ni kwamba zile 10 unazoniambia utanipa hunipi! *(Makofi)*

Sasa mimi sizalishi, mimi natumia. Ninapoambiwa kwamba 10 hazipo tunakuwekea 5, basi zile 5 nipewe. Kwa sababu naomba kukwambia Mhe. Spika, kwamba vifungu vyote vilivyoelezwa humu, nina maelezo ya kutosha kuvitetea na mkavielewa, lakini kwa sababu kuna nafasi ya watu kutusikia nje ya ukumbi, basi ni vizuri wakatusikia. Lakini ni mahali muchache sana ambapo tutaweza kushindwa kusema kwa nini hapo pana pesa hizo.

Natoa mfano mmoja tu Mhe. Spika, Mhe. Hamza Hassan kasema kuna bilioni 1 katika Utawala. Yale ni maposho yaliyokubalika ya Waziri, madereva na watumishi wengine wote liko pale kama posho ni sehemu ya mshahara. Sasa ukilikata lile, watakuja tena hapa wafanyakazi *allowance* zetu hatukulipwa. Kwa hivyo, ni suala ambalo tunaweza kulieleza kwenye Kamati.

Ninachoomba Mhe. Spika, Wizara ya Fedha iwepo kama kunarekebishwa vifungu virekebishwe, lakini ukweli utabaki hivyo hivyo; kwamba bajeti ya Wizara ya Afya ni ndogo na hatukatai kwamba serikali haina uwezo wa kutupa nyingi. Tunachokiomba jicho la rehema. Ahsante Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Acha tukubaliane kwamba bajeti hii irudi kwenye kamati, na siku ya Jumatatu sitomwita Mhe. Waziri kwa ajili ya kufanya majumuisho, badala yake siku ya Jumatatu asubuhi baada ya kipindi cha maswali na majibu, basi itakuwa ni zamu ya Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto. Sijui kama Waziri

yupo, basi tumpe taarifa kwamba siku hiyo ya Jumatatu ya tarehe 09/06/2014 asubuhi, yeye atakuwa anawasilisha, na tutaendelea mpaka kumaliza shughuli yake, baada ya hapo ndipo nitakapokuja kumuomba Mhe. Waziri wa Afya kuja kufanya majumuisho, chini ya utaratibu huo maana yake ni kwamba Mhe. Waziri wa Afya tunamtegemea afanye majumuisho siku ya tarehe 10/06/2014 jioni.

Kwa maana hiyo hapo katikati utaratibu wa Kamati mtakaa lini na lini, hiyo mtajipangia wenyewe. Mwenyekiti wa Kamati yupo, atazungumza na Waziri. Lakini tarehe 10/06/2014 jioni tutamtaka Mhe Waziri wa Afya afanye majumuisho, wakati huo wizara ile ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto itakuwa tumemaliza shughuli yake.

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya hayo basi niakhirishe kikao hiki mpaka siku ya Jumatatu, tarehe 09/06/2014, saa 3:00 barabara za asubuhi.

(Saa 1:51 usiku Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 09/06/2014)